ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni

16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/ Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
57.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 26 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Mohammed Mussa)) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 108

Ajira kwa watu wenye ulemavu

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Aliuliza:-

Bado utekelezji wa suala la ajira kwa watu wenye ulemavu kwa baadhi ya Wizara halijafikiwa.

Je, Mhe. Waziri ni Wizara ngapi ambazo zimeshatekeleza suala hili na hazijatekeleza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 106 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kweli inazingatia sana utekelezaji wa sheria namba 6 ya mwaka 2006 juu ya sheria ya watu wenye ulemavu kupata haki na fursa sawa chini ya kifungu cha 6, ambayo inakataza ubaguzi katika ajira kwa muajiri yoyote na pia kufanya sera ya ajira ambayo italeta ubaguzi kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti naomba nikiri mbele ya Baraza lako hili tukufu kwamba hakuna ubaguzi wowote katika utoaji wa ajira katika Wizara za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ni Wizara ngapi na watu wangapi wameajiriwa katika Ofisi na Wizara mbali mbali za Serikali, kwa hivi sasa takwimu hiyo hatuna, lakini tunashirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuona kwamba data hii inapatikana na itakapotikana tu tutampelekea Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kwa kuwa msingi wa suali hili ni watu walemavu kupata haki zao na huduma zao na kwa kuwa huduma ambazo wanastahiki watu walemavu wapate, ni pamoja na huduma ya kutumia majengo ya ghorofa. Na kwa kuwa mpaka sasa wajengaji wetu wengi ikiwa wizara au majengo mengine hayajazingatia miundombinu ya kuwawezesha watu wenye ulemavu kuweza kufikia juu ya majengo yale. Je, Wizara ina mpango gani wa kushajihisha taasisi mbali mbali zinazofanya majengo kuzingatia suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba tuna changamoto kwamba baadhi ya majengo ambayo yanatoa huduma za jamii kuweza kufikiwa na ndugu zetu ambao wana ulemavu hasa wa viungo. Mhe. Mwenyekiti kwa kuliona hilo Ofisi yangu kwa kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu hivi sasa inaifanyia mapitio sheria namba 6 ya mwaka 2006 kwa kuweza kuona ni jinsi gani Serikali itaweza kuwabana watu wote ambao wanajenga majengo ambayo yanakusudia kutoa huduma kwa jamii yaweze kupitika na watu wenye ulemavu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali lake, juu ya suali kwamba ni Wizara ngapi ambazo zimeshatekeleza suali hili na ngapi hazijatekeleza aliliarifu Baraza lako kwamba bado anaendelea kufanya utafiti na Wizara ya Utumishi juu ya kujua takwimu hizi.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa masuala kama haya huwa yanawasilishwa mapema siku 21 kabla ya kikao hiki, na kwa kuwa jukumu la Mawaziri ni kufuatilia masuala yale yanayopelekwa na kupata majibu kwa niaba ya wananchi. Je, Mhe. Mwenyekiti huoni Mhe. Waziri ameshindwa kutimiza wajibu wake katika shughuli yake hii kama Waziri anayehusika. Na zaidi ukizingatia suala la walemavu linasimamiwa na Wizara yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Salmin Awadh wa Jimbo la Magomeni swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti naomba nimkumbushe tena juu ya swali mama lilivyokuwa na jibu mama ambalo nimelitoa. Suali mama lilikuwa linauliza ni Wizara ngapi hazijatekeleza agizo la kuajiri watu wenye ulemavu na idadi ya watu ambao wameajiriwa katika Wizara mbali mbali.

Jibu nililotoa ni kwamba kwanza kabisa katika uajiri katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa maana ya Wizara na Taasisi za Serikali zote hakuna suala la ubaguzi wa watu wenye ulemavu alimradi nafasi imetokea inatangazwa, hakuna hadi hivi sasa malalamiko yoyote kutoka kwa watu wenye ulemavu kuja kwenye ofisi yangu kama wamenyimwa ajira kwa sababu ya ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, nilichokisema kama nitakileta hapa baadae ni idadi tu ya watu wenye ulemavu ambao wameajiriwa katika Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali, ambayo takwimu hiyo inachukua muda kuitengeneza kwa sababu inabidi ufanye *survey*, na yeye anajua kwamba *survey* si kitu cha haraka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana kwa kuniona. Kwa vile Mhe. Waziri amekiri kwamba Serikali hii haina ubaguzi kwa walemavu na tunawaona walemavu wengi hawana baskeli za magurudumu matatu, ni lini utanunua baskeli na kuwakabidhi wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Muyuni kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti naomba nikiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba, visaidizi ukiacha baskeli anazozizungumzia kwa sababu ulemavu uko wa aina mbali mbali bado ni changamoto kubwa inayotukabili ndani ya jamii yetu. Hivi sasa kwa mara ya kwanza kabisa katika bajeti ambayo nitaiwasilisha Mhe. Mwakilishi atasikia ni jinsi gani Serikali inajali kuwapatia visaidizi watu wenye ulemavu, kwa mara ya kwanza tumetenga fungu japokuwa halitakuwa kubwa lakini litatusaidia. Lakini vile vile jitihada mbali mbali za kuwasaliana na wafadhili ambao mara nyingi wamekuwa wanatupa misaada na wafanyabiashara, vile vile kwa ajili ya kuwapatia walemavu visaidizi vinaendelea kuchukuliwa na ofisi yangu.

Nam.57
Ujenzi wa Bandari Mpigaduri

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Aliuliza:-
Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeeleza nia ya kujenga bandari mpya ya kisasa katika eneo la Mpigaduri, Mjini Zanzibar.

a) Pendekezo hilo limeshafanyiwa kazi kiasi gani na imefikia hatua ipi.
b) Mradi huo mkubwa unategemewa kugharimu kiasi gani
c) Fedha hizo zinategemewa zitatoka wapi na zina masharti gani.

Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mji mkongwe swali lake namba 57 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina nia ya kujenga Bandari mpya ya kisasa katika eneo maarufu kwa jina la Mpigaduri.

a) Mhe. Mwenyekiti, pendekezo hilo linaendelea kufanyiwa kazi, na kwa muda huu Serikali imeshakamilisha pembuzi yakinifu uliofanywa na kampuni ya *CRB* ya China. Hata hivyo baada ya upembuzi yakinifu huu kuletwa Wizarani kwetu, na baada ya kuipitia kwa kina uchambuzi huu, Wizara kupitia wataalamu wameona kwamba gharama iliyopendekezwa na kampuni hii yaani kiwango cha USD 800 milioni ni kingi sana, na hivyo na bado Serikali imo katika kutafuta njia mbadala ya kufanikisha suala hili.

b) Kwa gharama ambazo zinakisiwa kulingana na *Concept paper* ya Wizara, mradi huu usingeweza kuzidi USD 400 milioni. Hata hivyo kwa vile gharama hizo zilikisiwa kipindi cha miaka 5 iliyopita tungeweza kuweka ongezeko la asilimia 10 ambapo mradi huu usingeweza kuzidi shilingi USD 500 milioni.

c) Fedha bado hazijapatikana na hivyo masharti ya fedha yasingekuwa tayari kupatikana.

Hata hivyo matumaini ya Serikali yetu kwamba fedha hizo zitapatikana kwa njia ya mkopo au msaada kutoka kwa wahisani na washirika wetu wa maendeleo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

a) Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba anieleze kwamba kutokana na majibu yake kampuni ya *CRB* inaonekana imetoa makisio ambayo ni zaidi ya mara mbili kile ambacho kinadhaniwa kwamba kingekuwa ni gharama halisi kutoka dola 400 milioni zilizokisiwa na Wizara hadi dola 800 milioni.

   Swali langu ni kwamba ikiwa hivyo ndivyo, kampuni hii ina uadilifu na uaminifu kiasi gani na kwa nini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapenda kuitumia katika miradi yake mingi.

b) Hii bandari inayokusudiwa kujengwa ningemuomba Naibu Waziri atusaidie inategemea kuchukua meli ngapi katika hiyo *concept paper* ambayo imeandaliwa, kwa sababu kuna mazungumzo huku nje ni kwamba pamoja na maelezo mengi tunayopewa kwamba itakuwa bandari ya kisasa na itakuwa ya aina yake katika ukanda wa Afrika Mashariki, upande wa magharibi ya bahari ya hindi tunaambiwa kwamba imekusudiwa isichukuwe zaidi ya meli tatu kwa wakati mmoja.

   Naomba atupe maelezo inakusudia kuchukua meli ngapi wakati mmoja kwa mujibu wa hiyo *concept paper*.

Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b)
kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kampuni ya CRB ni kampuni ya China na ndiyo kampuni ambayo tulikuwa tumeingia nayo makubaliano ya awali ya kutufanyia tathmini na uchambuzi yakinifu kuhusiana na suala zima la ujenzi.

Taarifa anazozisema Mhe. Mwakilishi kwamba gharama hizi kuongezeka mara dufu kutoka shilingi milioni 400 mpaka milioni 800 waliokuja nazo, pengine inawezekana ikawa kuna *factor* nyingi kuwepo kupanda kwa gharama, lakini pia inawezekana ikawa vitu walivyoviongeza ikawa zaidi ya vile ambavyo tuli-*demand* sisi pale awali katika ile *study* waliyokuwa wakiifanya.

Lakini hata hivyo baada ya Serikali kupitia kwa kina tumeona kwamba gharama hii ni kubwa, na kwa sababu kuna baadhi ya vitu sisi kama Serikali tungeona kwamba tunaweza kuja kuvifanya kwa muda wa baadae.

Kwa msingi huo sina hakika na uwezo wa kampuni hii kusema kwamba si waadilifu. Sisi kama Serikali kwa kazi waliyotufanyia tumeridhika nayo, isipokuwa suala la gharama hatujakubaliana nao.

b) Mhe. Mwenyekiti, bandari inayotarajiwa kujengwa pale ni bandari yenye kiwango cha kuitwa *harbor port*, bandari ya *harbor port* ni bandari ambayo inakuwa kubwa zaidi kutoka katika bandari zile za kibiashara.

Matarajio yetu bandari hii tutajenga kwa *phase* hadi kukamilika kwa *phase* zake zote tatu itakuwa ina uwezo wa kuegesha mpaka meli tano. Lakini katika mipango yetu ya ujenzi hatutoweza kujenga zote *stage* tatu kwa wakati mmoja, tutakwenda *stage* kwa *stage*. Mategemeo yetu kwamba katika hatua ya awali tuna uwezo wa kuegesha meli mbili mpaka tatu na wakati huo utaratibu wa ujenzi ukawa unaendelea. Matarajio yetu bandari ikikamilika yote itakuwa na uwezo wa kufunga mpaka meli tano kwa kuzingatia ukubwa wa meli husika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri katika jawabu ulizojibu fedha hizo hazipo huoni hii ni ndoto ya usingizini kuota usingizini ukawa tajiri, baadae ukaamka asubuhi ukawa huna pesa. Hii imekuwa ni kawaida yako Mhe. Naibu Waziri. Kwa nini Serikali huwa inapanga mipango mikubwa wakati uwezo haupo huku si kutiana mchanga wa macho.

b) Ni sababu zipi zilizopelekea Wachina kupewa kazi muda mrefu huoni itakuwa kama tatizo la uwanja wa ndege kuacha njiani kutojengwa tena huu.

Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana namuomba Mhe. Mwakilishi arudie swali lake (b) sikulisikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Alijibu katika jawabu lake Serikali bado haijapata fedha kwa ajili ya bandari hiyo. Haoni hii ndoto ya usingizini kuota usingizini, una pesa ukaja ukaamka asubuhi ukawa huna pesa. Kwa kuwa Serikali inapanga mipango mikubwa wakati uwezo wenyewe haupo huku si kutiana mchanga wa macho.

Ni sababu zipi zilizopelekea Wachina kupewa kazi wakati uwanja wa ndege haujamalizwa uliopo pale hawatokuja kuingia mitini hawa.

Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa Serikali katika miradi mikubwa kama hii cha kwanza kinachofanya Serikali ni kuandaa *concept paper*, baadae kufanya upembuzi yakinifu ili kuwa na mradi kamili. Baada ya kuwa na mradi kamili ndipo pale Serikali inapofanya mipango kutafuta fedha. Maelezo aliyoyatoa Mhe. Mwakilishi nadhani anategemea miradi midogo sana, ndio Serikali ina uwezo kujipanga kutafuta fedha kabla baadae ndio wakaone gharama halisi ya mradi husika.

Mimi imani yangu kwamba mipango ya Serikali katika hii iko vizuri kwa maana kwamba tumefanya *study* baada ya kujua gharama ndio Serikali ihangaike kutafuta fedha. Na katika jibu langu mama nimeeleza wazi kama matarajio ya Serikali fedha hizi aidha zitapatikana kwa mkopo au msaada kutoka kwa wahisani na washirika wa maendeleo.

Jibu (b) Mhe. Mwenyekiti, tulichokizungumza hapa Kampuni iliyokuwa ikifanya kazi ni kampuni ya CRB asili yake China. Kama kuna mgogoro au kama kuna tatizo na kampuni ya China haimaanishi kuwa kila kampuni ya China itakuwa *disqualified*. Kazi hii ambayo tumeifanya na Wachina imekwenda vizuri, matarajio ya Serikali yamefikiwa, changamoto iliyojitokeza katika suala la gharama kwamba ni kubwa kwa wakati huu.

Kampuni nyengine za China zinazotufanyia bado Serikali inaridhika nazo na ndio maana tukashindwa hatujavunja nazo mkataba tunaendelea nazo na kazi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake alitwambia kama Serikali inakusudia kwenda kwa *phase* katika kujenga bandari ya Mpiga duri, na akatwambia kama *estimate* waliyoileta kampuni ya kichina ni dola milioni 800. Swali langu lipo hapa, dola hizi milini 800 ni kwa *phase* zote au ni kwa phase ya kwanza.

Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, gharama hizi zingeweza kwa phase ya kwanza kulingana na mchoro na mahitaji ya ujenzi wa bandari husika.

Nam.70

Uhaba wa Walimu wa Sayansi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aliuliza:-

Wanafunzi wa Skuli mbali mbali katika Jimbo la Muyuni wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa walimu wa sayansi jambo ambalo linachangia kuzorotesha maendeleo ya wanafunzi katika masomo hayo.

a) Je ni sababu gani zimepelekea hadi sasa Serikali kutoondoa tatizo hilo.
b) Kwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali aliahidi kulipatia ufumbuzi tatizo hilo, ni sababu gani zimempelekea kushindwa kutekeleza ahadi yake hiyo hadi sasa na wanafunzi kuendelea kuathirika na tatizo hilo.
c) Kukosekana kwa walimu hao Serikali haioni kuwa ni miongoni mwa sababu zinazopelekea wanafunzi wa kidato cha nne na sita kufanya vibaya mitihani yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Muyuni swali lake namba 70 lenye a, b, na c.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Skuli ya Muyuni na Skuli nyengine nyingi zina uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi. Uhaba huu unatokana na idadi ndogo ya wanafunzi wanaofaulu masomo ya sayansi katika mitihani ya kidato cha nne na kidato cha sita, na hatimae kujiunga na mafunzo ya Ualimu na kuongezeka kwa Skuli za Sekondari. Wengi wa waombaji wa mafunzo ya ualimu wanafaulu katika masomo ya sanaa kuliko sayansi. Hata hivyo Wizara imeandaa mafunzo ya Ualimu kazini kwa walimu wasio na sifa za kufundisha masomo ya sayansi ili kuinua uwezo na hatimae waweze kumudu kufundisha masomo hayo.

Pia Wizara imeajiri vijana waliomaliza kidato cha sita na kufaulu masomo ya sayansi ili kusaidia kupunguza uhaba wa walimu wa sayansi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Jaku kama ifuatavyo:-

a) Uhaba wa Walimu wa Sayansi katika Skuli zetu unatokana na wanafunzi wengi kutofaulu masomo ya sayansi katika mitihani ya Kidato cha Nne na cha Sita, na hivyo kupelekea vijana wachache tu ndio wenye sifa za kujiunga na mafunzo ya ualimu kwa masomo ya sayansi.

b) Ni kweli kuwa Wizara iliahidi kulipatia ufumbuzi suala hilo, lakini ufumbuzi wake hauwezi kupatikana mara moja na unahitaji muda wa kutosha kuweza kulitatua tatizo la upungufu huu. Wizara imepata vibali vya kuajiri walimu wapya. Katika mwezi wa Aprili, 2012 Wizara iliajiri walimu 197 wenye shahada na stashahada mbali mbali wakiwemo walimu wa masomo ya sayansi. Katika mwezi wa Juni, 2012 Wizara imepata kibali chengine cha uajiri wa walimu 111 wenye shahada na stashahada ya ualimu wakiwemo walimu 48 wenye shahada ya masomo ya sayansi.

   Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhakikisha kuwa walimu wote wanaomaliza mafunzo hasa masomo ya sayansi na hesabati, wanaajiriwa ili kuondoa upungufu wa walimu hao unaokabili skuli zetu. Napenda pia kumuahidi Mhe. Mwakilishi baadhi ya walimu wapya tutampangia katika skuli yake na skuli nyengine zenye upungufu wa walimu wa sayansi.

c) Kukosekana kwa walimu hao kunawezekana kuwa ni moja ya sababu inayochangia kushindwa kwa wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao ya kidato cha nne na kidato cha sita. Lakini pia sababu hiyo haitoshelezi peke yake. Sababu nyengine zinazoweza kuchangia kushindwa kwa wanafunzi ni wanafunzi wenyewe kutopenda kusoma masomo ya sayansi kwa dhana kuwa masomo haya ni magumu au wanafunzi kuogopa somo la hesabati ambalo ndio msingi wa masomo mengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hili suala limekuwa la muda mrefu linapigiwa kelele na katika majibu alivyokuwa akijibu itakuwa ni miujiza hii Mhe. Naibu Waziri, walimu wa sayansi hawapo na wanafunzi wanasoma sayansi na wanapasi watatu, wanne hii ni miujiza mikubwa Mhe. Naibu Waziri. Hebu tueleze tatizo hili litamalizika lini na katika walimu hao 111 na 197 ni sababu gani walimu hao kutopatikana Kitogani, Pete, Jambiani, Bwejuu na Muyuni huu si ubaguzi Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili litamaliza lini, Wizara tunajitahidi kwa upande wetu kama ambavyo nilizungumza kwenye jibu langu kwamba kuna mafunzo tunatoa kwa walimu, ili angalau kuwapa uwezo wa kuweza kusomesha. Lakini pia kama nilivyozungumza tumeajiri walimu wa form six. Lakini kama haitoshi *SUZA* imeanzisha diploma ya sayansi, lakini pia imeanzisha darasa la form five na form six la sayansi ili wanafunzi wataotoka pale basi tuweze kuwaajiri, lakini vile vile wale ambao watakuwa na uwezo wa kuingia Chuoni basi waweze kuingia Chuo Kikuu.
Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hilo kuna skuli mpya hizi ambazo tumejenga, skuli hizi Mhe. Mwenyekiti, zitakuwa na maabara ya kutosha kwa ajili ya masomo ya sayansi. Kwa hivyo hizi skuli pia nadhani zitaweza kuwashawishi watoto wetu waweze kupenda masomo ya sayansi. Lakini na sisi si kwa Wizara tu na wazee pia tuwahimize watoto wapende haya masomo ya sayansi. Mzee ana uwezo wa kumtizama mtoto wake pasi ambazo kapata na akaweza kumshawishi kwa pasi hizi wewe usiende *art* nienda sayansi. Kwa hivyo si suala la Wizara tu lakini ni suala ambalo tunatakiwa na wazee pia tushirikiane. Kuwa Wizara ina ubaguzi Mhe. Mwenyekiti, sidhani. Kwa sababu siku zote kupanga ni kuchagua, kuna chururu na kuna ndondondo. Tatizo la walimu wa sayansi si tatizo la skuli ya Muyuni tu, ni tatizo la Zanzibar nzima, Tanzania nzima na Dunia nzima.

Kwa hivyo tunatizama na pale palipokuwa taaban, ndio walimu tunaopata kuwaajiri tunawapeleka, na pale palipokuwa afadhali tunatizama kwanza kuondoa kule kulikokuwa kuzito na baadae kule kama ambavyo nimekuahidi, hawa wa kwanza tumepeleka huku kulikokuwa hakuna kabisa.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti kwanza ninashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna tatizo kubwa la somo la sayansi hapa Zanzibar kwa muda mrefu, na kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu, ni miaka mingi imeanzisha mchipuo kwa ajili ya kuwalea wanafunzi wetu kimasomo. Je, Mhe. Naibu Waziri, wanafunzi hao wa michipuo mnawalea vipi kwa kipindi cha *form one* mpaka *form six*, mpaka ikabidi tatizo hili la somo la sayansi Zanzibar liwe ni sugu. Hiyo ni (a).

(b) Mtajitayarisha vipi hivi sasa kwa kupitia wanafunzi wa michipuo kuliondoa kabisa tatizo la somo la sayansi Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Mwakilishi Mohammed wa Jimbo la Chambani swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

Ni kweli kama alivyozungumza Mhe. Mwakilishi kama tulianzisha madarasa ya michipuo wa sayansi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tatizo ambalo tunalo wanafunzi wetu wanapomaliza kazi kama unavyosema tunawalea mpaka wanamaliza *form six*. Lakini wakimaliza *form six* wanachagua kazi, hawataki kwenda kwenye ualimu. Hizi nafasi ambazo tumetoa sisi za ajira basi katika walimu 200 ambao tulitaka tuwaajiri ni walimu hawa ambao nimewataja ambao walijitokeza kuomba na hawa walimu 111 tuliopatiwa kibali pia cha kutaka kuwaajiri mpaka sasa hivi hatujatimiza hawa walimu. Na wapo ambao wana sifa lakini hawataki kusomesha. Kwa hivyo hili pia ni jukumu letu Wawakilishi kuzungumza na vijana wetu wawasaidie watoto wetu na ndugu zetu, kwa sababu na wao pia wamesomeshwa na serikali hii. Kwa hivyo ni wajibu wao na wao sasa kwa vile wamesomeshwa basi na wao wawasomeshe wenzao.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwamba bado ana upungufu wa walimu wa sayansi katika wizara yake, lakini pamoja na upungufu wa walimu hao aliokuwanao atakubaliana nami kwamba hakuna uwiano mzuri wa walimu hao wachache waliopo katika skuli.

Pili, atakubaliana nami kwamba Skuli ya Sekondari ya Nyerere ina mwalimu mmoja tu wa sayansi ambayo ina madarasa kuanzia *Form 1 – Form IV* na ambapo tunategemea kufanya mitihani ya sayansi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikubaliane na Mhe. Salmin moja kwa moja kuwa ni kweli, licha ya kuwa tuna tatizo la walimu wa sayansi lakini skuli zetu hazina uwiyano. Hilo tumeliona kama wizara na tumeanza kulifanyia kazi. Kuna skuli nyingi za mjini ambazo zilikuwa zina walimu wamerundikana tu, kwa hivyo tumeanza kuwahamisha na kuwagawa katika skuli nyengine.

Suala la Skuli ya Nyerere ni kweli taarifa ninayo na tutahakikisha katika mgao huu basi na wao pia tunawaongezea walimu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na majadiliano ningependa kuchukua nafasi hii kukuarifuni juu ya ujio wa wageni ambao tunao siku ya leo hapa. Tuna wageni kutoka Manispaa ya Iringa ni Madiwani hawa ambao wanaongozwa na Naibu Meya, Karvas Mbage. Ahsanteni sana.

Lakini pia tuna watendaji Ndugu Gress Mbilingi, Ndugu Fidya Nakomandu, Ndugu Sima Gimboleki na Ndugu Asha Kitagole. Pia tuna viongozi wa msafara kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi ikiongozwa na Ndugu Ali Abdalla Said, Ndugu Iddi Mbarak Uledi, Ndugu Mwanaidi Ame Moh.d. Ahsanteni sana.
Waheshimiwa Wajumbe hapa nilipo nina orodha ya wachangiaji 13 na muda wetu tulionao naona ni mdogo kwa sababu jioni tunataka kufanya majumuisho katika shughuli yetu hii ya leo. Kwa hivyo, basi naomba tukubaliane basi kwamba Wajumbe watakaokuwa wamesimama watumie muda usiozidi dakika 15 katika kuchangia kwao ili kila mtu aweze kupata nafasi ya kuchangia.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 43 wa Kanuni Kifungu Nam.5 (6) kinaeleza kuwa katika kuchangia Mjumbe atachangia dakika zisizozidi 20 kwa ile mikutano ya Baraza la kawaida lakini katika Bajeti zisizopungua 30. Na ikibidi kama Mhe. Spika, ataona kuwa iko haja anaweza akaongeza mpaka dakika 10.

Mhe. Mwenyekiti, tunajadili bajeti ya serikali na hii ni wizara ya Makamu wa Pili wa Rais inagusa wizara zote na ni mambo makubwa sana. Kwa sababu hiyo naomba moja kwa moja tufuate kifungu hiki cha Kanuni ili tuweze kuichangia bajeti hii vizuri ipasavyo kwa manufaa yetu na taifa kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe uliyoyazungumza ni sahihi na ndivyo utaratibu wa Kanuni unavyotuongoza, lakini lazima tuzingatie vile vile kwamba pamoja na kuwa utaratibu unatutaka tuchangie katika dakika hizo ambazo zimeoneshwa katika Kanuni, nilisema kwamba jana tulianza na watu 12 na leo mpaka dakika hii tuna watu 13 wa ziada, tukiwagawa hao nafikiri mwenyewe katika hesabu zako wakati wewe ni maalim wangu utakuwa unaelewa muda ambao tutakuwa tunautumia wa ziada katika hili. Utaratibu uliokuwa umepangwa leo ni siku ambayo inatakiwa kutolewa mchango lakini vile vile na kuweza kufanya majumuisho katika utaratibu ambao umeelekezwa kwa mujibu wa *schedule* ambayo sote tumekabidhiwa.

Kwa misingi hiyo basi, ndio maana nikachukua fursa hii kuwaomba Wajumbe kwa sababu michango yenyewe inayokuja ni ile ile ya kujirudia ndio maana tukasema kwamba tujitahidi basi na angalau wale ambao watakuwa wanachangia wasirudie rudie yale yale ili na wenzao waweze kupata nafasi ya kufanya hivyo. Tulikuwa tunajua kwamba Kanuni inaelekeza hivyo na tunaheshimu Kanuni. Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Kwa kuendelea tunaomba tumalizie dakika tano kwa Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nitumie fursa hii kueleza ile sababu yangu ya mwisho ya kwa nini kuwa siutaki Muungano huu uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba lazima tukubali kuwa sasa ulimwengu mzima una *advocate* mambo ya demokrasia na utawala bora. Naamua nitoe sababu hii lakini kabla ya kumalizia nianze kuomba radhi wana Afroshirazi wenzangu, nalizimika kutoa sababu hii ya mwisho ya kuukataa Muungano huu kama ifuatavyo:

Kwamba sisi mwaka 1964 Afroshirazi tuliikomboa nchi hii kwa Mapinduzi tukiongozwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Karume tulimchagua wana Afroshirazi kuwa Rais wa Afroshirazi, hatukumchagua Mhe. Karume kuwa Rais wa Wazanzibari. Tuliingia kwenye Mapinduzi tukashinda Afroshirazi kwa hivyo Mhe. Karume alikuwa na *legitimacy* ya kuwasemea Afroshirazi, alikuwa hana *legitimacy* ya kuwasemea Wazanzibari katika kipindi kile. Lakini kwa sababu tuliingia kwenye Mapinduzi ndio mambo yakaenda yalivyokwenda.

Kwa hivyo, nasema kwamba kwa hali ya sasa na ulimwengu ulivyo hivi sasa ni kuwa tunazungumzia Utawala Bora, demokrasia kwa hivyo Muungano uliopo ulikosa uhalali pale kwa sababu hatukushauriwa sisi Wazanzibari na Mzee Karume amekaa ameingia bila ya kutushauri kwenye Muungano ule na kwa yeye kwa sababu hakuwa *Elected President* kwa hivyo *legitimacy* ilikosekana. Hii ndio sababu yangu ya mwisho Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nije katika maafa. Mhe. Mwenyekiti sisi siku zote serikali yetu sio sikivu, maumbile sio bahili katika kugawa vipawa, tumepewa masikio tusikie, tumepewa mdomo tusemee, tumepewa miguu tutembelee Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha sisi tunapiga kelele hapa kuiambia serikali kwamba ni bora kinga kuliko tiba, ni bora kukinga kuliko kutibu. Leo serikali inajitayarisha yatokee maafa iende ikasaidie tu, maafa ya nchi hii lazima tujitayarishe kukinga na kukinga ni pamoja na kununua meli. Bajeti sijaiona mimi kuzungumzia meli mpya ya serikali hapa, labda tukishakufa ndio uone panakodiwa helkopta, panafanywa nini, jamani ni bora kukinga kuliko kutibu.

Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, serikali ina viongozi wasikivu, wenye akili tambuzi, wenye mawazo mazuri, waadilifu katika maneno na makini sana katika kutenda, hebu wasikilize huu ushauri wetu kwamba serikali isijitayarishe kwa kupambana na maafa tu ijitayarishe kukinga maafa, iwasikilize wataalamu. Hivi sasa tuko katika matatizo ya mabadiliko ya tabia ya nchi tunaambiwa kisiwa kile cha Ksiwa Panza karibu kitazama kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Hivi sasa wataalamu wanatwambia Chuo chetu Kikuu pale *SUZA* kuna programu ya yule *Vice Chancellor Prof. Idrissa Rai* ana programu anataka kuanzisha ya *degree* ya mwanzo ya mazingira ili kupata wataalamu wa kuweza kupambana na haya mabadiliko ya tabia ya nchi, leo hajawezeshwa mwaka wa ngapi pale chuoni kufungua programu hiyo ya mazingira. Kwa hivyo mtusikilize sisi jamani mmepewa masikio na Mwenyezi Mungu kawapa vitumieni vipawa hivi mlivyopewa katika kusikia, kufikiri na kutoa maamuzi baada ya ushauri wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwamba Wazanzibari tuko katika kipindi hiki cha kushikamana zaidi kuliko kutengana. Tume inakuja hii ya kuratibu maoni kuhusu katiba mpya, nawaombeni sana tuacheni itikadi zetu za kisiasa, tuacheni tofauti zetu za kidini, tuacheni tofauti zetu za kimila na silka tuungane pamoja itakapokuja tume hii twende tukatoe maoni yetu ya kuwa namna gani tunataka Tanzania iwe na namna gani Wazanzibari tunaihitaji Zanzibar mpya.

Mimi Muungano siutaki lakini nyinyi mawazo yenu wananchi mtakayotoa nawahakikishia basi sisi tutayasimamia hayo msiwe na shaka. Huwezi kwenda Pemba kwa miguu narudia, lazima upande boti, jahazi, mashua au ndege ndio ufike Pemba. Hiyo dhamira yenu ya Zanzibar mnayoitaka chombo pekee cha kupanda ndio hiyo tume inayokuja. Kwa hivyo, wananchi nendeni kwenye tume mkatoe maoni yenu na naiomba sana serikali katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba sana Serikali dira yao ya Zanzibar tunayoitaka iwe ni maoni ya Wazanzibari isije serikali ikathubutu hata siku moja kupinga maoni ya Wazanzibari sisi tuko pamoja nao Wazanzibari wote ahsanteni sana.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii ya kumpongeza na kumshukuru sana Waziri wetu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya pili baada ya kuondoka mwanamapinduzi hapa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nichangie machache na nianzie suala la Muungano na hali ya kisiasa tuliyonayo hivi sasa.

Mhe, Mwenyekiti, mwakilishi aliyemaliza wa Jimbo la Wawi ametamka wazi kwamba yeye hautaki Muungano. Lakini mimi niseme kwamba, mimi nautaka Muungano, nautaka kwa sababu najua faida yake, umetulea, umetuenzi

na kuwaenzi viongozi wetu ambao walianzisha Muungano huu ni kuudumisha Muungano huu. Kwa kweli kama viongozi wa wananchi wetu tukifanya masikhara na kuvunjika Muungano huu ukiwa ndani ya mikono kama sisi ni viongozi hatutawatendea haki watoto na wajukuu wetu wataokuja hapo baadae wakija wakisikia historia ya kwamba Muungano ulivunjika na ulivunjika kupitia maoni ya Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo ningewaomba sana waheshimiwa wenzangu tuungane kwa pamoja tuijenge amani, tuujenge Muungano wetu kwa kuthamini yale ambayo viongozi wetu walikaa na kutafakari na kuona kwamba umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya kisiasa tuliyonayo hivi sasa kwa kweli tuko katika hali ya utulivu na amani, Rais wetu Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume kwa kushirikiana na wenzake leo ametuweka katika hali ya umoja huu tulionao, Barazani hapa tupo tunakaa pamoja, tunazungumza pamoja, tunatembea kwa pamoja, lakini ikija hali ambayo itachafua hayo hayatakuwepo na yataondoka. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningewaomba sana viongozi wetu wakuu pamoja na sisi wawakilishi, mawaziri na wabunge tuweze kupeleka ujumbe kwa wanachi wetu majimboni ili kuweza kudumisha Muungano huu.

Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa hii ya Mhe. Waziri ametamka hapa kuhusu hali ilivyo vile ambavyo wenzetu hawa tunaowaita UAMSHO walivyoharibu hali ya amani katika siku mbili tatu na ametaja maeneo ambayo yameathirika. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimesikitika sana kuona kwamba hata katika maeneo mengine ambayo yameathirika hayakutajwa humu zikiwemo maskani zetu za chama ambazo pia zilichomwa moto lakini hazikutajwa. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi atupe maelezo kwa nini maskani zetu za chama zimechomwa moto kutokana na maandamano yale ambayo yalifanywa na Jumuiya ya UAMSHO.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 40 Idara ya Sheria na Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa. Katika kipengele kile ambacho kinasema kuendelea na matayarisho ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ambayo tutayafanya baada ya miaka miwili ijayo, mwaka 2014. Mhe. Mwenyekiti, nimependa kuzungumzia hili nikiwa kama mdau wa michezo, katika sherehe zetu za miaka minne mitano iliyopita sherehe zetu zilikuwa zinashajihika sana kwa kupitia mashindano ya *Mapinduzi Cup*. Mhe. Mwenyekiti, kamati ile ya *Mapinduzi Cup* ambayo ilikuwa inafanya mashindano katika kusherehekea Mapinduzi matukufu tunaelekea katika miaka 50 ya Mapinduzi matukufu hivyo ningeiomba sana ofisi ya Mhe. Waziri kuwa karibu na kamati ile ili kuweza kuboresha zaidi mashindano yale ya miaka 50 inayo kuja ili kuweza kuhamasisha zaidi sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu wakati itapofikia miaka 50.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, michezo inajenga umoja na mshikamano na michezo ndio inayoleta umoja hata katika huu Muungano wetu. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri ajipange vizuri na kukutana na ile kamati ili kuweza kuipangia mambo haya ya sherehe zetu za miaka 50.
Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesema kwamba sina mchango mkubwa lakini tu namuomba Mhe. Waziri yale ambayo nimeyazungumza ya kudumisha umoja na mshikamano na usalama wetu Wazanzibari namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hali tunayokwendanayo kama haitasimamiwa vizuri tutafika pabaya. Nakuomba sana Mhe. Makamu wa Pili ulichukulie hilo ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata nafasi hii kuchangia machache na mimi kutokana na wakati mdogo uliotoa. Kwa hivyo mimi nianze na hali ya kisiasa iliyopo hivi sasa ambayo Mhe. Waziri aliitaja. Kwa kweli tuko katika utulivu mzuri wa kisiasa na tunakwenda vizuri na ningeomba Wazanzibari utulivu huu wa kisiasa uliopo tuudumishe ili Zanzibar iweze kusonga mbele, pasipo na utulivu basi hakuna uchumi wala maendeleo. Kwa hivyo, ningewaomba Wazanzibari wenzangu hali hii ya kisiasa iliyopo tuidumishe.

Nije katika eneo linalozungumzia uwezeshaji wananchi kiuchumi na kwenye Mfuko wa JK na AK, ambapo hapa zimetajwa shilingi bilioni moja, milioni mia tano na ishirini na tisa, mia nane na thamanini na nne zimetumika kuwawezesha wananchi. Lakini ukizitizama mimi sioni kuwa pesa hizi zimewanufaisha hao waliopewa, kwa hivyo ningetaka kujua pesa hizi zimesaidia vipi na imeleta maendeleo gani kwa hao waliopata fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika migogoro ya ardhi, ardhi ina migogoro mikubwa na ni sugu, nashukuru kuwa imetajwa kuwa baadhi ya wanaosababisha ni viongozi. Mimi ningeomba nchi hii tunakwenda kwa utawala bora kwa hivyo tusirudi katika zama za maisha ya jangwani kuwa mwenye nguvu tu ndiye mwenye haki. Huu si wakati tena wa kuwa mwenye nguvu ndiye mwenye haki, lakini kila mmoja lazima apate haki yake kulingana na haki yenyewe

ilivyo. Zanzibar lazima tugawane haki sawa kwa wote kila anayehusika apate haki yake. Kwa hivyo, tuache wakubwa kung'ang'ania sehemu ambazo hazituhusu na tuzirudishe kwa wenyewe.
Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipoingia nashukuru alianza kwa *speed* nzuri kuhusu yale maeneo ya wazi kuwa yasijengwe na alisimamia vizuri, lakini baadae nguvu zile zilirudi chini, sijui sababu zipi za msingi zilizosababisha kusimamia maamuzi yale ya kimsingi mpaka yakaachwa leo ikawa maeneo yale watu wanaendelea kufanya watakavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la maafa. Maafa ni jambo ambalo linatokea bila ya kutarajia, mara kadhaa hutokea maafa mbali mbali kama vile ya baharini, ardhini na mengineyo. Katika jimbo langu kulitokea maafa fulani ya sehemu fulani kuingia moto na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais alikuja ile hali alipoiona akairipoti serikalini kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na yeye Mhe. Makamu wa Pili hakuajizi alifanya ziara ya kuja kuiona ile hali ilivyo katika sehemu husika. Lakini kwa kuwa mimi kamati yangu inahusika na mambo ya maafa niliona kuwa Mhe. Makamu wa Pili ataambatana ama na Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ni Mwenyekiti wa kamati yangu inayohusika na mambo hayo au Mhe. Mgeni Hassan Juma au Mhe. Usi Jecha Simai na wengineo, lakini badala yake alikuja na watu ambao si wa kamati ya maafa.

Sasa wale watu wa kamati yangu hawakuona lile jambo ambalo limetokea kule. Kwa hivyo ningeomba mambo kama haya kamati husika ishirikishwe kwenda katika kitu kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nigusie kidogo hili suala la Muungano na kero zake. Hapa tunazungumza kero za Muungano lakini hizi kero za Muungano zinatoka wapi, ilikuwaje ikawa kuna kero hizi? Kabla ya Muungano kulikuwa na kero zozote baina ya Tanganyika na Zanzibar, baina ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa Tanganyika? Nadhani kulikuwa hakuna kero na ushirikiano baina ya nchi mbili hizi ulikuwepo na pia ushirikiano baina ya Afrika Mashariki ulikuwepo. Ninavyojua mimi Afrika Mashariki ilikuwa ina nchi nne ikiwa ni Tanganyika, Kenya, Uganda na Zanzibar na wala si Uganda na Rwanda kama ilivyo leo kuingizwa na ikatolewa Zanzibar. Muungano huu wa Afrika Mashariki hii una lengo la kuifanya Zanzibar itoke katika ramani ya dunia. Wazanzibari tusilikubali hilo kwa sababu Zanzibar ni nchi na ipo sasa basi, mimi nadhani kero kubwa ni Muungano ***in such***, kwa hivyo unahitaji marekebisho ya hali ya juu, unahitaji mabadiliko makubwa kweli kweli ili usiwe kero baina ya Watanganyika na Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kunapotokea mambo ya aina hii kuundwa tume uzoefu wangu unanionesha kwamba Zanzibar tume hiyo huivamia mwanzo kuliko kule Tanganyika, leo tume hii tayari iko Zanzibar na pengine itaanza Kusini Pemba sijui na wapi kwa nini wasianze Tanganyika watuanzie Zanzibar mapema, hawatuachi tukajipanga. Wao kule wanajitayarisha wanaanza kwetu hatujajipanga kwa nini? Kwa nini wasianze Tanganyika ambako ni kukubwa zaidi ikichukuliwa Zanzibar ikatiwa kule Dar es Salaam yote inazama wala haionekani lakini hawaanzi kule wanakuja kuanza kwetu. *Why*?

Mhe Mwenyekiti, Mhe. Jussa alisema serikali lazima iwe na mambo manne. Sisi tunayo matatu tumekosa moja. Hatujulikani duniani. Tulikuwa na kiti Umoja wa Mataifa, leo hatuna tena kwa sababu hatuna foreign affairs, kwa hivyo hatutambulikani kama ni nchi.

Ili Zanzibar irudi kuwa ni Zanzibar, ni lazima kwa uono wangu mimi tuanzishe umoja ambao Zanzibar itakuwa ni nchi kamili inayomiliki kila kitu chake, na Tanganyika imiliki kila kitu chake, tena ikiwa tunataka kufanya ushirikiano fulani hapo ndio tufanye. Ninakusudia Zanzibar iwe na maamuzi yake yaliyokamilika kwa kila kitu na Tanganyika iwe hivyo kwa kila kitu. Halafu tutafute jambo la kushirikiana, si la kuungana kama ilivyokuwa umoja wa Afrika ya Mashariki, Umoja wa Ulaya.

Muungano wa aina hii mingi Mhe. Mwenyekiti, imepotea. USSR ulikuwa ni muungano mkubwa sana, leo haupo. Hapa Afrika; Senegal na Gambia walifanya muungano, leo haupo. Kwa kweli muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni wa muda mrefu na wa kiajabu ajabu.

Sasa ili kuondoa ajabu hii ya kidunia, lazima Watanganyika wawe na serikali yao kwa kila kitu, na Zanzibar iwe hivyo hivyo. Wale ambao wana mawazo kwamba muungano uliopo ni kuelekea serikali moja, moja haitufai kwa sababu itakuwa Zanzibar haipo na Baraza hili litakuwa halipo ambapo ninaamini Wazanzibari hatuko tayari ku-*surrender* Zanzibar ikawa haipo. Hii ni imani ipo hivyo.

Na kuhusu suala la serikali tatu, bado hii ya tatu ikija kuhodhi haya mambo ya nje na mengineo bado Zanzibar itakuwa haijapata haki yake kama ni nchi. Ili Zanzibar iwe kama ni nchi tuwe na muungano wa serikali mbili. Tanganyika iwe na serikali yao na Zanzibar iwe na serikali yao na watafute mambo tushirikiane.

Mhe. Mwenyekiti, vyovyote itakuwa Zanzibar hatujaifanyia haki, itakuwa mapinduzi hatujayafanyia haki, itakuwa Wazanzibari hatujawafanyia haki. Ili Zanzibar isiondoke katika ramani ya dunia ambayo leo inaning'inia kuondoka, ni juu yetu kuhakikisha kuwa Zanzibar inadumu kama Zanzibar mpaka mwisho wa dunia.

Tusiwafanye watoto na wajuu wetu wakafunga vimbuga kuitafuta Zanzibar yao, sisi tutakuwa *mas-ul*, tulikuwa wapi? Wakati ni huu Tume iliyokuja Mwenyekiti kazungumza jambo kwamba watu wazungumze vyote watakavyo, vile ni kututia changa la macho.

Kujadili jambo ambalo limo nje ya utaratibu, yeye atasikiliza lakini jee atalichukua. Kusikiliza ni jambo jengine na kuchukua ni jambo jengine. Nawaomba Wazanzibari wenzangu tuelimishane twende katika Tume, na tudai Zanzibar iwe na serikali yake tegemezi kwa kujitegemea kila kitu, na wenzetu iwe hivyo hivyo ili tuondokane na hizi kero za kila siku.

Kero hizi kwa mfumo huu hazishi, haziondoki. Kero iliyoondoka ni moja tu waliyotaka Tanganyika kuondosha pasipoti, kwa sababu wametaka wao imeondolewa. Nyengine zote zipo, hata kama wameziondoa zimeondoka katika karatasi lakini kiutendaji zipo pale pale. Kwa hivyo tuhakikisheni kwamba hizi kero zimeondoka kweli.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze Serikali na Wizara hii kwa kufanyia matengenezo makubwa kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Pindipo kiwanda hiki kikikamilika mashapisho ya serikali yatakuwa pahala pazuri, salama na siri za serikali zitakuwa salama. Kwa hivyo ningeomba Ofisi hii iiboreshe kiwanda hiki ili kiweze kufanya kazi zake za serikali katika pahala pazuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Dakika 5 za ziada.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Dakika 5 za ziada.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Jengine nimalizie kwa muda huu ulionipa kwa Baraza lina kamati zake, na kila kamati zinafanya kazi zake. Lakini muda wa kazi kwa kila kipindi cha kamati ni siku kumi.

Mhe. Mwenyekiti, muda huu ni mdogo sana kwa kufanya kazi katika sehemu ambazo kamati zimepangiwa. Ningeiomba serikali itazame uwezekano wa kuziongezea kamati muda wa kufanya kazi, ili kazi inapofanywa ikamilike katika kipindi ambacho kimepangwa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza au sisi tupo katika Utumishi wa Baraza, lakini watumishi wa Baraza wamo katika utumishi wa umma. Ikiwezekana ningeomba mimi tufanye marekebisho ili waheshimiwa pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi hii ya Baraza wawe katika Tume moja ya utumishi, yaani Tume ya Baraza kwa sababu wao ni watu wa hapa, ni wafanyakazi wa hapa. Kwa hivyo mambo yao yote yamalizike katika Baraza kama yanavyomalizika yetu sisi wengine.

Baada ya hayo machache kwa kuwa umenitaka nimalizie, na kwa kuwa Kanuni tumekiuka hapa kidogo kwa maombi yako nimalizie hapo, niseme ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makofi).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupe shukurani zangu za dhati baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukiwa wazima wenye afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, niliposimama niliangalia nyuma juu pale, nilikuwa ninaangalia kama wageni wetu kama wangalipo Waheshimiwa Madiwani. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, wageni wetu Madiwani wameshaondoka.

Lakini pamoja na kuondoka bila shaka walipoleta maombi yao ya kuja yalifika katika Ofisi ya Mhe. Spika. Kwa hivyo nilikuwa naomba ningependelea zaidi ninapozungumza na wao wangekuwepo, ili na wao wakatuelewa sisi Wazanzibari tunasema nini.

Mhe. Mwenyekiti, wageni wale Madiwani moja ya zawadi wakiondoka wape Katiba ya Zanzibar, kwa sababu sisi tupo katika muungano wa nchi mbili. Lakini nikizungumza Muungano wa nchi mbili wao Madiwani hawaelewi kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 1 kabisa kinasema, "Tanzania ni nchi moja tena ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Lakini sasa Katiba ya Zanzibar kifungu hicho hicho cha 1 kinasema, "Zanzibar ni nchi tena miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". Sasa naomba sana kwa sababu sisi, mimi pamoja na wewe tumeapa kuzitumia Katiba mbili hizi na tuliapa kwa kitabu cha Mwenyezi Mungu *Subhana wataallah*.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka nianze na hapo hapo. Mimi nataka nianze na suala zima la mchakato wa Katiba. Mimi kwanza ninataka niilaumu serikali. Kwa nini nikasema hivyo? Mhe. Mwenyekiti, kwenye bajeti iliyopita mimi nilisimama kwenye kiriri hiki hiki, nikaiomba serikali tumejiandaa vipi, tena nilimuelekeza moja kwa moja Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kunakuja suala zima la mchakato wa Katiba, jee tumewaandaa vipi wananchi wetu kwenda kutoa taaluma alau wakaelewa hiyo Katiba inasemaje na wanatakiwa waje wafanye nini.

Mhe. Mwenyekiti, hilo halikufanyika. Sasa leo tujiulize, Tume juzi imeshakuja ingawa mheshimiwa mwenzangu Mhe. Mohamed kazungumza wameanza Zanzibar, hawakuanza Zanzibar peke yao. Wameanza Zanzibar katika mikoa miwili ya Kusini, lakini na baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara. Kwa hivyo kote kote wamekwenda.

Lakini Mhe. Mwenyekiti tujiulize, Leo wananchi wetu wa Zanzibar ni wangapi wanaoijua hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo wananchi hao hao wanatakiwa wakatoe maoni kuiboresha Katiba hii. Mhe. Mwenyekiti, hata sisi inapoletwa miswada hapa tunatakiwa miswada ile tuipate mapema, karibu siku 21 ili tupate kuipitia tuangalie vifungu na halafu baadae tuje tufanye marekebisho.

Miswada ile Mhe. Mwenyekiti, ukiiangalia inaandikwa na wanasheria waliobobea ndio inaletwa hapa, sisi wanasiasa kwa kuwa tunakaa na watu na kusikiliza mawazo ya watu, tunakuja hapa tunaikosoa na Serikali inakubali.

Sasa leo tunakwenda wananchi wetu tunawapa mzigo wa kwenda kutoa maoni juu ya Katiba. Sasa waswahili wanasema vipi, "Asiyefunzwa na babaye na mamaye, hufunzwa na ulimwengu". Matokeo yake serikali imeshindwa kuja kutoa elimu, sasa kuna watu wameamua wao kwa kuwa wanahisi wanajua hiyo elimu, wamekwenda kuitoa wao na wanavyotaka wao, ndio tatizo.

Hapa watu wanalaumu sijui Uamsho, sijui Serikali na Uamsho wanajuana, kwa sababu hata katika vyombo vya habari tushawaona wanasutana. Sasa hilo ninamuachia mwenyewe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nije ndani kidogo,juu ya suala la Katiba. Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa kama Wawakilishi wa wananchi bado hatujafanya ile kazi inayotakiwa. Kwa hivyo tujiulize nani mpaka sasa hivi kakaa jimboni mwake alau akenda akawasomea hii Katiba ya nchi yake. Kila mmoja anaogopa, anaogopa nini kwa sababu inatonesha.

Kwa sababu leo utakapoangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano vifungu vyake vinagongana na vifungu vya Katiba ya Zanzibar, utajipeleka wewe? Hujipeleki utaogopa, maana ukisema hivi, hii utaikosoa, ukiikosoa hii, hii utaisifu.

Ndio hicho kifungu cha mwanzo tu, mlango wa kuingilia tayari umeshagongana. Sasa hapa kuna tatizo, lakini kwa kuwa tunatakiwa tuje tuirekebishe Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi ninadhani sasa hivi tuichambue Katiba ya Jamhuri ya Muungano na tuangalie vipengele gani vinavyotuathiri.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote hapa tunakuja kupiga kelele, lakini makelele yetu ni ya bure. Ukiangalia kifungu cha 64 cha Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetuwekea mipaka. Mambo yote ya Muungano yapo chini ya Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Serikali ya Muungano.

Lakini mambo yote ya Zanzibar yamo kwenye mamlaka ya Baraza la Wawakilishi. Sisi tulipoingia, tuliapa kuziheshimu Katiba hizi mbili. Sasa kama tunaendelea kukubaliana na yaliyomo humu kwamba mamlaka ya Zanzibar yaishie hapa Zanzibar mwisho Chumbe, basi tukatoe maoni tuseme hewalla bwana! Tuendelee na uzi huo huo kama tutakuwa tumeridhika.
Lakini kama hatujaridhika, huu wakati umefika na sio wakati wa kulalamika. Wengine wanasema haukushirikisha wananchi. Ipo Miungano mengine haikushirikisha wananchi. Mfano moja ni Falme za Kiarabu, pale kwanza hapana utawala wa kupigiana kura. Pale pana wafalme, na muungano wao unakwenda vizuri tu. Muungano ni maslahi.

Kule wenzetu ni wafalme wapo pale, muungano upo na kwa kuwa wananchi wanashiba wamenyamaza kimya. Sasa tatizo Mhe. Mwenyekiti, hata ukakuta hizi kero Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tutamuonea bure. Mamlaka yake ni mwisho Zanzibar. Sasa leo unataka akadai nini juu ya Jamhuri ya Muungano?

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tusimuonee bure. Kama wa kuwaambia tuwaambie ni Wabunge wetu watano tuliowachagua hapa kuwapeleka Bungeni. Mhe. Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa nini? Ukiangalia kifungu cha 98 cha Katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimelipa mamlaka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika ile orodha ya kwanza ya mambo ya muungano, jambo lolote wanaweza wakaliongeza, wengine wanasema wameongezwa kinyemela, hayajaongezwa kinyemela, Katiba imeruhusu hata kama sisi hatutaki, wakati Katiba imeruhusu yataongezwa tu.

Leo kifungu hiki cha 98(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kinasema: "Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litaweza kufanya jambo lolote katika haya mambo ya muungano ikiwa litapata ridhaa ya Wabunge thuluthi mbili au tatu kama sikosei ndani ya Katiba hii.

Sasa jee tujiulize jambo gani hawa watakapokwenda kule wakaweza kulizuia lisipite, yatapita tu kwa mbele, nyuma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki hiki cha 98 (1) (b) kinasemaje, "Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyongeza ya pili kuna mambo manane pale". Yale jambo lolote wakitaka wao, ikipigwa kura ya *two third* majority Zanzibar na Tanzania Bara jambo hilo lishakubalika.

Na hata huu muungano tunaosema sisi tunaulinda kwa nguvu zetu zote, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitokea Mbunge mmoja tu akipeleka hoja Bungeni, ikijadiliwa tena ndani ya masaa mawili tu, ikiungwa mkono na *two third* majority ya pande zote mbili, muungano haupo.

Sasa ndio tunaulinda huo muungano. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa mlango wa kuvunja muungano. Lakini ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Katiba ya Zanzibar ambapo vijana wetu wengi hivi sasa walioshawishiwa wakaambiwa kwanza tupige kura ya maoni, Katiba hii haina mamlaka ya kuvunja muungano kwa sababu mambo ya muungano Zanzibar sisi hatuna mamlaka nayo, na mambo ya muungano moja katika orodha ya kwanza ile ni Katiba ya Jamhuri na Serikali ya Muungano. Sasa tutatokea wapi.

Matokezeo yake hivi sasa alau tunashukuru vijana wetu wameshaelewa wamerudishwa katika mstari waende wakatoe maoni.

Sasa tuje katika hayo maoni. Juzi baada ya Jaji Warioba Mwenyekiti wa Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba kusema kwamba ameruhusu wale waliosema hawautaki muungano wache waseme wamefurahi. Ni kinyonyo hicho, hicho kinaitwa kinyonyo. Mhe. Mwenyekiti kinyonyo unakijua, mtoto akilia kama mama yake kenda kazini huna ziwa la kumpa basi unampa kinyonyo, ananyonya ananyamaza ili mzee apate kufanya shughuli zake nyengine.

Mhe. Spika, ukiangalia kwenye kifungu cha 46 (b), hebu twende mpaka kwenye mabano tatu kinasemaje. Kuna viongozi wakuu, wananchi wao kwanza wametakiwa kabla ya kushika madaraka yao, kwanza wale kiapo cha kuulinda umoja na muungano. Sasa hii Tume kaiteua nani. Tena viongozi wenyewe ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamo wa Rais, Rais wa Zanzibar na Waziri Mkuu. Hao wamelazimishwa na Katiba hii kabla ya kushika madaraka yao, kwanza wale kiapo cha kuulinda Muungano.

Sasa tujiulize hii Tume kaiunda nani ambayo Mwenyekiti Warioba kateuliwa na huyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akawa mwenyekiti. Leo utegemee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kaapa kuulinda muungano, akasikilize maoni kwamba kuuvunja muungano?

Ndio maana nikakwambieni hicho ni kinyonyo. Mimi ninadhani Wazanzibari tatizo letu hatujui tunachokitaka. Sisi kazi yetu ni kulalamika tu. Wazanzibari tukienda hivi sasa tumegawika mapande manne.Kuna pande linataka serikali moja japo ni asilimia ndogo, kuna pande la serikali mbili lipo kubwa, kuna pande linataka serikali tatu lipo kubwa, na sasa hivi kuna pande halitaki kabisa huo Muungano.

Ukija kwenye maoni Mhe. Mwenyekiti, tuseme wanaotaka serikali moja ni asilimia 10, wanaotaka serikali mbili asilimia 30, serikali tatu asilimia 30, waliokuwa hawautaki muungano ni asilimia 30. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar itakuwa hakuna majority wanaotaka kitu fulani.

Ukija kwenye *percentage wise* huwezi kupata percentage kwa sababu alau ufike asilimia 51 ndio ijulikane Wazanzibari wengi wanataka hivi, lakini asilimia thalathini thalathini, Wazanzibari hatujui tunakitaka nini. Wenzetu kule Bara watajipanga watasema kile wanachokitaka. Matokeo yake kile wanachokitaka wao ndicho kitakachokuwa. Sasa hizo kelele zetu bure tushapigwa kinyonyo kimya na hatuna kitu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sisi viongozi tuwe wakweli tusiwe tunalalamika, yepi yanayotusumbua. Mhe. Mwenyekiti, mambo yanayotusumbua yamo ndani ya Katiba. Mhe. Mwenyekiti, muungano wetu sisi tumeungana kwa wizara ninadhani hazizidi nne.

Lakini ukija katika *practical*, wizara zote ni za muungano. Ukija *reality* wizara zote ni za muungano na hapo ndipo penye tatizo. Leo sisi kuna kitu Umoja wa Mataifa, tunajua Waziri wetu wa Ulinzi akisafiri nchi yoyote kakalia kitu chetu cha Umoja wa Mataifa, Waziri wa Mambo ya Ndani akisafiri nchi za nje, tunajua kakalia kiti chetu cha Muungano, Waziri wa Mambo ya Nje akisafiri kakalia kiti cha Muungano.

Sasa Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano akisafiri nje ya nchi, kakalia kiti chetu, kwa maana sisi katupakata, kama kakalia yeye sisi katupakata kwa sababu kile kiti yeye hakupaswa kukikalia pale kwa sababu tumeungana kwa wizara nne.

Lakini jee tuje na ndio maana muungano wetu unaitwa *unique*, hauna tafsiri ya moja kwa moja, hapa utatafsiri unavyotaka wewe. Kama tutasema mambo ya nje ni ya muungano, kwa hivyo ina maana wizara zote moja kwa moja tutakuja zitakuwa kama za muungano.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba sana Wazanzibari hebu tujiulize hasa nini tunachokitaka? Vijana wetu hivi sasa wanasema wanataka Zanzibar yao, kwani hivi sasa tupo wapi? Si tupo hapa hapa Zanzibar.

Sasa tuseme mamlaka. Tunataka mamlaka ya Rais wa Zanzibar atambulikane Rais popote anapokwenda awe na mamlaka yake kamili. Ndio maana yake mimi nimeshakaa nao sana. Mimi mwenzenu munaniita kila majina Muamsho, sijui hautaki muungano, niiteni munavyotaka? Lakini ninatafuta taarifa za wananchi.

Hivi sasa serikali za demokrasia ukiangalia kifungu hiki cha 9 cha Katiba ya Zanzibar, Utawala wa nchi unaletwa na wananchi. Sasa kama hamkusikiliza wananchi wenye maoni tofauti wanataka nini ukaweza kufanya *conclusion*, ukapata lile jawabu mheshimiwa wataturamba hawa, huwezi ukawa mwakilishi kama hukuchaguliwa.

Mimi ninajisifu chama changu tawala lakini kama mawazo yake hayakukubalika na wananchi wengi tutatawala? Hatutokuwa chama tawala. Mimi ninadhani hebu tukaeni tuacheni tofauti, wengine wanasema hawautaki muungano, hapa Mhe. Saleh Nassor yupo wapi? Wewe unasema huutaki muungano, hii Katiba ndio uliyokula kiapo pale.

Mimi ninadhani tusiwatawanye wananchi tukae nao pamoja. Mhe. Mwenyekiti, najua unataka uniambie ninyamaze...

Mhe. Mwenyekiti: Dakika tano za ziada.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa nitakuja kumalizia siku ya Waziri wa Utawala Bora ajitayarishe, siku hiyo tutakuja kuichambua kifungu baada ya kifungu cha Katiba ili tujue hiki kinatuumiza, hiki kinatusidia.

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja kwenye suala la dharau. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninashtaki leo kwa Makamo wa Pili wa Rais. Kamati yangu imedharauliwa, tena kamati hii kwa bahati mbaya ni kamati nzito sana. Ni kamati inayosimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa, tena inaongozwa na Mwenyekiti wa wenyeviti, lakini kuna mwenyekiti mkubwa zaidi ni mwenyekiti wa Baraza, sitaki kumsimamisha.

Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya wenyeviti Mhe. Hamza Hassan Juma, na Mwenyekiti wa Baraza Mhe. Mgeni Hassan Juma, majina yetu ni mamoja. Leo kwenye kamati tumeagiza tuleteeni *documents* za kampuni ya Nahil.

Tumepata malalamiko kwamba eneo lake limefutwa. Watu wa ardhi hawakutuletea mpaka leo. Jeuri gani hii? Mhe. Mwenyekiti, mimi wala sikuvutiwa na kuundwa na kamati teule kutokana na kudharauliwa kwa kamati yangu, kwa hivyo kama hawakuleta *document* kuna kitu wanakificha.

Sasa hicho kitu walichokificha mimi ninacho hichi hapa. Eneo na Nahil lilipofutwa Mhe. Mwenyekiti, eneo lile liligaiwa mapande manane haya hapa nimeyaandika. Kuna Muyuni Beach Resort and Spa Ltd, Ocean Sands Limited, Ocean Key Resort and Spa Ltd, Grand Isle Resort and Spa, Coral Mist and Spa, Tides Resort and Spa Ltd na kadhalika.

Leo Mhe. Mwenyekiti, sisi mukituona tunasema hapa Kanuni zinadhibiti hapa huwezi ukasema kitu cha uongo. Unaposema kitu unatakiwa uwe na ushahidi. Ushahidi ninao mpaka tarehe zilizotoka.

Leo tumewaambieni baada ya kufutwa eneo lile limerudi wapi, kama limerudi serikalini tujue kapewa nani? Mhe. Mwenyekiti, hizi kampuni zilizotajwa hapa ni hewa. Nimefuatilia hazipo *registered*. Kwa hivyo hapa watu walitengeneza *deal* sasa hivi wamepachika tayari eneo hili kuna kampuni imepewa ndio kwanza wamepeleka maombi ZIPA. Tumemuuliza sisi Mkurugenzi wa ZIPA kasema eneo hili sisi hatujaliruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Makamo wa Pili umruhusu mheshimiwa aliyetaka watu waende wakafuatilie mambo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe zungumza na kiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia migogoro ya ardhi nina wasiwasi kama Chama chetu cha Mapinduzi sasa hivi kitaendelea kuwa imara kama kilivyokuwa imara.

Mhe. Mwenyekiti, mule mlimokuwa ngome zetu za Chama cha Mapinduzi hivi sasa tayari kuna migogoro ya ardhi. Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti hapo Mfenesini, ni jimbo letu ni migogoro ya ardhi mpaka leo haishi. Bambi Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tulishughulikie.

Sisi hatuna tatizo Bakhressa eneo lile kupewa kufuga ng'ombe lakini mbona mashamba yapo mengi. Kuna shamba pale Makue pale Pemba, anaweza akapeleka ng'ombe akafuga wengi tu. Leo shamba la Bambi, viazi vyote tunavyokula katika mwezi wa Ramadhan vinatoka Bambi. Leo wanaambiwa wananchi wale waondoke apewe Bakheressa aende akafuge ng'ombe, Makurunge kuna shamba letu la ng'ombe apewe akufuge ng'ombe. Maeneo yapo mengi Zanzibar Mhe. Mwenyekiti ya kufuga ng'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia malizia ni kamati teule. Kamati teule ile ripoti iliyopita tuliisaidia zaidi serikali na tulimwambia sisi mheshimiwa tumeangalia homa ya serikali, tukajua matatizo yake haya hapa, tumepeleka dirishani kwa Makamo wa Pili ili atafute dawa.

Mhe. Mwenyekiti, yako mambo mengine madogo madogo. Juzi Mhe. Mwanasheria Mkuu hakutufurahisha, anapenda sana kutupa misemo, hatupendi. Anatuambia tusije tukawa kobe na kasa. Sasa sisi kobe, haya tunaishi mtoni wao kasa, lakini kasa anaishi baharini, kasa tukimuona kaingia kwenye maji ni lazima tutamsema.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana kwa sababu sheria tumezitunga sisi, katiba tumezitunga sisi hivyo tunapozikiuka hizi sheria ni lazima tuseme hapa. Sasa mambo ya kobe na kasa hapa sio pahala pake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi naunga mkono hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais sina matatizo nayo, kwa sababu nina amini kwa kudhalilishwa kwa kamati yake basi ataruhusu twende tukafanye *research* katika maeneo yote yale ambayo yana migogoro na tunaamini dawa tutamletea tena Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, hasa kwa umahiri wa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naamini haya yote, sasa hivi vimeshaandikwa vyeti nafikiri dawa karibu itatoka.

Kwa hayo machache nakushukuru ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe, nawaombeni sana tunapofurahika twende taratibu, hizi meza zina mitambo kwa hivyo ukigonga kwa nguvu inawapa athari waliokuwemo ndani kule kwenye mitambo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba nichangie hotuba hii kama ambavyo nimejiandaa na nakuomba Mhe. Mwenyekiti, unistahamilie kwa sababu Mhe. Jaku amesema nafasi yake yeye niichukuwe mimi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia waziri wake wa nchi, kwa jinsi ambavyo ametoa hotuba yake na mimi kama mimi sina matatizo nayo. Sina matatizo kwa sababu ni lazima nikiri kwamba sina hoja kwenye hotuba za wizara nne.

Nilipitisha hotuba ya Waziri wa Fedha,Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa maana ya mpango wa serikali, nitaunga mkono hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais, nitaunga mkono hotuba ya Makamu wa Kwanza wa Rais na pia nitaunga mkono hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wizara hizi mimi nasema sina tatizo na ninawaomba wawakilishi wenzangu wote waunge mkono hotuba hizi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ni lazima serikali tuioneshe kwamba haturidhiki na hotuba za wizara nyengine, ni lazima warudi nazo tukiamua warudi nazo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu inaonekana serikali haiheshimu mipaka ya Baraza, kwa sababu tumekuwa tukisema sana lakini inaonekana kuna jambo ambalo linawakwaza. Kwa hivyo, ili tuisaidie serikali basi kuanzia bajeti hii tuamuwe kuwarejesha mawaziri wengine ambao bajeti zao zinakuwa hazina maana kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye suala la maafa. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotupa takwimu na walivyosimamia masuala haya ya maafa na michango waliyoitoa. Lakini nimuombe Mhe. Waziri basi atupatie orodha ya wale waliofaidika kila jimbo ili tusimamie ule uhalisia wenyewe, isijekuwa takwimu hizi zimo kwenye karatasi tu ni lazima kila mwakilishi apewe orodha ya jimbo lake, ya kwamba nani kafaidika na nani hajapata msaada ule.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mimi nimefanya utafiti nimeambiwa kwamba kuna fedha zimetolewa kwa ajili ya Bima ya Meli, Bima ya mizigo na abiria zaidi ya dola laki tatu, karibu milioni mia tano. Mhe. Waziri hebu tuambie hizi pia unazijua, na kama unazijua fedha zake zimekwenda wapi, hilo la kwanza.

Jambo la pili Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amezungumza habari ya mazingira na uvamizi wa fukwe. Mimi nimpongeze sana tena kwa dhati kabisa, mmiliki wa Hoteli ya *Ocean View* kaka yangu Makungu, kwa kutii amri ya serikali na amri ya Baraza la Wawakilishi. Wawakilishi walivyolalamika kuhusu hoteli yake chini kule, basi kwa hiyari yake ameamua kuvunja, huu ndio uungwana huu ndio ustaarabu na huyu ndie mwekezaji mwenye heshima kwa nchi hii.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana na kwa kweli ni lazima wengine waige mwendo huu, watuwekee heshima ndani ya serikali yetu na watuwekee heshima ndani ya Baraza letu. Wale wote ambao hawafuati maagizo yetu, sasa maana yake wavunjiwe kwa nguvu, hawa sio wawekezaji ni wahuni.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningelizungumza ni suala zima la sensa ya watu na makaazi, Mhe. Waziri ametuomba tuhamasishe, lakini ningeomba nikumbushe kwamba wajumbe hawa hawa waliwahi kuambiwa kwamba watakuwa ni wajumbe wa kamati za sensa za wilaya. Hadi hii leo mimi sijaambiwa kitu, naamini na wenzangu hawajaambiwa kitu. Sasa isijekuwa mulitupaka mafuta kwa nyuma ya mgongo, kumbe muna mambo yenu mnataka kuyafanya. Kwa hivyo, kama ni wajumbe wa kamati za wilaya, basi angalau tuitwe, wala tusipewe posho tuitwe tu

tuambiwe nyinyi mmepewa jukumu la kuhamasisha, lakini inaonekana mnasema mengi Mhe. Mwenyekiti, lakini hatushirikishwi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile suala la *TASAF*, wawakilishi wengi hawana taarifa ya miradi ya TASAF katika majimbo yetu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe sana, kama kweli nia ni kuwasaidia kazi basi angalau tuiteni mutuambie nini malengo na nini changamoto tuwasaidie katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo naunga mkono ni kweli kwamba miradi yote ya *TASAF* Mhe. Waziri, nikuombe tuwe karibu sana na kamati za maendeleo za jimbo, hasa kwa vile umeanzishwa mfuko wa maendeleo wa jimbo, miradi hii ni lazima viongozi wa jimbo, masheha, madiwani na wawakilishi washirikishwe kikamilifu ili kupatikana ufanisi wa miradi hii.
Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningelizungumza ni suala zima la nidhamu ya watendaji. Mhe. Mwenyekiti, serikali inaongozwa kwa sheria na sheria inapovunjwa matokeo yake huwa ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, hivi punde Mhe. Hamza Hassan alizungumza jinsi watendaji wetu wanavyokiuka taratibu na sheria, wengine hawajui kabisa kwamba Baraza la Wawakilishi ni muhimili mmoja wa dola. Mimi nasema kwamba ni muhimili mkubwa sana kuliko ile mihimili mingine ile miwili. Kwa sababu jeuri yote ya watendaji ni lazima ipitie Baraza la Wawakilishi baada ya kuidhinishiwa pesa.

Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza hapa jinsi watendaji wanavyokiuka maagizo ya Baraza. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi mmoja. Sheria nambari 4 ya mwaka 2007 inayohusu kinga, fursa na uwezo wa wajumbe unakataza kabisa pale ambapo Baraza limepita kuhoji mashahidi, halafu baadhi ya mashahidi hao wakabughdhiwa ni kosa la jinai. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekuja na barua, kamati zetu teule zilipopita kabla hata ya kutoa ripoti tayari watendaji wa serikali waliotoa ushahidi wamefukuzwa, huu sio utawala bora. Maana yake yule aliyetoa ushahidi kwa nia safi basi anafukuzwa na aliyeiba mali ya umma analindwa, ni hatari kubwa. Sasa Mhe. Waziri kama kweli wewe ni msimamizi wa kulinda maslahi ya Wazanzibari, basi huyo aliyefanya uhuni huo naomba afukuzwe kazi yeye.

Mhe. Mwenyekiti, tumewaita watu kuja kutoa ushahidi na huo ni wajibu wetu, leo mtu anasema ukweli kwa uchumi wa nchi hii, yeye ndiye anafukuzwa na kesho mtu aje na hotuba yake au bajeti yake tumpe fedha, maana yake afanye jeuri tena afukuze wengine. Mimi sitokuwa mjinga wa kutoa fedha kwa kila ambaye kuwa hataki kutoa fedha kihalali. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tusiwe wajinga. Tuwape fedha wale ambao wanataka kupewa fedha. Fedha apewe Makamu wa Pili wa Rais, Fedha apewe Makamu wa Kwanza wa Rais na fedha apewe Rais na fedha apewe waziri wa fedha.

Hawa ndio ambao angalau wana mwelekeo wa kuwalinda Wazanzibari. Wengine hao wababaishaji ambao wanataka fedha na baadae watukaanga wasipewe fedha. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi nakupa barua hizi kwa nia safi, nakuomba umchukulie hatua yule ambaye amembughudhi mfanyakazi shahidi wa kamati na amefukuzwa kazi, wakati yeye tayari amepoteza mamilioni ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, hizi barua naomba uchukuwe na tafadhali unisaidie jibu, ni hatua gani ambayo serikali imechukua. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, kwamba watendaji wanatoa ushahidi mbele ya kamati kisha mnawabughudhi na kuwafukuza kazi, wakati wewe uliyefanya makosa ndio wa kufukuzwa kazi.
Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye mimi namjua, uwezo wake mkubwa na atusaidi na kama kuna vikwazo basi atuambie tumsaidie. Sisi hata kama utatuambia kwamba katiba ibadilishwe mubakie miaka yote 20 muwe Marais, lakini watu hawa waondoshwe madarakani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningelizungumza ni suala zima la migogoro ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiri kama ni kosa nitakiri kama ni kosa. Mimi ni miongoni mwa wawakilishi ambao waliotembea majimbo yote Unguja na Pemba kufanya tathmini ya wakubwa waliochukua ardhi Unguja na Pemba na mimi nilikuwa na Mhe. Hamza Hassan Juma niseme wazi wazi. Tumetembea Unguja na Pemba na tumegundua jinsi wakubwa wanavyowanyonya wanyonge. Ninao orodha hapa ni zaidi ya maeneo 40 yamefutwa kwa kisingizio cha kukiuka sheria ya ardhi, kumbe mtu amefuta kwa ajili ya maslahi yake binafsi. Spa, spa, spa, ni mtu mmoja tu. Mhe. Mwenyekiti, mtu mmoja ame-*create* makampuni kwa majina tofauti lakini mwisho kuna neno spa limemalizia, ni mtu mmoja tu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kuna siku nasema msipochukua hatua mimi nitakuwa muhanga wa kuwataja wote hapa Barazani. Leo nina orodha, siwataji, lakini musipochukua hatua ya kuwafukuza kazi watu hawa basi nitawataja mmoja baada ya mmoja mbele ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani sisi kama wawakilishi tuko tayari ardhi ifutwe lakini irejee mikononi mwa serikali. Lakini ardhi inafutwa kisha mtu anachukua yeye na wanawe. Huu ni ukoloni, huu ni unyonyaji na huu ni ubepari hatukubaliani nao.

Mhe. Mwenyekiti, Zimbabwe wananchi wamekuwa na migogoro ya ardhi kwa sababu ya hii, maana yake imekuwa hakuna tofauti ya mkoloni na mtawala, mtu anafuta ardhi kwa kisingizio sheria imevunjwa. Sawa kama sheria imevunjwa basi mpelekee waziri, nenda serikalini, hatimaye mtu anasajili makampuni kwa jina la mwanawe.

Mhe. Mwenyekiti, leo wenzangu wananiambia nisiwataje, lakini Mhe. Waziri tafadhali sana. Kwani kuna tatizo gani. Nimekwenda mimi na Mhe. Hamza Hassan Juma, Nungwi, kuna ardhi imegemwa mapande manne, watu wanne wamegawana, dalali ametuambia nimeambiwa niuze dola laki nane kila upande mmoja. Dola laki nane si chini ya bilioni moja, upande mmoja mtu anatoa bilioni moja na mapande kumi bilioni ngapi. Kumbe ndio maana mkatuambia uchumi umepanda, kumbe umepanda kwa wakubwa. Pande moja Nungwi huko na wote ni wahusika wa ndani ya serikali hii, pande linauzwa dola laki nane mtu mmoja, mapande kumi maana yake dola milioni nane, ni pesa ngapi hizo. Baadae mnakaa kikao wataalamu mnatuambia uchumi umepanda, kumbe mnachukuana watu kumi na mapande kumi mnayahesabu uchumi umepanda.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara ya mwanzo Rais wa Zanzibar amepokelewa Kizimkazi kwa mabango ni aibu. Wananchi wamechoka wanaandika mabango, wananchi wanapenda wampokee Rais kwa mapambo, mauwa na vigelegele. Leo ndio mnawaambia wananchi waandike mabango ya matusi kumpokea Rais ni aibu. Wameamua hivi kwa sababu watu wanalindwa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi najitoa muhanga, kuna siku nitawataja humu nikiwa hai kwa majina wale wote ambao wamechukua ardhi za umma za wanyonge. Natangaza wazi, yeyote aliyechukua ardhi yangu Mwambe katika Jimbo la Kiwani, mimi nitaanza kujenga mwenyewe nyumba yangu. Kuna watu wanne wamechukua ardhi Mwambe nakwenda kupima pegi najenga mimi mwanzo ndani ya ardhi yake. Najua nitashtakiwa, sasa yeye atasema wapi kaipata ardhi ile. Haiwezekani, watu wanapima ardhi bila sheria wala utaratibu, huku Rais anasema na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anasema, sisi tunashangaa, maana yake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akisema wawakilishi wanamuheshimu sana, lakini mwakilishi anamuheshimu Balozi, mtu wa kawaida yeye anadharau. Sasa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohamed Aboud, mimi nakuamini sana, nakuomba watu washughulikie.

Mhe. Waziri CCM haina upungufu wa wasomi, CCM haina upungufu wa mawaziri mtapata tu, CUF haina upungufu wa mawaziri mtapata tu. Msilinde watu kwa sababu ni waziri, mtowe na mpe mwengine, kwa sababu usipomtoa Mhe. Mwenyekiti, wawakilishi wataamua kuzuia bajeti utatulaumu, *Wallah* utatulaumu. Huna lugha ya kutuletea humu, wakati mtu tunayemshutumu kwa ushahidi bado tumpe fedha, hatumpi fedha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaambia wawakilishi wenzangu, kila mwakilishi ambaye amechaguliwa, waziri ambaye kuna ushahidi wa wizi pesa tusimpe, huyo hafai kuwa waziri. Kwa hivyo, Mhe. Mohamed Aboud sitokuheshimu, ndio maana hotuba yako tukaipitisha, lakini tafadhali tusaidie kwa maana ya kuwasaidia wanyonge, watu wametajirika mno kwa migongo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ujumbe wangu umefika kopi hii Mhe. Waziri ukitaka nitakupa, lakini nitakupa kwa maana ya kwamba ushughulikie, kuna siku nitataja majina hadharani, sote tukaonana wabaya hapa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka nilizungumze ni suala la Muungano ambalo wenzangu wamelizungumza. Kwa kweli wenzangu wamezungumza sana. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Hamza Hassan Juma wamezungumza hapa. Mimi ninachowashawishi wenzangu tu kwamba sioni haja tena ya kuendelea na hivi vikao vya Muungano. Sioni haya kwa sababu ya kupoteza pesa. Hatuwezi kupoteza pesa watu wakenda Dar es Salaama wakala tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile kuna marekebisho ya katiba na Wazanzibari tayari wameamua kurekebisha Muungano. Mimi niwaombe wawakilishi wenzangu, tusimpe waziri fedha yoyote ya kuweza kufanya vikao vya Muungano havina faida na sisi.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana Mhe. Waziri alituambia kuwa wamefanya vikao saba vya changamoto za Muungano kwa ngazi za watendaji, baadae wakafanya vikao vitatu vya makatibu wakuu na vikao viwili vya ngazi ya mawaziri jumla ni vikao 12. Baadae vikaja vikao vya viongozi wakuu, kikao cha Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, bado hapo. Baadae vikao sita vya kisekta vya mashirikiano baina ya SMZ na SMT. Sasa mimi najiuliza vikao 13 hee! Basi hakuna hata hatua moja iliyofikiwa. Bado Mhe. Waziri utuombe fedha tukupe tena mkakae kikao tena. Mimi nadhani hizi fedha tumpe Mhe. Ali Mzee na Mhe. Moyo wapite kila jimbo wahamasishe watu jinsi ya kutetea haki yao ya Muungano. Mimi nawaambia wawakilishi wenzangu tusiwe tayari kumpa Mhe. Mohamed Aboud fedha hii Mhe. Waziri tuwachie ili tuwape wajumbe wa Baraza la Wawakilishi chini ya mzee wetu Mhe. Ali Mzee na Mzee wetu Nassor Moyo, ili watuelimishe nini faida ya Muungano, nini malengo yetu na nini muelekeo wetu kwa ajili ya kupata Zanzibar mpya chini ya Uhuru na Kujitegemea kama Zanzibari.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa hili Mhe. Balozi nakuomba unistahamilie sitokuwa tayari kukupitishia pesa kwa ajili ya kwenda kufanya vikao vya Muungano. Najua hapa ni mtaji wa watu na ni biashara ya watu, kwa sababu ikiwa vikao vya sekreterieti ni vikao saba, mimi sioni faida yake. Kwa hivyo, fedha hii yote ikiwa ni milioni 300 basi iende kwenye elimu kwa wapiga kura wetu au iende kwenye elimu kwa wananchi wetu ili wajuwe nini mwelekeo wa Muungano na nini madai yao Wazanzibari, badala ya kupeleka fedha na watu wakenda kule wakajipepea na mafeni wala hatuna faida tunayoipata.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kabisa tu kwamba katika hili

Mhe. Mwenyekit: Zingatia muda Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba katika hili mimi sina tatizo na wizara hii, ugomvi wangu ni fedha ile ya Muungano ambayo sitokuwa tayari kuwapa kwa sababu haina faida. Lakini nakuhusia Mhe. Waziri hasa kwa vile hii ofisi ni ya mtu mzima sana, tafadhali washughulikie hawa wote waliokuwa wanachukua ardhi ya wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nasema kwamba nitakuwa wa mwanzo kwenda kujenga nyumba kule kwetu Mwambe ndani ya ardhi ya mkubwa, kwa sababu hawakupewa kihalali. Haiwezekani mimi niliyezaliwa Mwambe na wazee wangu sipewi ardhi ile, halafu akaja mtu kwa sababu ni mkubwa akachukua ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, nikuambie kwamba kazi hii tumeifanya ndani ya miezi miwili. Mtu mmoja katika sikukuu ya Mfungo Mosi alikwenda Urowa na familia yake, picha ya huyo mkubwa aliyekwenda zipo. Siku ya skukuu unawaendea watu na kuwaambia kuwa nimekuja hapa kuwapa zawadi akawagaia fedha, kumbe lengo lake ni kuja kuchukua ardhi. Ni lazima ardhi ile airejeshe na madaraka yale anyang'anywe na ushahidi upo tutakusaidia na kuna siku nitawataja kwa majina ndani ya Baraza hili.

Mhe. Mohamed Aboud wewe humo, wewe ni msafi huna tatizo, lakini usafi wako utakuwa msafi zaidi iwapo hawa utawatowa hadharani na kuwapa heshima ambayo kuwa inatakiwa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia asubuhi hii kuwepo hapa na kuendelea na majukumu yetu ambayo tumepewa na wananchi wetu kwa ajili ya kulitetea taifa letu la Zanzibar.

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kutuletea kitabu chake ambacho kina muongozo katika kuendeleza ofisi yake kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia hali ya kisiasa ilivyo hapa nchini mwetu hapa Zanzibar, kama alivyoizungumza Mhe. Waziri katika ukurasa wa 3.

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli hali ya kisiasa, mimi nasema kwamba hivi sasa Zanzibar ni nzuri kiasi kikubwa sana, hali hii haikuja tu bali imekuja baada ya mazungumzo mengi yaliyofanywa na viongozi wa awamu ya sita, akiwemo Mhe. Dk. Aman Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Katibu Mkuu wa CUF, pale walipoleta maridhiano ya kisiasa

kuondoa mtafaruku ambao umedumu kwa muda mrefu hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hili mimi napongeza sana na niwaombe wananchi wa Zanzibar kwa jumla tuulinde utulivu huu tulionao kwa hali yoyote na kwa bei yoyote *Inshaallah.*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niingie katika Ofisi ya Baraza la Wawakilishi katika ukurasa wa 51. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa chombo kikubwa sana katika nchi yetu ya Zanzibar. Baraza hili lipo kwa ajili ya wananchi kusimamia haki za wananchi wetu, kuangalia taratibu na mienendo ya nchi yetu kwa hali yoyote ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo niseme kwamba ndani ya Baraza la Wawakilishi kuna kamati mbali mbali ambazo Mhe. Spika, huziunda kwa ajili ya kusimamia mambo mbali mbali yaliomo katika wizara za serikali yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa kamati hizi hupangiwa siku takriban huwa ni wiki mbili labda katika kipindi cha kati. Mhe. Mwenyekiti, kwa maoni yangu mimi niseme kwamba wiki mbili za kazi ya kamati ni siku kidogo sana, hasa ukizingatia kwamba mawizarani kuna mambo mengi ambayo yanataka kufuatiliwa na wajumbe hawa wa Baraza la Wawakilishi. Zaidi ya hayo, niseme kwamba kuna kamati ya PAC ambayo inakuwa na jukumu la kuzisimamia wizara 16 pamoja na mashirika, kwa wiki mbili zinakuwa ni ndogo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri aongeze muda wa kamati ili kufikisha ufanisi zaidi wa kazi za kamati za Baraza.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kamati hizo, tunashukuru kwamba Baraza limethubutu kuunda kamati teule kwa ajili ya kushughulikia mambo mbali mbali ambayo yanatendwa katika baadhi ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita, Mhe. Spika, aliunda kamati teule kwa ajili ya kuchunguza wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, na ilileta ripoti yake katika Baraza la Wawakilishi lililopita. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hadi leo hayajatokea matokeo yoyote baada ya ripoti ile ya kamati teule.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuchelewa kutoa ripoti kunaweza kukatokezea athari nyingi katika mawizara, kwa sababu baadhi ya watendaji wa wizara wanaweza kujiona kwamba wako huru, wanaweza wakafanya lolote bila ya woga wa aina yoyote. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba athari zinazoweza kutokea kama serikali haikuchukua hatua juu ya mapendekezo ya kamati teule. Kwanza ni kuruhusu ubadhirifu wa mali za umma kutumika ovyo ovyo, kwa sababu ya kuhofu chochote watendaji.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, kulipunguzia nguvu Baraza la Wawakilishi, kwa sababu ile kamati ni ya Baraza la Wawakilishi, bila ya matokeo yoyote basi ni kulifanya Baraza kukosa nguvu. Lakini jambo la tatu kuwafanya baadhi ya watendaji kutokuwa na hofu katika kazi zao na jengine ambalo linaweza kutokea ni kuwajenga watendaji wetu kibri mbele ya wananchi wao ambao wapo katika nchi.

Kwa hivyo, ningeiomba serikali kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuchukua hatua muafaka juu ya ripoti ya kamati teule, huku tukiona kwamba kuna kamati nyengine ambazo hivi sasa zinaendelea na mchakato wa kazi ya kuchunguza mule ambamo wametumwa.

Mhe. Mwenyekiti, wawakilishi wengi wanaposimama wanaomba kuundwe kamati teule, kwa nini kwa sababu ya uharibifu mkubwa uliopo katika mawizara, kupoteza mali za serikali, kutumia pesa ovyo bila ya kufuata taratibu. Hili linafanya nchi yetu tuseme kila wakati hali ya maisha ngumu. Lakini ulaini wa maisha utapatikana kwa uadilifu, kufuatilia na utekelezaji wa matokeo baada ya ufuatiliaji. Kwa hivyo, ningeiomba serikali suala la kutoa maelekezo sahihi, maelezo muafaka kwa kamati teule ambayo tayari imeshatoa ripoti yake isichelewe kufanya hivi, ili kuwafanya wananchi wake kujenga matumaini ili kuwafanya watendaji kuwa makini katika ufuatiliaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichangie katika suala la Maafa ya Baharini. Kihistoria ni kwamba kuna meli tofauti mbali ya *Mv. Spice Islander* ambayo imezama hivi karibuni tu, lakini kuna Meli ya Mv. Kabul imezama Zanzibar, Meli ya Mv. Fatih imezama na hivi juzi Meli ya *Mv. Spice Islander* ambayo imeua mamia ya wananchi wa Zanzibar. Sasa mimi naiomba serikali, ili kulitatua tatizo hili kutoa tamko rasmi la ununuaji wa meli Zanzibar, ili Serikali ya Zanzibar kuwa na meli yake, kwa sababu tupo katika visiwa jamani Unguja na Pemba hatuwezi kwenda kwa miguu, baiskeli wala gani, isipokuwa usafiri wetu ni wa meli na ndege na wananchi wetu wengi wanaingia

katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa kupitia usafiri wa meli. Kwa hivyo, tunaiomba serikali isiwe na kigugumizi juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika visiwa hatuendi tu, isipokuwa lazima tuende kwa usafiri maalum, mbali ya matajiri kununua meli na kuleta hapa Zanzibar. Lakini serikali yenyewe ingekuwa na meli yake kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wake wa Zanzibar na kupunguza haya maafa kwa meli ambazo hazina uangalizi au uhakika wa safari.

Nikiondoka hapo sasa nizungumzie kuhusu suala zima la Muungano, kama sikutaja muungano hata kidogo itakuwa sijatenda haki katika Zanzibar yetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme kwamba kuna Kero za Muungano, isipokuwa nataka niseme kwamba Zanzibar huu Muungano uliopo ni kero, kwa sababu gani nikasema hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo yangu binafsi nasema kwamba Muungano uliopo ni kero kwa sababu kabla ya Muungano huu Zanzibar ilikuwa ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, na hivi sasa jina hili lipo wapi, halipo kwa sababu ya muungano huu. Lakini kabla ya muungano huu pia Zanzibar ilikuwa na kiti Umoja wa Mataifa, kiko wapi na tunakitumia vipi kiti hiki. *(Makofi)*

Jengine mbali ya hayo, Rais wa Zanzibar kukosa hata kuwa Makamo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii ni kero. Kwa hivyo, niseme kwamba Muungano huu unaoendelea hivi sasa nasema kwamba ni kikwazo kwa Zanzibar, na ni miongoni mwa mambo ambayo yanarudisha nyuma maendeleo ya Zanzibar na tutaendelea kulemaa. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ni kwamba Wazanzibari walio wengi hivi sasa tunasubiri hayo Maoni ya Marekebisho ya Katiba. Kwa hivyo, wito wangu kwa Wazanzibari tuwe makini tuwe na kauli moja na tujenge umoja wa Kizanzibari, ili kuirudisha Zanzibar katika himaya yake ya kuwa na uwezo wa kujitegemea kitaifa na kimataifa, vyenginevyo tutabakia Zanzibar kuwa ni butu tu la ulimwengu, lakini ni kitongoji ambacho hakina mamlaka ya aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo wa Kiswahili unaosema hivi “kawia ufike”. Kwa kweli tumekaa muda mrefu kero za muungano na wala hakujakuwa na mchakato wowote wa maoni ya wananchi kuhusu Marekebisho ya Katiba na tumekaa muda wote huo.

Lakini leo *Alhamdulillah*, timu itapita kwa ajili ya kusikiliza maoni ya wananchi, hivyo wananchi tuwe makini, madhubuti na tuwe na uhakika wa tunachotaka Zanzibar. Zanzibar tunachotaka sisi ni serikali yenye mamlaka kamili kuanzia Zanzibar, Tanganyika na duniani kwa jumla. *(Makofi)*

Kwa haya machache Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata muda huu wa kuchangia angalau mawili matatu katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukurani za dhati kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa namna alivyowasilisha hotuba yake vilivyo. Vile vile na wale wote waliochangia hotuba hii kwa umakini na umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya wakati na kwa vile wengi wameshazungumza, mimi kwa upande wangu naomba nianze kwa kuchangia kuhusu Vitambulisho vya Kupigia Kura. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu chetu cha bajeti hii ukurasa wa 18 kifungu cha 39 kimeeleza kuwa katika mambo mengi ambayo yatakayofanywa kwa mwaka huu, ni kuweka kipaumbele katika kuimarisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura pamoja na mambo mengine zaidi ya hayo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kupiga kura ni haki ya kila Mzanzibari baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa. Kwa kweli sote tumeshuhudia kuwa katika Daftari liliopo kuna baadhi ya watu kama wanavyozungumza Waheshimiwa, wameingizwa mule ikiwa hawana haki ya kuwa wapiga kura au kupewa kitambulisho na kupiga kura.

Vile vile hivi sasa na hata juzi nilivyozungumza hapa na nilizungumza kwa urefu juu ya wale watu ambao tayari wameshafika umri wa miaka 18 na vielelezo vyote wanavyo. Lakini wanapokwenda kwa Sheha kupewa fomu, ili waende wanakohusika kwa kupewa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, ili waweze kupata Kitambulisho cha Kupiga Kura, Sheha anasema fomu zile zimemalizika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, naomba kunukuu

Katiba ya Zanzibar inaeleza hivi:-

> "Kila Mzanzibari anayo haki ya kupiga kura na hatapiga kura tu ikiwa kuna mambo kwa bahati mbaya hatoyatimiza;
>
> (i) Akiwa si Mzanzibari;
> (ii) Pengine labda ana makosa ya Jinai amefungwa katika jela;
> (iii) Ameshindwa kutoa kielelezo kuhusu umri wake, uraia wake au Kitambulisho kama Mpiga Kura".

Mhe. Mwenyekiti, hivyo ndio Katiba inavyoelekeza. Kwa hivyo, ninashangaa kuona kuwa katika nchi hii kuna Wazanzibari ambao wengine ni wazee wetu wamepiga kura katika siku zote zilizopita, na Vitambulisho vya Kupiga Kura wanavyo, lakini safari hii wakakoseshwa kwa sababu hawakuwa na vyeti vya kuzaliwa *register*, Wakati Katiba inaeleza kama mtu anacho Kitambulisho cha Kupiga Kura basi huyo ni mpiga kura. *(Makofi)*

Kwa hawa ambao tayari wameshatimiza umri, na Sheha mpaka leo wanafanya ukaidi, maana yake ni kuwa na mimi binafsi narudia kauli ile kwamba kuna ajenga ya siri kuonesha kuwa Wazanzibari tunawakosesha haki zao, hasa kwa kufuata maneno ya Waheshimiwa Wajumbe wengine wanaosema kuwa wapo ambao si Wazanzibari wanapewa haki hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kufanya marekebisho ya Daftari la Kupigia Kura, basi tuone marekebisho haya yamefanywa kwa kweli. Kwa hivyo, pale ambapo penye kizuizi basi kiondoke na watu wapate kupiga kura na wale ambao walikoseshwa kwa makusudi na mpaka leo ni wapiga kura tena ni Wazanzibari, warejeshewe haki yao na wale ambao hawamo basi si haki yao kubakia katika Daftari na watolewe.

Lakini kwenye Katiba imeeleza kuwa kama mtu atashindwa kuonesha Kitambulisho cha Uraia na hii Mwenyezi Mungu ametujaalia kuwa kuna jambo, kumbe sisi tulikuwa tunalifanya kinyume na Katiba, kwa sababu Katiba imetaja uraia, lakini hakuna hata Mzanzibari mmoja mwenye Kitambulisho cha Uraia.

Kutokana na hali hiyo, natumia fursa hii kwa sababu Katiba ndio yenye nguvu kuliko kitu chochote chengine, na hasa kwa sababu kuna Vitambulisho vya Utaifa vinakuja vya Tanzania na Wazanzibari kwa vile wana msimamo katika mchakato huu wa Katiba wa kudai haki, maslahi pamoja na utawala wa nchi yao.

Kwa hivyo, wapewe moja kwa moja Vitambulisho vya Uraia vya Zanzibar, na hivi vya Ukaazi mimi nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti havina maana kwa sababu hata hivyo vya Bara vitakavyotolewa vitakuwapo vya Taifa, pia vitakuwepo vya ukaazi kwa wafanyabiashara na kadhalika. Kwa nini sisi na nchi yetu bado tubakie na Vitambulisho vya Ukaazi.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo nataka nilizungumze tena kwa ufupi tu, kutokana na wakati ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaamini Marais wetu wa mwanzo Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Rais wa Tanganyika na Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume aliyekuwa Rais wa Zanzibar kuungana kwao, na hasa Sheikh Karume waliungana kwa kuhakikisha kuwa muungano huu utakuwa wenye maslahi kwa Wazanzibari wote, utakuwa wenye maslahi kwa Watanzania wote.

Lakini kwa bahati mbaya hivi sasa kwa tulipofikia muungano umekuwa na matatizo, na wala hauwezi kustahamilika. Serikali yenyewe inajua kwamba ina kero za muungano nyingi sana ambazo tumepiga makelele waende wakazungumzie, ili zimalizike.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya na kwa muundo ulivyo kwa vile yule Mwenyekiti wa Tume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba ni Rais mwenza, nguvu na uwezo wa kutatua na kutokana na Katiba ya Muungano ilivyo kuwa wanaamua kuwa Zanzibar si nchi, hasa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda alisisitiza mara nyingi wakati tulipokuwa tukipiga kelele, maisha hakutatokea suluhu.

Kwa kweli matatizo yamekuwa makubwa mpaka serikali yenyewe Mhe. Mwenyekiti ikafanya marekebisho ya Katiba baada ya Kura ya Maoni, hivi sasa mna vifungu vingi katika Katiba ya Zanzibar ambavyo vinapingana na Katiba ya Muungano. Vile vile kifungu cha 4 cha Katiba ya Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 4 kinaeleza hivi:-

> "Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchi kote na isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ikiwa sheria yoyote inatofautiana na Katiba hii, basi Katiba hii ndiyo itakayokuwa na nguvu, na sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kimehitilafiana".

Kifungu hiki cha 4 ni moja katika vifungu vilivyowekwa katika kifungu cha 80 cha Katiba ya Zanzibar kuwa haviwezi kubadilika mpaka kupigwe Kura ya Maoni tena.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa Katiba ya Muungano inasema Tanzania ni nchi moja na Jamhuri ya Muungano, na ya Zanzibar inasema Zanzibar ni nchi na hiyo ni hitilafu. Sasa ikiwa Katiba ya Muungano inasema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenye mamlaka nje ya maeneo ya Tanzania, lakini isipokuwa Zanzibar atashauriana na Rais wa Zanzibar na Katiba ya Zanzibar inasema ndiye peke yake aliyekuwa na mamlaka hayo.

Kutokana na hali hiyo, inaonekana kuna kero mpaka kwenye hizi Katiba zetu wenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti panapokuwa na kero tutafute njia ya kuondoa kero zaidi kuliko ile ya mazungumzo wakati tayari imeshafeli.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuondoa kero tena kwa nia safi kabisa, basi ni kutafuta njia ambayo haina utata na yenye kueleweka, yaani ni njia ya kuimarisha muungano huu kwa kila nchi kuwa na mamlaka yake kamili basi na tukifika hapo hizi kero *automatic* zitamaliza, na halafu tena tutatafuta njia namna gani twende kwa maslahi ya nchi zetu na muungano wetu huo wa baadae.

Lakini katika hali hii mimi nakubaliana na wananchi wakati tunapojibiwa maswali hapa wakaambiwa kwamba suala tunalishughulikia na mambo haya yatamaliza, na kadhalika na kusema watu wakubwa na kwenda kule na kutumia fedha tu na wala hakuna lolote linaloweza kufanywa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kejeli kwa sababu Zanzibar ni nchi na kama nchi ikesha kuamua jambo basi lazima liheshimike, lakini kuna Kampuni ndogo hapa ya kuchimba Mafuta, ambayo si ya muungano isipokuwa ni ya Tanganyika tu inaitwa *TPDC.*

Kwa kweli *kijikampuni* hiki kazi yote tuliyozungumza Mhe. Mwenyekiti na kupitisha kuwa mafuta si mali ya muungano, basi wameweza kutoa kibali kuwa mafuta yachimbwe, na nyinyi mnatwambia mumeshapeleka barua kwamba yaondolewe, lakini *TPDC* wanasema nendeni mukachimbe mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba ninukuu kidogo tu kwa faida ya wananchi, ili kuweza kujua ni kitu gani kinaendelea katika muungano huu. Mhe. Mwenyekiti, waraka huu unasema hivi "Ruhusa ya Kuchimba Mafuta yatolewa Kampuni moja ya Canada, *Antrim Energy*, inasemekana imepewa na Shirika la Maendeleo la Mafuta la Tanzania, na wala si la Tanganyika tena, *Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC)* haki ya kuanza kutafuta mafuta Zanzibar.

Hatua hii imefungua njia ya kuanza tena kazi ya utafutaji wa mafuta kwa mkataba wa kugawana kinachozalishwa *Production Sharing Agreement (PSA)* Kisiwani Pemba, ambayo ilikwama kwa miaka kadhaa iliyopita.

Stephen Greer, Rais na Kiongozi Mkuu wa Kampuni ya *Antrim Energy*, amesema kufuatia kutiwa saini kwa mkataba huo Kampuni ya *Ras Al Khaimah Gas Tanzania Limited* (*RAK Gas*) na *NOR Energy AS* ya Norway zimeingia mkataba unaoipa *RAK Gas* haki ya kudhibiti huo Mkataba wa *PSA* wa Pemba na Unguja.

Vile vile bwana Greer amesema kuwa kama ni sehemu ya makubaliano hayo Kampuni ya *RAK Gas* itafanya mazungumzo na hiyo Kampuni ya P-Z *PSA* na *TPDC* juu ya makubaliano na mpangilio wa kazi ya utafutaji wa mafuta, ili ipate leseni kutoka kwa mamlaka zinazohusika.

Tumeshashajihishwa sana na kuingia kwa *RAK Gas* katika leseni hii, pande la Pemba Unguja linaonekana kuwa na mafuta mengi, na sehemu hii hivi karibuni imevutia Kampuni kubwa ya *Petrol* aliongeza kusema.

Leseni hii inajumuisha eneo la ekari 3.5 milioni ambalo linasemekana lina mafuta mengi na gesi na kupelekea kuwepo kwa harakati nyingi za kampuni kubwa kutafuta mafuta.

Miongoni mwa kampuni hizi ni *Shell, Exon, Mobil, Statoil, Petrobras, Ophir Energy, British Gas* na *Tullow Oil*.

Antrim Energy inatarajia mikataba hiyo miwili na hasa kwa kushiriki Kampuni ya *RAK Gas*, kutapelekea kuanza tena kazi ya utafutaji wa mafuta katika eneo hilo la Unguja na Pemba katika kipindi cha muda mfupi ujao. *TPDC* inatarajia kuchimba visima vipatavyo 10 baharini.

Eneo la Pemba – Zanzibar limethibitishwa kuwa na dalili za mafuta ambayo yamekuwa yakija juu sehemu ya Tungauwa, na uchunguzi uliofanyika nyuma umeonesha kuwa sehemu hiyo ni yenye mafuta mengi. Karibu asilimia 75 ya leseni ya kufanya shughuli za utafutaji wa mafuta ni ya sehemu zilizokuwemo katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

RAK Gas, LLC, iliyomilikiwa na Falme ya Ras Al Khaimah ya nchi za Ghuba iliyoanzishwa mwaka 1984, na biashara zake kubwa ni gesi na soko la mafuta. Kampuni hii pia inajihusisha na masuala ya utafutaji wa mafuta Afrika ya Mashariki na Misri.

Dalili za mafuta katika eneo la Tungauwa nje kidogo tu ya Mji wa Chake Chake zilionekana mwaka 1985, pale eneo lote la ufukwe wa sehemu hiyo lilipofoka mafuta na hata kuharibu mikoko, minazi na viumbe vya baharini.

Viongozi wakuu wa Zanzibar wakati ule, Rais Mstaafu wa tatu wa Zanzibar, Sheikh Ali Hassan Mwinyi na aliyekuwa Waziri Kiongozi Maalim Seif Sharif Hamad, walitembelea Tundauwa kuona hali ilivyokuwa. Wote wawili waliwaambia wananchi kwamba licha ya kuwepo uharibufu huo hiyo huenda ikawa neema ya mafuta ambayo itanufaisha vizazi vijavyo vya Zanzibar.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti Gazeti linasema kuwa “Eneo jengine la Zanzibar lililowahi kuonesha dalili za mafuta ni Kama, karibu kilomita 20 Kaskazini ya Mji wa Zanzibar. Dalili za kwanza zilionekana katika miaka ya mwisho ya 1950 na tena katika miaka 1971.

Gazeti la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la wakati ule liitwalo “Ukweli Ukidhihiri Uongo Hujitenga” la tarehe 11 Machi, 1971 lilitoa maelekezo marefu juu ya utafutaji wa mafuta katika sehemu hiyo, na picha ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume akizungumza na Meneja wa kampuni ya *AGIP* iliyokuwa ikifanya uchunguzi”.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa wakati ulivyo mfupi naomba nimalizie hapo. Lakini kutokana na gazeti hili Wazanzibari wanasema waambiwe ukweli juu ya uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza natoa wito kwa Wazanzibari wote kwamba waiunge mkono serikali yao imeipitisha kwa makusudi kuwa mafuta na gesi asilia si mali ya muungano. Kwa hivyo, wasikubali kampuni yoyote kuja kuchimba

mafuta katika eneo la Zanzibar. Mimi ikiwa ni mwakilishi wao, basi tutakuwa pamoja kwa ajili ya kupambana na suala hili mpaka kieleweke.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa huu ndio muungano tulionao na halafu tunaambiwa kwamba inakuja Tume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba, tuitumie tume hii italeta muungano mzuri wa masikilizano na kadhalika. Kwa kweli mimi napingana na kauli ya Wizara hii kuhusu Tume hii, isipokuwa naamini kwamba Tume itakuja. Vile vile naomba kuungana na wenzangu kusema kuwa wananchi wajitokeze kwa wingi sana kwenda kwenye Tume na kutoa maoni yao.

Lakini maoni yetu kama Wazanzibari yatasikilizwa, basi yangesikilizwa hapa mwanzo, ndio ninawaomba Wazanzibari waitumie fursa ya tume hii kwa ajili ya kujikomboa katika muungano huu uliokuwa haufahamiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba nisameheke sana na haya ni maoni yangu mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na mashaka sana huko nyuma na halafu yakaja makubaliano tukafanya Kura ya Maoni, ambayo hata Sheha aliwekwa kule na ilikuwa safi kabisa hakuna aliyeguswa, na halafu tena ukafuata Uchaguzi Mkuu nao tukaufanya vizuri safi sana na wala hakuna aliyeguswa, isipokuwa kulikuwa na malalamiko kwa wananchi waliokosesha haki yao ya kupiga kura.

Sasa leo tumeikabidhi serikali mpya ambayo tunaiita Serikali ya Mapinduzi yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Lengo letu ilikuwa ni kuilinda amani ile, lakini tusiwe na mfumo wa kulinda amani kwa vile mtu anavyoona yeye ndivyo japo kuwa sivyo hali halisi ilivyo, hivyo lazima twende na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, tunawaongoza wananchi na wao wanatutarajia sisi kuwa ndio tutakaowaelekeza katika njia. Kwa hivyo, sioni kuwa kwa hali ninavyoiona hivi sasa kwa matokeo yaliyotokea juzi hapo, na matokeo yaliyotokea Mahonda juzi mpaka Msikitini watu kupigwa mabomu na hivi sasa ukipita katika barabara majeshi tele wanafanya mafunzo wakati misitu ya kufanyia mafunzo ipo. Kwa kweli hali hii inafanywa na serikali na tena inahatarisha amani.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna jambo lolote la kuzungumzwa basi lizungumzwe, lakini tukianza kutishana hivi na sasa wananchi wote wameshawajua walipo. Kwa hivyo, nakuhakikishia kwamba tutasema kuwa wananchi wanavuruga amani, kumbe sisi wenyewe wakati ni viongozi hatujajua namna gani tu-*deal* na hawa watu, ili twende pamoja.

Vile vile sisi tumechaguliwa na baada ya kuchaguliwa kukawa na serikali na watu wenye serikali Mhe. Rais Mtukufu akachagua wenzake, lakini tujue kwamba vyanzo ni uchaguzi uliopita. Kwa maana hiyo, lazima tuheshimu matakwa ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili na kwa vile hivi sasa inakuja Tume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba na hali tumeshaiona kwamba kuna wale ambao hawautaki muungano katika hali ilivyo, na hata na mimi ni mmoja wao na wanaomba Kura ya Maoni waulizwe. Vile vile kuna wale wengine wanaozungumza kama tunavyosikia kwa hili, kwa sababu ni la kitaifa, basi naiomba serikali nayo itoe msimamo ambao unakwenda sambamba na matakwa ya wananchi. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013.

Awali ya yote kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuweka hapa tukiwa wazima na afya njema. Vile vile napenda kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake ambayo imetoa matumaini kwa Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa lakini sina mengi sana ya kusema kwamba sababu mengi tayari yameshazungumzwa na wenzangu waliopita. Kwa hivyo, kwa kuwa nimesimama sinabudi angalau nizungumzie masuala ambayo nafikiri yatakuwa ni muhimu kwa mustakbali wa taifa letu.

Kwanza naomba kuzungumzia kuhusu suala la muungano kama Waheshimiwa Wajumbe wengi wametangulia kusema na kueleza hisia zao kuhusu muungano, wamezungumzia maono yao kuhusu muungano na mimi nina haki kuzungumzia hisia zangu, pamoja na muono wangu kuhusu muungano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna wengine wamesimama hapa na kila mmoja amesema lake, kama vile mfumo na wanataka serikali mbili, tatu na hata moja. Lakini mimi ninachokisema kwanza tutizame huu muungano umetokana na nini. Muungano haukuwepo kabla ya Mapinduzi. Muungano ni mtoto wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Tukiukataa muungano ina maana tunamkataa mtoto wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Cha kufanya Wazanzibari nawaomba tuwe makini katika hili. Sikatai mimi nakubali kwamba kuna kero nyingi za muungano. Mimi nakubali hakika zipo kero za Muungano, na tayari kuna hatua ambazo zimeshaanza kuchukuliwa. Tunaishukuru Serikali yetu sana kwa kufanya hivyo. Na kuna mambo ambayo bado wenzetu wanafanya ukaidi kutufanyia mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, tunaponyoosha kwa wenzetu kidole turudishe sisi vinne vinaturudia sisi. Sisi tunafanya nini kuhakikisha kwamba haki zetu tunazipata. Hilo ndio swali. Wengi hapa ni wanasiasa wanajua zaidi kuliko mimi. Lakini hebu tutizameni kitu gani ambacho tutakuja kukifanya ili kuhakikisha kwamba haki za Wazanzibari zinapatikana. Wazanzibari wote tunataka haki zetu. Sikiri kama kuna mtu anaweza akazuka leo akasema mimi Mzanzibari lakini sitaki haki yangu, hakuna kila mtu anataka haki.

Mimi naomba Serikali Kuu namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, tunajua uwezo wako, tunajua wewe ni mtu wa busara, tunajua wewe ni mtu mwenye hekma, na tunajua wewe ni mpole. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuwa wewe umepewa jukumu hili tunakuomba kwenye hili upole uondoshe. Simamia yale ambayo Wazanzibari wanayataka, lakini naomba Muungano usivunjike. Kwa sababu watu wanasema *umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu*. Kinachotakiwa ni kujipanga na sio kuvunja. Uhusiano tuliokuwa nao wa miaka 48, leo hii tukisema tunauvunja tunaanza wapi na tunakwenda wapi?

Wazanzibari Tume itakuja, tutaamua tunayoyataka, tutaendelea na nchi yetu, lakini tutahakikisha kwamba haki za Wazanzibari zinapatikana. Baada ya hayo sasa naomba kuingia katika kitabu cha hotuba katika ukurasa wa 22.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze tena Makamo wa Pili wa Rais kwa ahadi zake nyingi ambazo amezitoa, lakini pia ahadi ambazo zimetekelezwa. Mimi nafikiri ahadi nyingi ambazo amezitoa Makamo wa Pili wa Rais zimetekelezwa, na naamini kwamba zile kidogo ambazo zimebakia basi itakuwa zipo katika mchakato wa kutekelezwa.

Katika ukurasa wa 22 unaosema Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mimi nawapa pongezi sana, kwa sababu asilimia kubwa ya wafanyakazi katika Idara hii basi wamepata fursa ya kupata masomo ya kuongeza ujuzi wao na elimu yao. Mimi nampongeza sana Waziri kwa kazi hii. Ningeomba nafasi hizi zinapotolewa sio ziende kwa watu maalum, au ziende katika jinsia maalum. Tunaomba wanawake mtufikirie mtuone zinapotokea nafasi za kusoma basi wanawake na wanaume iwe sawa sawa.

Vile vile naipongeza Wizara yako kuhusu suala la sera na utafiti, nafikiri kwa mwaka huu kwa kushirikiana na Chuo cha *SUZA*. Mimi nafikiria kwamba kuna tafiti nyingi sana ambazo zinatakiwa kufanywa.Kwa hiyo Wizara yako Mhe. Waziri nafikiri imeamua vizuri zaidi kutoa kifungu cha fedha ambacho kitasaidia katika utafiti huo. Tukumbuke kwamba wenzetu wengi wameendelea kutokana na tafiti mbali mbali ambazo zimefanywa. Mimi naipongeza sana Wizara kwa kukiamini Chuo cha *SUZA* kuwapa jukumu la kusimamia masuala ya tafiti.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maafa Mhe. Waziri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu ambapo mara nyingi sana tunatembelea Idara mbali mbali. Kwanza nawapongeza sana watendaji wa Idara ya Maafa, watendaji wengi katika idara hiyo wana ujuzi wa kutosha na wanafanya kazi vizuri tena katika mazingira magumu. Hata vifaa vya kufanyia kazi hawana, usafiri hawana.

Ningeliomba Idara hii muitizame kwa moyo wa huruma. Isitoshe tunafahamu sasa hali iliyokuwepo, Mungu atunusuru lakini maafa ni kitu ambacho sasa hivi tunakitarajia wakati wowote. Kwa hiyo tuhakikishe katika stoo zao kuna vifaa vitakavyoweza kutosheleza pindipo maafa yatakapotokea.

Vile vile naipongeza Idara ya Upigaji Chapa, kwa kweli wamestahamili muda mrefu sana kuwepo katika eneo lile ambalo lilikuwa sio eneo sahihi la kufanya kazi. Lakini leo naipongeza Wizara kwa kuwapa fursa watendaji wa idara ile kwenda katika eneo jengine ambalo lipo katika matengenezo ambayo Mwenyezi Mungu akijaalia mwaka huu wa fedha watamaliza na wataanza kazi zao. Naamini hapa ndipo itakapokuwa sehemu ya kuweka kumbukumbu na siri za Serikali. Sasa hivi uchapaji unakwenda kiholela. Matokeo yake hata zile sehemu za kuweka kumbukumbu na siri za Serikali hatuna katika eneo ambalo walilokuwepo. Mimi ningefurahi zaidi hata lile gazeti letu kwa sasa basi utakuwa wakati muafaka wa kuweza gazeti lile kuchapishwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ningeomba tunakuja kwenye Tume ya Uchaguzi huwa kawaida inapofika karibu ya uchaguzi ndio inapoanza kuhangaika na kuanza kutaka kutoa elimu ya uraia. Nasema hayo kwa sababu nakumbuka wakati nipo katika Asasi zisizo za kiserikali, nakumbuka vizuri sana. Wakati wa kura ya maoni na uchaguzi tulibahatika kupata nafasi kutoka Tume ya Uchaguzi pamoja na *UNDP* dakika ya mwisho, tunaambiwa tuwafundishe raia elimu ya kupiga kura au elimu ya kutoa maoni. Nafikiria hilo tungekuwa tunajipanga mapema.

Elimu kubwa inahitajika sana, lazima wananchi waanze kutambua umuhimu wa kupiga kura, umuhimu wa kuchagua viongozi wao, umuhimu wa kuitengeneza Serikali yao. Mhe. Waziri hili ni muhimu sana tena sana. Na halitaki muwe wa mwisho, linataka pale ambapo tunaona kwamba tuna fedha ambazo tunakwenda kuzitumia katika kutoa elimu ya uraia. Siku zote huwa nasema elimu ya Uraia kwa kweli inaanza tangu mtoto akiwa skuli. Tunataka watoto wetu wajitambue wao ni kina nani na kwa nini wapo katika taifa hili. Lakini waje watambue hapo baadae majukumu yao wakiwa watu wazima, ni majukumu gani wanayo kwa taifa lao. Hii ndio elimu ya kutolewa kwa watoto wetu. Mhe. Waziri ningekuomba sana wizara yako ilifikirie suala hili na ihakikishe kwamba inafanya kazi pamoja na Wizara ya Elimu kuhakikisha elimu ya uraia inatolewa kuanzia darasa la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, naingia kwenye suala nyeti. Leo kwa bahati mbaya au nzuri nilikuwa nina maneno nataka kumwambia Spika. Maneno yangu nilikuwa nataka kumwambia hivi Spika. Tunapokwenda kwenye Kamati maneno tunayoelezwa na watu tunajisikia vibaya, kwa sababu ya matatizo ya ardhi. Tumekwenda Uroa wametuuliza umekuja kufanya nini? Kula? Mngetwambia mapema tukakutayarishieni, maana nyie sio wa kwanza kuja.

Sasa Mhe. Makamo wa Pili ulipoingia Serikalini ulisimama kidete kuzungumzia suala la ardhi, tunakupongeza kwa hilo. Na ukataka watu wapewe haki zao na ukataka maeneo mengi ambayo yamechukuliwa yarudishwe. Lakini ile nguvu imepungua iko wapi? Watu wanalalamika wanatwambia nyinyi viongozi ndio mnaotuchukulia ardhi zetu. Wamesema tumefika pahala mpaka eneo la makaburi la wananchi limejengwa hoteli. Eneo la makaburi la mwisho mnatufufulia wazee wetu? Muwekezaji kapewa.
Baya zaidi siku ambayo tumekwenda siku moja kabla au siku mbili Mhe. Rais, mpenzi wetu amepelekwa kwenye hoteli hiyo kula chakula cha mchana. Tukaambiwa kwamba hapa wamekuja wametwambia msiseme kitu kwa sababu Rais anakuja.

Mhe. Makamo wa Pili kesi zipo nyingi, mimi nimeshafatwa mpaka nyumbani mara mbili watu wananiletea *documents* za haki zao wanadai, hawajui masikini wapi waende. Tukikaa kimya kila siku, hakuna kinachotatulika ndiyo hayo ambayo mengine tunayaona yanazuka, kwa sababu watu wanakuwa na uchungu wa haki zao. Kama ikiwa ardhi ni ya Serikali kwa nini Serikali ishindwe kufanya kazi zake.

Mhe. Makamo wa Pili nakuomba mimi nilikuwa leo nimwambie Spika, kwamba usinipeleke tena katika Kamati najua sivyo kanuni haisemi hivyo. Nilikuwa nataka kumwambia, kwa sababu mie ni mtu wa haya, naona haya kwenda kule wananchi wakanisuta kwa maneno, sipendi kusutwa mie. Na wao wanasema ukweli, wana uchungu wananchi.

Tumekwenda pahala muwekezaji anaingia usiku na dude lake anachimba mchanga, wananchi wamepiga picha na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Wamepiga picha wameziweka ukutani wanatwambia haya ndio mambo yanayotufika sisi. Hawa wananchi watasemewa na nani jamani.

Kwa hiyo Mhe. Makamo wa Pili, tunakuomba wewe ndiye mwenye serikali, tunakuomba sisi Wawakilishi tena mimi naungana na yule ambaye alisema anataka iundwe Tume kuhusiana na masuala ya ardhi. Namuunga mkono, dalili inavyoonesha kwamba hapa suluhisho halitopatikana.

Mwisho kabisa Mhe. Waziri niipongeze tena Wizara yako kwa hatua ambayo imefikia ya kutaka Baraza kuwa na muhimili wake. Hatua iliyofikia ni nzuri na sisi tuna matarajio kwamba taratibu hiyo haitochukua muda Baraza liwe muhimili kama mihimili mengine, isiwe ndani ya muhimili mwengine bali ijitegemee.

Mhe. Waziri nina ombi, sisi tulivyoanza kuja hapa katika Baraza tumekuja kama vipofu, wengine wetu hatujui kitu, wengi wetu ni wanasiasa wa mitaani wengine hata hawakuwa wana siasa. Tumefika hapa tunaanza moja kwa moja kuambiwa kupitia Miswada na kuipitisha bila ya kupata mafunzo ya aina yoyote na tumepitisha Miswada. Sasa hivi mimi ndio naanza kujiuliza hivi ilikuwa ni uhakika au ni vizuri kwamba tumepitisha Miswada wakati hatujui, kama tumedanganywa au kama tumetupiwa changa la macho je? Lakini hapa nasema asilimia kubwa ni wapya waliokuwemo kwenye Baraza hili. Hamkututendea haki.

Mhe. Waziri tunakuomba tena hili lisirudiwe, wenzetu Wabunge wanapoanza Bunge wanapewa mafunzo kamili ambayo yanamsaidia Mbunge kuhakikisha kwamba ataweza kusimama na kutetea haki za wananchi ambao wamemchagua. Mafunnzo ya kupitisha Mswada ambapo utahakikisha kwamba Mswada ule ndio utakaotumika Serikalini. Hivi tutakuwa hatujafanya kitu sawa sawa na ziro.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nataka nizungumzie Kamati katika Baraza. Katika Mabunge mengi Kamati huwa zinakaa na inategemea aina ya Kamati. Kuna Kamati ambazo zinashughulikia masuala kama ya fedha. Kama zile huwa zinakaa muda mrefu zaidi ya miaka miwili na nusu. Kama zile huwa zinapewa mafunzo maalum. Leo nasikia hapa kwamba kamati zile kama ya PAC, Kama ile baada ya miaka miwili na nusu inabadilika inaondoshwa.

Mimi natoa wazo, nafikiria kwamba hakuna haja ya Kamati kama ile kubadilisha. Kwa sababu wale tayari watakuwa wana utaalamu wa kutosha. Leo ukinichukua mie mgeni ukianza kunipeleka kwenye Kamati ile japo kuwa si mzito wa kujifunza, lakini naamini kwamba itachukua muda mpaka nikaweza kushika yale ambayo yaliyokuwepo. Mimi naomba kuna baadhi na sijui kama tatubadilisha kanuni au vipi. Lakini naomba kuwa Kamati kama hizi Mhe. Waziri nafikiri kwa sababu zitakuwa zimeshakuwa na ujuzi wa kutosha basi ziendelee hivyo hivyo. Kamati nyengine tunaweza tukachanganya lakini hizi *special* ziachiwe ili zifanye kazi zake vizuri zaidi.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niwaombe ndugu zangu Wazanzibari tutulie, Tume ya Katiba inakuja. Tutulie ili tuweze kutoa maoni yetu. Maoni yetu mimi nina hakika kwa hapa tulipofikia sasa hivi ambaye kila anayesimama anasema kwamba Muungano una matatizo. Basi mimi naamini kwamba hili ambalo tunalitaka sisi litatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesikitishwa sana na suala zima la kuchukua watoto kuwatia katika maandamano ambayo hayajawahusu. Nawaomba akina mama wenzangu kwa sababu wao wanakuwepo na watoto wanakuwa mbele. Nawaomba sana na mimi pia ni mzazi, watoto wenu msiwahusishe katika masuala haya. Kwanza lolote litakalotokea mkosa ni wewe mzazi unayemchukua mtoto wako ukampeleka kwenye maandamano au shughuli zozote za kisiasa. Pili ni uvunjaji wa sheria kumchukua mtoto ukampeleka maeneo ambayo mtoto hahusiki, ni uvunjaji wa sheria wa kimataifa nawatahadharisha akina mama msije mkajikuta kwenye matatizo, watoto waachieni nyumbani na hata nyinyi nakushaurini mkae nyumbani mtulie, maoni yenu yatazingatiwa na Inshaallah Mwenyezi Mungu atajaalia haki zetu tutazipata. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kupata fursa ya kusema machache kuhusu mustakbali wa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yetu hivi sasa kuna maneno mawili ambayo yamebahatika sana kuwa utumiaji wake ni mpana mno. Waheshimiwa hapa wengi ni weledi, wamejifaragua kila mmoja amelieleza jinsi uweledi wake ulivyomfikisha. Mpaka wananchi na wao maneno haya mawili wanayatumia kwa upana sana hivi sasa, mpaka watoto wadogo, Maimamu na Mashekhe wote maneno haya wameyapa kipaumbele na ndiyo wanayoyatumia.

Hii inanithibitishia wale wataalamu wa lugha waliposema kwamba, lugha ni kuchagua neno halafu ukaliunganisha na jengine ndio ukapata maana. Kipindi hichi tulichonacho wamechagua katika maneno yote ya Kiswahili

wamechagua neno Muungano. Katika sifa zilizomo katika lugha ya Kiswahili wakachagua neno hatuutaki. Kwa hiyo hii ikawa ni ujumbe kuwapelekea wale waliohusuka. Nafikiri ujumbe huu umefika na umefika wakati wake.

Mhe. Mwenyekiti, kama mimi ningekuwa ni profesa katika Chuo Kikuu na nikapewa fursa ya wanafunzi hawa niwasomeshe somo hili la muungano, basi mwaka huu nisengeliwafanyisha mtihani. Ningewambia nyinyi subirini ile siku ya mahafali kwa sababu uelewa mlionao ni mkubwa sana kuhusu suala hili. Nina imani kwamba ujumbe umefika na kila mtu ameufahamu. Lakini tunapokuwa Chuo Kikuu mara nyingi huwa tunafanya mambo *theory* na *practical* ili lile ulilolifanyia *theory* ulithibitishe zaidi ili upate uelewa mkubwa zaidi. Sisi upande wa *theory* tumemaliza tulichobakia ni kuwezeshwa kufanya ile sehemu ya pili ambayo ni *practical* tupate kufahamu zaidi, na kufikia lengo tunalolifanikiwa. Kuhusu hilo nimalizie hapo.

Mhe. Mwenyekiti, Bajeti hii imeelezea kuhusu Ofisi ya Faragha. Unajua kila ng'ombe au kila mbuzi waswahili wanasema anakula kutokana na urefu wa ile kamba yake. Hivi sasa kinachojitokeza ni kwamba kuna ujanja mwingi, na wengi katika sisi huwa tunatumia ujanja huo kwa ajili ya kutufanikishia kukipata kile tunachokihitaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Ofisi yetu ya Faragha ambayo mara nyingi huwa inaandaa safari za kwenda ndani ya nchi au nje ya nchi. Kwa mara hii tumetajiwa zaidi ya safari tano (5) ambazo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amezienda. Mimi nimekuwa nina wasiwasi kuhusu hizi safari zetu. Wakati unapofika wa safari msafara unakuwa ni mkubwa kiasi kwamba unakuwa ni mzigo kwa Serikali. Inabidi wanaokwenda kule tuwahudumie. Sina kumbukumbu rasmi lakini nina imani kwamba ujumbe uliokwenda Marekani ulikuwa haupungui watu 20. Sijui walichokwenda kufanya, lakini kwa nchi kama yetu kupeleka watu 20 na gharama zake za kila siku za wiki nzima. Mhe. Waziri wa Fedha asingeweza kutwambia kwamba jamani tuongeze kodi ili tupate kuondoa nakisi katika bajeti yetu. Lakini amekuja hapa ametwambia kwamba nakisi itabidi tuibebe sisi. Kwa hivyo sisi akatuongezea kodi katika *propela* kwenye mafuta ambapo kwenye mafuta kila kitu likizunguka tu *propela* itapanda juu.

Mimi ningependa kuwambia hawa wanaoandaa mambo haya kwamba ujumbe unaokwenda basi uangalie na uwezo wetu. Uwezo wetu bado ni mdogo kama ni ujumbe wa watu 20 basi ingepunguzwa, nafikiri Taifa lingepungua mzigo. Je, niulize tena katika safari zetu zote hizi ambazo tulikwenda kuna nini ambacho kilichopatikana na nini utekelezaji wake. Je, kuna faida yoyote ambayo taifa hili itaipata katika hilo au watu inabidi tuende tu kwa sababu tunakwenda New York mimi sijakwenda waende kutembea na baadae warudi hapa ikawa hakuna lolote lililofanyikana.

Mhe. Mwenyekiti katika hilo lile lile nililosema kwamba tuna ujanja wa kutafuta majani kwa ajili ya kula. Hapa tumeelezwa kwamba tuna gari imetengenezwa kuna mmoja kavumbua gari, na katika hesabu zake tumeambiwa kapewa tunzo ya shilingi milioni mbili. Lakini pia zimetumika milioni kumi na mbili katika kununua vifaa, sasa mimi najiuliza huyu mtu kavumbua huyu au kafufua kwa sababu naona kapewa pesa kwa ajili ya kununua vifaa kutiwa katika hilo dude alilolitengeneza na liko wapi labda Mhe. Waziri atakuja kutwambia liko wapi na lina utambulisho kiasi gani kwamba kweli linapata *international recognition* kiasi kwamba atawekwa katika kile kitabu cha *guinness;* kwamba mzanzibari sasa kavumbua gari au mlikuwa mnafanya mbinu za kupata ile milioni kumi na mbili labda ziingie katika mifuko mengine. Hebu Mhe. Waziri tusaidie hapa mimi nahisi hapa ni mbinu moja tu ya kuweza kujipatia chochote na baadae mkatwambia bajeti iko nakisi tukaanza kutoa sisi migongoni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni Idara ya Uratibu ya shughuli zetu iliyopo Dar es Salaam shughuli za SMZ. Ilivyokua najua siku za nyuma kwamba Idara hii ilikuwa inaandaa hasa mipango ya wanafunzi kutoka Zanzibar kupata *scholarships,* na mimi mmoja nilibahatika kupata *scholarship* kupitia Ofisi hii katika miaka ya 1980. Lakini Idara hii naihisi hivi sasa ipo tu shughuli zake zimekuwa ni chache sana, hata hii shughuli ya kutafutia fursa za masomo nchi za nje basi haipo. Na labda ningemuoma Mhe. Waziri atakapokuja hapa akatueleza hebu hiyo Ofisi yetu siku hizi baada ya kuratibu hizi shughuli za masomo zinazokuja kupitia Serikali ya Muungano sisi mara hii tumepata ngapi na tumekwenda wapi wanafunzi wetu tumewapeleka wapi kwenda kujifunza mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pia kitabu chetu kimezungumzia suala la AK na JK, mifuko hii imeanza zamani na nilikuwa na imani kwamba mifuko hii itakuja kuboresha hali za wananchi lakini sivyo ilivyo. Kitabu kimetueleza kwamba kuna karibu bilioni moja lakini je *out come* yake iko wapi? Wizara inatwambia hivi sasa kwamba wanakwenda katika mpango maalum yaani kuna vipaumbele vya taifa ambavyo vimewekwa. Sasa je katika miradi yetu hii ambayo iko chini ya AK na JK pia inazingatia programu yetu ya taifa ili kusaidia kupeleka mbele au tunawawezesha

wananchi tu tunawapa pesa wakijua kwamba pesa hizi sisi tumepewa *for political reasons*, na nahisi zaidi mfuko huu umekuja kwa ajili hiyo siyo kwa ajili ya kuwapa wananchi uwezo, yaani ajira lakini ajira yenyewe inayotokea hapa una-*occupy* tu basi lakini huwapi kazi kwa maana wapate *profit* ili waweze kujitegemea wao.

Kwa hivyo mimi ninahisi mfuko huu ungekuja na utaratibu mwengine ili kumuwezesha mtu akaweza kujitegemea. Lakini milioni moja tumezigawa kwa watu wasiopungua mia kwa maana hiyo kila mmoja atakuwa kapata laki moja. Sasa laki moja ukiipeleka katika soko la biashara hivi sasa atakuwa *nill* huyu, matokeo yake atazila hana uwezo wa kufanya lolote na kesho atakuja kukwambia mimi sina ajira. Kwa hivyo ningeomba tu sasa katika mfuko huu tukatafuta utaratibu mwengine.

Mhe. Mwenyekiti wengi wamezungumzia mgogoro wa ardhi lakini mimi ningependa niulize, ninachokijua ni kwamba ardhi bado ni mali ya serikali sasa je ina maana hata katika hii mali yake yenyewe serikali imeshindwa kutatua tatizo hili? Hata kujilindia mali yake yenyewe imeshindwa? Lakini jengine tuna migogoro ambayo haiko mikononi mwetu tunayo migogoro labda tumeita ni changamoto za muungano au kero za muungano. Sasa hata haya sisi yamo mikononi mwetu Mhe. Mwenyekiti tumeshindwa kuyafanyia kazi? Kiasi kwamba leo kila kona unayopita unakutia kuna mgogoro wa ardhi. Lakini cha kushangaza ni kwamba kuna sheria inayosema kwamba umiliki wa ardhi kwa wale ambao wamemilikishwa na serikali kama imefika miaka miwili hujaitumia inatakiwa serikali ihodhi ichukue wenyewe.

Na miezi mitatu iliyopita Mhe. Mwenyekiti niliona zoezi hili likifanyika katika maeneo ya Kijichi na Bububu na wafanyakazi wa Idara ya Upimaji walipita maeneo tofauti kuratibu viwanja ambavyo vimefikia muda wa miaka miwili na havijatumiwa. Sasa sijui zoezi lile limefikia hatua gani. Je wale ambao wamepitiwa na wakati muda umefika viwanja vile wamepokonywa na kupewa walio navyo vyengine au bado wanaendelea navyo na sijui zoezi hili limetupa picha gani. Wapo wangapi ambao viwanja vile vimepitiwa na wakati na tayari Idara imevirudisha kwao wako tayari kuwapa watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti sasa kidogo nije katika utaratibu wa Baraza au Baraza la Wawakilishi. Nilivyokuwa ninajua kwamba sisi ni moja kati ya mihimili mitatu ya nchi hii. Lakini juzi nilipata maelezo mengi na nikafikia uamuzi labda sasa sisi Baraza la Wawakilishi tumekuwa kama ni PP yaani *public prosecutor*, kuna hakimu yeye ataamua masuala yale. Sasa ripoti zetu kwa maana hiyo haziko kamili hazijitegemei, kwa hivyo sisi tunahitaji mtu mwengine aje kuzifanyia utafiti tena zaidi ripoti zile. Sasa hii itakuwa ni kupoteza muda.
Sasa kama sisi ni PP tumempelekea hakimu, hakimu ni *executive.* Sasa *executive* atajihukumu vipi yeye itakuwa sasa tunapoteza wakati. Tukija hapa tutaambiwa aa bado tumo katika kulifuatilia hili suala na hii ndio njia ya serikali hivi sasa ya kutujibu sisi Waheshimiwa masuala yetu mbali mbali. Tuko mbioni, karibu tutafikia hatua fulani, karibu tutafanya hivi. Sasa leo mimi ninajiuliza kesho tunakuja kupitia bajeti ambazo kuna watuhumiwa waliotuhumiwa na Baraza letu tukufu, sasa nitakuwa na uhalali gani mimi wa kumthibitishia yule au kumuidhinishia matumizi na mimi ndio naambiwa *accounting officer* kwamba yeye awe ndio mtumiaji wa pesa zile. Lakini yeye huku ni *prime suspect*, sasa je kutakuwa na uhalali huo mimi wa kuwa nimtilie pesa zile.

Sasa Mhe. Waziri sisi hatutaki tufikie huko, ninafikiri kama ripoti imekuja basi kunahitajika ifanyiwe kazi mapema kabla hatujafika tukaingia katika migogoro ya kisheria yamalizike mapema haya ili tusije tukafikia hatua hiyo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, labda niseme neno moja kwamba sisi mara nyingi huwa ndio tunayaona yale mambo huwa mara nyingi ukiona uchafu unakimbia chooni ili kujisafisha.

Sasa sisi Waheshimiwa tulichokifanya mara hii kwamba tulipofika chooni tukaona aa tuna uchafu tukajitia sabuni, tulipojitia sabuni tukaona aa tushasafika sasa tukatoka nje kumbe sivyo tumeingia uchafu zaidi kwa sababu yale tuliyoyaona sasa yameshafika kwa wananchi. Sasa imekuwa sisi tuna kero, serikali na wao wana kero kutoka kwetu tufanye nini? La msingi Mhe. Mwenyekiti ninafikiri sasa itabidi ile ya mwanzo tuliyoitumia tujitie sabuni sisi aa *no*, tuibadilishe sasa tuanze na kujitia maji. Tukijitia maji halafu tujitie sabuni halafu tujitie na maji tena tutasafika, hapo ndipo tutakapofika Mhe. Mwenyekiti, kama si hivyo itakuwa ni kurudi kule kule. Tumekwambieni, tuko mbioni na la kushangaza kabisa mbio hizi hawatwambii wameanzia wapi, kwamba labda sisi Mhe. Mwenyekiti tutaanza mbio Gombani tutamalizia uwanja wa Amani Stadium, tungepata angalau ile imani kidogo kwamba haya masuala yatatatuka.

Na pengine alau wangetwambia kwamba aa hizi mbio bwana ukubwa wake ni kilomita moja kwa sababu huko ulimwenguni kuna vipimo maalum vilivyowekwa ya kwamba kila kilomita moja mkimbiaji anatakiwa akimbie saa

mbili na dakika fulani. Kwa nini ninasema hivyo, kwa sababu mimi nina imani kwamba hizi mbio wanazokwenda mwaka huu huenda wakavunja rekodi ya dunia, kwa hivyo sisi tujiandae kuja kuwapokea kwa shangwe. Kwa sababu Zanzibar mara hii itakuwa rekodi yake imepita hii.

Mhe. Mwenyekiti mimi naona nimalizie hapo niwape wenzangu nafasi.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwanza nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake wote wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti mimi nitaanza hapo hapo na mgogoro wa ardhi ambao hili ni kero kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenayekiti kitabu cha Mhe. Waziri anasema migogoro yote 35 iko katika sheria na mengine amewaachia masheha na Wakuu wa Wilaya. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti mimi najiuliza sana, kwa nini hii Serikali ishindwe ikamwachia masuala kama haya yule mtendaji ambaye ameshafanya suala hili baada ya yeye ahukumiwe ajihukumu mwenyewe, hebu tujiulizeni hili limetokea wapi? Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hapa hujawatendea haki wananchi hata kidogo, ninaiomba serikali kwa suala hili isimwachie Mkuu wa Mkoa, isimwachie Mkuu wa Wilaya, isimwachie hata Sheha kwa sababu haya ndiyo yanayosababisha matatizo. Na matatizo haya yanaanza kwa masheha, sasa kama matatizo yanaanza kwa masheha Mhe. Mwenyekiti usimpe mtu ajihukumu mwenyewe, ahukumiwe kunakohusika, haya ndio mawazo yangu.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri masuala haya ya migogoro ya ardhi na mengine yanasababisha mizozo kwenye wilaya huko hata kunyimwa vitambulisho vya uzanzibari, kutokana na wilaya na masheha. Sababu yote hiyo Mhe. Mawaziri mimi naona kwa upande wangu hawa wanateuliwa hawachaguliwi na wananchi wenyewe ndio maana matatizo haya yanajitokeza. Kwa hivyo ninaiomba serikali kama kuna sheria tuiondoe tubadilishe tuweke Sheha, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, tuwachague sio wateuliwe na Rais tena asipewe majukumu makubwa Mhe. Rais mazito mengine yanamzidi tumsaidie.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kuondoka hapo naenda sehemu ya sensa ya watu na makaazi. Hapa tunaambiwa tuwaelimishe wananchi wetu kutokana na sensa ili wahesabiwe, lakini Mhe. Mwenyekiti hapa ninaiomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndio watu wetu wahesabiwe lakini katika nchi yetu sisi tuna wazanzibari na wazanzibara. Sasa hapa tu hizi takwimu zitakazokuja mimi naomba wazanzibari takwimu yao iwe mbali na wazanzibara takwimu yao iwe mbali, ikisha itolewe takwimu ya pamoja.

Halafu vile vile hapa Mhe. Mwenyekiti nizungumzie masuala haya ya vitambulisho vya mzanzibari hapa ile sheria iliyowekwa inawakandamiza wazanzibari. Kweli Mhe. Mwenyekiti mtu wa miaka 60 akalishwe kiapo kama vile kaiba hatuwatendei haki wazanzibari tunawanyima haki zao kwa makusudi serikali hii. Kwa hivyo serikali inabeba dhima kubwa ikesha haiwatekelezei wananchi wake. Kwa maana hiyo sheria iletwe tuirekebishe vizuri kila mzanzibari awe na haki yake aipate ya vitambulisho anaefikia miaka 18.

Kwa kuendelea Mhe. Mwenyekiti niende sehemu ya maafa. Hapa Mhe. Mwenyekiti mimi ninatoa msisitizo tu kwa serikali, kuwa serikali yetu mpaka litokee jambo lenyewe ndio idara hii ndio ifanye kazi zake. Lakini ninaiomba serikali itoe taarifa kabla ya kutokea maafa yenyewe.

Halafu maafa mengine Mhe. Mwenyekiti serikali yetu inajitakia, kwa sababu meli zetu zote mbovu, si ya kujitakia haya sasa serikali vyombo kama hivi wavifanyie utafiti je hivi vinachukua muda gani, vizima, vibovu kila siku tutauana hapa, ukesha tuseme maafa haya ya kujitakia Makamo wa Pili wa Rais tuyafanyie kazi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa ruhsa leo kuchangia kitabu hiki cha hotuba ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mheshimiwa mimi nitaanzia sehemu hii ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yetu tuna vijana wengi, tuna wananchi wengi hususan vijana wanakosa ajira, kwa hivyo serikali ningeliomba kwanza iwape taaluma wananchi vipi wananchi wanajiendesha kiuchumi. Kwa sababu

wananchi wengi wanafanya kazi lakini wanatumia maguvu tu lakini utaalamu hawana. Kwa hivyo ningeliiomba serikali kwamba waelimishe wananchi jinsi ya kujiendeleza kiuchumi.

La pili nchi yetu imeuza ardhi yote lakini imekosa kuweka akiba hata ya kuweka viwanda kwa sababu nchi yoyote kama haina viwanda haiwezi ikaendelea, wananchi wake watakuwa wanakwenda tu wanakosa ajira kwa sababu hapana nyanja za kufanyia kazi. Tukienda katika sehemu zetu katika majimbo yetu ya mashamba wengi vijana ambao wamesoma kidogo lakini hawana ajira kwa sababu ajira hakuna pa kupatikana. Nchi yetu imeogelea katika mahoteli sasa wengi hawapati katika sehemu zile za hoteli kwa hivyo tatizo la ajira limekuwa limetuzonga sana.

Kwa hivyo ningeliomba kwamba, serikali inajitahidi sana kukopesha wananchi fedha, lakini inawakopesha fedha za chajio tu lakini haikopeshi fedha za maendeleo. Serikali ijitahidi kuwapa vifaa wananchi wajiendeleze, ukimpa kifaa mwananchi atajiendeleza lakini ukimpa fedha mwananchi atazitumia kwa sababu hana elimu nazo. Serikali iweke fedha iwawezeshe wananchi zana za kufanyia kazi ikiwa elimu waelimishwe wananchi. Lakini itakuwa leo mwananchi anapewa shilingi thalathini elfu, thalathini elfu kwa leo ni samaki mmoja tu lakini mwananchi apewe kinu cha kusagia nafaka halafu aelimishwe kweli hatokwenda? Wananchi wajengewe viwanda vidogo vidogo halafu waelimishwe katika vyombo vidogo vidogo kweli hawatokwenda? Kwa hivyo ninaiomba serikali iweke mfumo huu wananchi waelimishwe, bila ya kuelimishwa mwananchi hawezi kwenda.

Mhe. Mwenyekiti nikienda katika ukurasa wa 12 katika migogoro ya ardhi, migogoro ya ardhi kitabu chetu kinasema inasababishwa na baadhi ya wakubwa. Sasa mimi najiuliza wakubwa wepi wanaosababisha migogoro ya ardhi. Mimi naona wakubwa wote wamo humu ndani serikali nzima imo humu ndani, humu kabakisha Mhe. Rais na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Mawaziri wamo humu, Wawakilishi wamo humu, Wakuu wa mikoa wanakuja humu humu, watendaji wanakuja humu humu. Sasa sisi tunawaambia wananchi kwamba migogoro ya ardhi inasababishwa na wakubwa, wakubwa wepi kama si sisi. Sasa kama kweli wakubwa wanasababisha migogoro tuende tukawavamie wakubwa wanaosababisha migogoro ya ardhi tuwatoe ndani ya serikali.

Lakini tunaambiwa wakubwa wanasababisha migogoro ya ardhi, wakubwa ni wepi wameshatajwa humu wakuu wa mikoa, kama wakuu wa mikoa ndio wanaosababisha migogoro ya ardhi kwa nini hawafukuzwi kazi? Wanatupa matatizo katika serikali yetu, wananchi wetu wanatudharau kwa sababu kila siku tukienda kule wanatwambia kwamba wakubwa ndio wanasababisha wakubwa wepi, wakubwa ndio sisi, ikiwa wakubwa ndio sisi kwa hivyo ardhi tumeikumba sisi tunawadhulumu wananchi tuwarejeshee ardhi zao.

Mhe. Mwenyekiti mimi mchango wangu si mkubwa sana, mchango wangu ni mdogo lakini ninaiomba serikali iwaangalie vijana, vijana hawana ajira, vijana wapewe nyanja za kufanyia kazi. Tuna majimbo yetu kule kama jimbo langu la Matemwe, hakuna hata nyanja moja iliyokuwa vijana wamo katika kazi. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali sisi kule tumezungukwa na bahari, samaki wengi tunavua vijengwe viwanda kule wananchi wapate ajira. Hii Muamsho yote inakuja kwa sababu tunaamshwa wananchi wapate ajira. Wananchi wameamua kutuamsha kwamba hawana ajira sasa tufanye maarifa wapate ajira.

Mheshimiwa ninakwenda katika sekta ya walemavu. Mhe. Mwenyekiti tuna walemavu wengi sasa hivi katika nchi yetu nao vile vile hawajapata haki zao za ulemavu. Kwa hivyo ninaiomba serikali iwapitie walemavu ndani ya majimbo yetu waajiriwe walemavu hawana ajira wengine hawawezi chochote, kwa hivyo wapate misaada walemavu.

Mhe. Mwenyekiti bila ya kupoteza wakati wako adhimu mimi ninaishia hapa. Ninaiomba serikali bajeti hii iweke maarifa ya kuwawezesha wananchi kuwapa elimu na kuwajengea zana za kufanyia kazi. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Ofisi muhimu sana hii, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ambayo inashughulikia suala zima katika utendaji wa serikali. Lakini pia ndio ofisi inayosimamia Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Ofisi yako ndio inayohusika na suala zima la utendaji kazi katika serikali, lakini kwa kweli suala la utendaji katika serikali bado linaonekana haliendi vizuri, na kwa sababu bado wafanyakazi wa serikali wanaonekana ama hawajui vizuri wajibu wao katika nchi hii au hawasimamiwi vizuri katika utendaji wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli utendaji katika serikali umekuwa dhaifu mno na suala hili linarejesha maendeleo katika nchi hii. Wafanyakazi wengi serikalini hawafanyi kazi kwa mujibu wa masaa yao ya kazi, na kwa kweli katika hali kama hii Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama utaiacha iendelee kwenda hivyo basi maendeleo hayawezi kupatikana hata siku moja. Sisi tunajua Mhe. Makamu wa Pili kwamba kuna masaa ya kazi, wafanyakazi wanatakiwa wafike kazini saa moja na nusu na waondoke saa tisa na nusu, lakini wafanyakazi wetu wa Zanzibar utakapokwenda kwenye ofisi yoyote ya serikali labda kuanzia saa mbili na nusu, na utakapokwenda saa tisa na nusu basi ofisini hakuna mtu. Kwa hivyo, hii ni hatari katika masuala mazima ya utendaji wa kazi.

Mimi sisemi kwamba uwafatilie wafanyakazi maofisini mwao sisemi hivyo, kwa sababu wenye mamlaka ya kuwasimamia wafanyakazi wapo, Wakurugenzi, Makatibu Wakuu, hawa ndio wenye dhamana ya kusimamia wafanyakazi wa serikali na kuhakikisha kwamba wanafika kazini kwa wakati na wanaondoka kwa wakati. Sasa hawa ndio waliokuwa chini yako na hawa ndio unaotakiwa uwasimamie kwa karibu kuona wanatekeleza wajibu wao wa kuwasimamia wafanyakazi. Lakini leo inashangaza unafika ofisini hata Mkurugenzi mwenyewe na yeye anafika saa tatu, unakwenda ofisini unamtafuta Mkurugenzi unaambiwa saa mbili na nusu au tatu hajafika sasa utegemee mfanyakazi yeye atafika saa ngapi.

Mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, kama Wakurugenzi wetu wangekuwa wanafika kazini mapema basi wafanyakazi na wao wangefika kazini mapema, lakini mtu keshajiona yeye tayari ni Mkurugenzi keshapewa na dhamana hana mtu wa kumuuliza basi anaamka nyumbani muda anaotaka, anakwenda kazini muda anaotaka, kwa kweli hii sio tabia nzuri na sio ufanyaji kazi bora. Kwa hivyo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tunakuomba sana hili ulisimamie, uwasimamie Wakurugenzi kuhakikisha wafanyakazi wao wanafika kazini kwa wakati.

Cha kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine hata zile sehemu za kukusanya mapato unakwenda ofisini saa mbili kulipa mapato ya serikali unaambiwa *cashier* hayupo hajafika, saa mbili, saa mbili na nusu, saa tatu *cashier* ndio kwanza anakuja kufungua ofisi watu wanamsubiri kuja kulipa fedha pale na fedha hizo ndizo ambazo tunazitegemea kwa ajili ya kuendesha serikali hii. Hili ni jambo la kusikitisha sana, kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais huu ni wajibu wako kusimamia kuhakikisha wafanyakazi wa serikali wanafika kazini kwa mujibu wa *time* zilizowekwa na wanaondoka kazini kwa mujibu wa wakati uliowekwa, huo ndio wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nije kwenye Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano ameteuwa Tume ya Kusimamia Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na muda si mrefu tume hiyo itaanza kazi kwa mujibu wa ratiba watakayojipangia. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sisi Wawakilishi wa wananchi tunajiuliza hivi tume hii itakapofika Zanzibar na kwenda katika maeneo mbali mbali tumeambiwa inaanzia Mkoa wa Kusini Unguna na Mkoa wa Kusini Pemba inategemea itapokea maoni gani kwa wananchi. Kwa sababu wananchi walio wengi sasa hivi hawajui waseme nini sisi wawakilishi wao wanatuuliza kwamba, hivi hii tume itakapokuja katika maeneo yetu sisi tukasema nini? Wanatuuliza hawajui la kusema.

Sasa katika hali ya kwenda mitaani, kwenda kwa wananchi, kwenda kuwauliza watu waliokuwa hawajui cha kusema tutegemee nini katika hilo. Serikali imechukua juhudi gani katika kuhakikisha kwamba wananchi wanafahamu cha kusema, wananchi wanafahamu nini madhumuni ya tume iliyoundwa, kwa kweli hata sisi wawakilishi wao tunajiuliza wananchi watasema nini.

Nilikuwa naangalia sheria hii iliyoanzisha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kama kuna eneo ambalo tume imepewa wajibu wa kufanya shughuli hiyo mbali ya yale makundi ambayo yameelezwa humo makundi ya kijamii, makundi ya hiyari. Nikaona hapa kifungu cha 17(2) (a) ambapo inazungumzia utaratibu wa utendaji wa kazi wa tume kinachosema, “kuandaa na kuendesha programu za kuelimisha juu ya madhumuni na majukumu ya tume”. Nilivyofahamu mimi maana yake ni kuelimisha jamii waelewe nini madhumuni ya tume na wananchi wanatakiwa wafanye nini tume itakapofika. Lakini sasa tujiulize kesho na keshokutwa tume inakuja mitaani imeshafanya hiyo shughuli? Jibu lake haijafanya, matokeo yake wanakwenda mitaani kwenda kuchukua maoni ya wananchi juu ya marekebisho ya katiba.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii ni kasoro kubwa ya shughuli hii muhimu ambayo kwa kweli ni shughuli tunayoitegemea sana ambayo itaweza kuondosha matatizo mbali mbali katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Sasa mimi nimekuwa na wasiwasi isije ikawa jambo hili linafanywa kwa makusudi ili wananchi wetu wakose uelewa kwa madhumuni ya kuundwa kwa tume hii. Mimi nikuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais

kwamba jambo hili tulione na wananchi wetu kukosa elimu juu ya jambo hili litasababisha waende ovyo, atakwenda mtu pale kusema mambo ambayo hayahusiani na jambo lenyewe, au pengine watu watashindwa kuhudhuria katika mikutano ile kwa sababu hawajui watakwenda kusema nini. Kwa hivyo, hili Mhe. Makamu nimesema niliseme na serikali mlijue na kama kuna hatua za kuchukuliwa juu ya jambo hili basi zichukuliwe.

Mhe. Makamu wa Pili tusifukuzie tu kwenda kwa wananchi kwenda kuwaambia watoe maoni yao bila ya kuwaelimisha, lazima tuanze mikutano ya kuwaelimisha wananchi waelewe madhumuni ya tume na sheria humu imeelekeza, mbali ya shughuli ya kwenda kuchukua maoni lakini kutoa elimu na watu wajue nini tume inatakiwa ifanye na wananchi wanatakiwa kufanya nini katika hili. Sasa mimi nimeona hii ni kasoro moja kubwa ambayo inahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie juu ya Mamlaka ya chombo hiki ambacho kiko ndani ya Ofisi yako, jambo ambalo limekuwa ama linapotoshwa kwa makusudi au halieleweki au vipi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi ambacho kiko chini yako au kiko chini ya ofisi yako kina mamlaka makubwa sana katika nchi hii na ni mamlaka ambayo kimepewa kwa mujibu wa katiba ya nchi. Mamlaka ya kwanza makubwa ambayo kimepewa chombo hiki ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma, hamna chombo kingine kwa tafsiri ya wepesi ni kuisimamia serikali katika utekelezaji wa shughuli zake mbali mbali. Tunafahamu mtu anapopewa dhamana ya kusimamia, kusimamia maana yake sio kuangalia tu mambo yanavyokwenda ni kuangalia na kutoa maamuzi. Baraza la Wawakilishi ni chombo cha maamuzi si chombo cha kusema tu, kinaweza kikatoa maamuzi, kinaweza kikashauri, kinaweza kikashauri na kutoa maamuzi juu ya jambo lolote linalohusu serikali. Kwa sababu sisi ndio wasimamizi.

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, halina muingiliano wa mihimili, lakini katika hali ya muingiliano pia katiba imeeleza kwamba, vyombo hivi vitaingiliana kwa mujibu wa katiba pale ilipotajwa katika katiba. Kwa hivyo, tutaisimamia serikali vizuri, tutashauri pale panapohitaji kushauri, lakini tutaamua panapohitaji kuamuliwa na lazima serikali ifuate maamuzi yanayotolewa na chombo hiki, vyenginevyo kufanya vyengine vyovyote ni kusababisha matatizo.

Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, nimesema nilizungumze hilo kwa sababu ya kukimbia hayo matatizo yatakayojitokeza baadae. Nakwambia kwamba Baraza la Wawakilishi ndilo lenye mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali, pale Baraza litakapoona kwamba huku serikali inakwenda siko basi Baraza litoe maelekezo wapi kwa kwenda kwa niaba ya wananchi.

Jengine la mwisho Mhe. Mwenyekiti, nisitumie muda wako mwingi juu ya suala la uratibu wa masuala ya Muungano. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ofisi yako ndio inayoshughulikia uratibu wa shughuli na masuala yote yanayohusiana na Muungano. Tumeshuhudia hapa Wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi wakilalamikia juu ya masuala mbali mbali yanayohusu Muungano wetu huu wa Tanganyika na Zanzibar. Sasa mimi nikuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mambo haya uyasimamie ipasavyo, hakuna haja ya kuoneana mihali.

Siku moja rafiki yangu hapa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora alisema mihali yetu hii inatusababishia mambo mengi yakwame. Kwa hivyo, nasema katika hili halihitaji muhali na kama tutaendelea kuwa na mihali katika kusimamia masuala haya basi hatimaye tutaharibikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kwamba wananchi wa Zanzibar kuwa hawataki Muungano siamini, Wananchi wa Zanzibar wote wanataka Muungano na kwa sababu umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, leo dunia nzima inazungumzia suala la kuungana na kuwa pamoja hata nchi za Ulaya wenzetu huko wanaunganisha mipango yao wanataka waungane ili wawe na nguvu, wengine wanathubutu kuunganisha sarafu zao ili sarafu yao iwe na nguvu. Lakini kinachowapelekea wananchi wa Zanzibar kukataa Muungano ni haya matatizo ya Muungano yaliyokuwa hayapati suluhu.

Kwa hivyo, ofisi yako Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ina dhima juu ya jambo hili, tume ile ya kuratibu masuala ya kero za Muungano ambayo wewe ni miongoni mwa wajumbe wake na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenyekiti wake ina dhima juu ya jambo lolote litakalotokea linalohusu suala la Muungano na utekelezaji wake. Kwa kweli kuna mambo ambayo yanaonesha dhahiri kwamba wenzetu hawajataka kuondosha matatizo yaliyopo.

Kwa mfano, tume ya pamoja ya fedha ambayo ripoti yake imewasilishwa katika serikali zote mbili tokea mwaka 2006 leo ni miaka mingapi Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshakaa na mapendekezo yake lakini wenzetu wa Jamhuri ya Muungano bado kuanzia mwaka 2006 hadi leo hawajakaa kuzungumzia mambo haya, hayo ni mambo ambayo yanaleta kero katika Muungano wetu. Mimi naamini wananchi wa Zanzibar wanautaka Muungano wao kwa sababu Muungano ni nguvu na utengano ni udhaifu ila matatizo yaliopo ndani ya Muungano ndio yanayosababisha wananchi wa Zanzibar kutaka kuukataa Muungano.

Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ofisi yako ifanye kila linalowezekana kuhakikisha matatizo yote ya Muungano ambayo tunayaita kero lakini ni matatizo basi inachukua hatua za haraka kwa kushauriana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhakikisha kwamba yanatatuliwa na hasa yale yanayohusiana na masuala ya uchumi. Hayo ni matatizo ambayo yanawapelekea wananchi wa Zanzibar kuona kwamba Muungano hauna faida kwao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako mimi niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi waikubali hotuba hii na itakapofika wakati tuipitishe, kwa sababu na sisi ofisi yetu imo humu basi bajeti hii ni yetu ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Tuipitishe kwa nguvu zote lakini huku tukimuachia ujumbe Mhe. Makamu wa Pili kwamba ashughulikie matatizo ya Muungano wetu ili tuone tunakwenda vizuri.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi sina zidi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili kwa kushughulikia kazi za uendeshaji wa Baraza hili na mimi nichukue fursa hii kama wenzangu kuchangia kwenye maeneo mbali mbali. Kwanza niende kwenye hali ya uchumi na mipango ya serikali ya kuimarisha uchumi.

Tumeambiwa kwamba uchumi wetu umekua kwa asilimia 6.8, kilichochangia kuongezeka kwa bei ya zao la karafuu, lakini nimuulize Mhe. Waziri kwa kweli pato hili ambalo limechangia la bei ya karafuu lakini hii miti yenyewe ya mikarafuu bado hatujaipa kipaumbele. Kwa sababu inaonesha kwamba ni miti mingi sasa ya mikarafuu imekuwa ni mikongwe na haina uwezo wa kuzalisha karafuu hizo ambazo tunazitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, lazima kila sehemu hata majumbani mwetu tuwe na bajeti na kama tuwe na bajeti basi ni lazima tuipange kwa matumizi yetu ya kila siku. Kwa hivyo na serikali ni jukumu lake kutuletea sisi Wawakilishi wa wananchi matumizi yao na mipango yao mbali mbali ili iweze kuendeshwa vizuri serikali yetu ambapo serikali yetu ndio tuliyoiridhia ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo ni lazima tukae na tutafakari baada ya kuletewa ripoti hizi za bajeti tukosoe lakini hatimaye tuweze kuwa kitu kimoja ili serikali yetu iweze kuendesha mipango yake mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikianza na kitabu hiki niende kwenye sehemu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza fursa ya ajira. Kwa kweli niseme wazi katika Baraza lako hili kwamba bado Mfuko huu wa AK na JK kwa maeneo mengi na hususan kwenye jimbo langu la Amani bado haujaweza kufanya kazi vizuri na sijui hasa kama kumewahi kupatikana mfuko huu. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba zile njia za kupata mfuko huu anielekeze ili na mimi niweze kupata kwa ajili ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa nambari 11 kuna Sekta za Huduma ya Jamii. Kwa kweli na mimi nichukue fursa hii nimshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wa kutaka mama wajawazito wasihusike katika kuchangia huduma hii. Hili ni jambo la msingi na sote tumefurahi kama ni wawakilishi pamoja na wananchi wetu ambao wako huko wanatusikiliza, kwa sababu hili ni jambo la msingi na ni suala la kulitilia maanani na ndio maana Mhe. Rais akalikubali na akalitolea maamuzi na niseme nampongeza sana.

Suala jengine ni suala la kuwapatia wananchi maji safi. Serikali inatilia mkazo sekta hii kwa kuijengea uwezo zaidi Mamlaka ya Maji, lakini bado tatizo la maji lipo na ufumbuzi mpaka leo haujapatikana. Mimi kinachonishangaza ni pale tunapoona miradi mbali mbali na hasa miradi ile inayofadhiliwa na wafadhili lakini baadae ikafa kwa kuwa serikali haikuweza kuiendeleza na ikawa endelevu. Ni aibu kwa mradi ule wa SEMUSO ambao umefadhiliwa na ndugu zetu wa Kimarekani lakini mpaka leo hii tunasikia pana matatizo ya hapa na pale ambayo mengine tutasema si *conducive*. Kwa sababu utaambiwa ni tatizo la umeme lakini mimi niseme kwamba bado serikali ina jukumu hili kwa sababu maji ni kitu muhimu, bila ya maji hakuna maisha.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwenda kwenye migogoro ya ardhi. Serikali imeshajua kwamba migogoro hiyo inasababishwa na viongozi na baadhi ya watendaji katika wizara husika kwa kutofuata taratibu na sheria za umiliki na uhaulishaji wa ardhi. Kwa hivyo, kwa kuwa serikali yenyewe imeshalijua hili tatizo niseme kwamba sasa ni lazima serikali iwajibike na ifuatilie suala hili kwa umakini sana, lazima taratibu zifuatwe na tatizo hili liondoke.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye suala la UKIMWI. Kwa kweli serikali imeliona kwamba ni tatizo na ni tatizo ambalo tunasema ni ajali kazini, kwa hivyo ni lazima kwenye suala hili wale wenzetu waliopata ajali hii basi tusiwanyanyapae kama serikali ilivyoona.

Vile vile kwenye suala la ulemavu. Serikali imesema wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ufikiaji wa huduma za kijamii. Ni kweli na kwa sababu kuna vipaumbele ambavyo bajeti yetu ya serikali ilisema ni kujenga majengo ya ghorofa kwa skuli. Kwa hivyo ni lazima itafakari juu ya majengo haya na lazima ziwekwe njia za walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mazingira duniani sasa hivi kutokana na kuongezeka kwa. *Carbon dioxide* imekuwa ni tatizo. Kwa hivyo ni lazima tuwaelimishe wananchi wetu ili waondokane na ile tabia ya kukatakata miti ovyo na kuharibu mazingira. Hilo serikali imeliona na niipongeze kwa juhudi zake mbali mbali za kututaka na sisi tushirikiane pamoja kama viongozi wa sehemu mbali mbali ili kutoa elimu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu kila pahala na kila taasisi ilikuwa ina mkakati wa kuelimisha wafanyakazi wake na pia nimeona katika jadweli, nilikuwa na hamu sana ya kuona lakini katika ukitizama kitabu hiki nimeona namna gani uwiyano umefanywa kati ya wanaume na wanawake. Wenzangu walisema hapa lakini kiko kiambatanisho cha jadweli ambacho kimeonesha si kiwango kikubwa ambacho tumepitana sisi wanawake na wanaume. Kwa hivyo, niipongeze sana serikali kwa kuona umuhimu wa mwanamke ndani ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Idara ya Utumishi na Uendeshaji inafanya kazi kubwa na ni moja hayo ya kuwaelimisha wafanyakazi wake wenye ujuzi mbalimbali.

La mwisho niseme niende kwenye suala la Muungano ambalo limekuwa ni kero kwa wananchi wengi lakini mimi binafsi niseme kwamba Muungano naupenda isipokuwa zile kero kama kawaida kero huzaa balaa na nasema hizi ni lazima ziondolewe kwa kupitia kwenye Katiba yetu ya Muungano. Mchango huu wa Katiba utapokuja basi kila mtu ana haki ya kuchangia na ni lazima waelimishwe wananchi kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma jirani yangu kwamba ni lazima katiba tuzielewe na kila tunapofanya mafunzo tunaambiwa tulale nazo iwe ndio wapenzi wetu. Kwa hivyo hili na mimi nalitilia mkazo kwamba lazima tuelewe katiba yetu.

Kwa hayo machache kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameshasema mengi nisiwe narudia humo kwa humo niseme kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tukiangalia muda tumebakiwa na dakika saba, lakini wachangiaji bado tuna watu 16. Sasa basi, tumuombe Mhe. Waziri awatambue wachangiaji waliobakia ili alielewe hilo na baadae jioni tuendelee kuwakaribisha tuanze na Mhe. Naibu Waziri wa Afya halafu aendelee Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na baadae aje Mwanasheria Mkuu akisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atupe majumuisho ya shughuli hii.

Mhe. Waziri naomba utambue mchango wa Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe Hassan Hamad Omar, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Farida Amour. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, Mhe.

Shawana Bukheti Hassan, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Bi Panya Ali Abdalla, Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ahsanteni sana.

Baada ya maelekezo haya sasa kwa heshima na taadhima naakhirisha Baraza hili mpaka jioni saa 11 kamili.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe asubuhi tulipoondoka hapa ilikuwa ni zamu ya Mhe. Dr. Sira ili aweze kuendelea lakini baada ya kwisha kukutana ndani na Mhe. Waziri Mhe. Mohamed Aboud kuona kwamba Wawakilishi hii ndio wizara yao, imebidi tuendelee na utaratibu wa kuchangia lakini tukiwa tunazingatia muda na majumuisho tutayafanya asubuhi.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima, na kuweza kufika wakati huu tukaweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitajaribu kuchukua muda wako hautokuwa mwingi sana kwa sababu bajeti hii imeshachangiwa sana, lakini na mimi niweze kutoa maoni yangu katika bajeti hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze ukurasa wa 4 katika kitabu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la hali ya kisiasa. Mimi ninadhani kama walivyosema wenzangu, na hali tunaiona kwamba hivi sasa ipo tulivu na hali basi tusiweze kuichokonoachokonoa na tukaibadilisha. Lakini ninamuomba Mhe. Waziri pia nitakuwa sikufanya haki kumuomba huu ni wajibu wake wa kila hali kutokana na cheo chake, kutokana na madaraka yake Mwenyezi Mungu aliyempa. Kwa hivyo ana wajibu wa kuyafanya hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya vuguvugu lote lilivyotokea tulimuomba katika vyombo vya habari akatoa tamko kwamba Makanisa yaliyoharibiwa serikali italipa. Basi na hili ni wajibu wake awe muadilifu kwa hili na pale pale popote utakapoharibiwa msikiti kwa vurugu lolote. Kama itatokea msikiti umeharibiwa atoe tamko katika vyombo vya habari kwamba msikiti huo utalipwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nije ukurasa wa 12 na 13. Mhe. Mwenyekiti, hapa wenzangu wengi wameshachangia migogoro ya ardhi, na kila aliyechangia amethibitisha kwamba kuna migogoro ya ardhi. Lakini katika kitabu chake hiki kuna sehemu ambayo nitainukuu inasema, “Serikali haitomvumilia mtu, viongozi na watendaji wanaojihusisha na kusababisha migogoro ya ardhi”.

Kwa hivyo mimi ningeliomba kwamba lazima serikali isimame katika matamko yake haya, kwa sababu maandishi haya ni sawa sawa na kula kiapo. Hivyo yasimame katika msimamo wa maandishi yake haya yaliyoandikwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna suala zima la maafa kwenye ukurasa wa 16. Mhe. Mwenyekiti, kwenye maelezo hapa serikali ilijaribu kulipa waathirika, na hesabu iliyotolewa kwamba kuna watu ambao wale ambao wale walioathirika kutokana na maafa hayo, wamepewa shilingi laki nne kumi na mbili elfu na mia tano.

Lakini mimi ninamuomba Mhe. Waziri kwa hisani yake aje atueleze kuwa fedha ni fedheha, na wakati wowote panapotokezea fedha kila mtu masikio yake yapo hapo.

Mgao huu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ulifanyika kwa mujibu wa taratibu gani, kwa sababu tangu jana iliposomwa hotuba hii na kila mmoja amefungua masikio yake, akajua kwamba kila mwananchi amehusika na kadhia hii amelipwa kiasi hiki. Lakini kuna wengine wamelipwa shilingi laki tatu na wengine wamelipwa shilingi laki mbili na nusu. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri mgao ulipofanywa ulizingatia kitu gani, kijinsia au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna fedha ambazo katika fedha hizi zilizotolewa na wahisani tunatarajia kuwa kuna fedha ambazo zimebakia. Jee, Mhe. Mwenyekiti, pia aje atueleze pesa hizi zilizobakia zinatarajiwa kufanywa nini.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 14. Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima ambalo lililozungumzwa juu ya suala la Ukimwi. Nalo hili suala hili nalo limetajwa katika kitabu hiki lakini pamoja na maneno mazuri ya Mhe. Waziri kwamba mkakati wa kwanza umemalizika. Lakini mimi ningemuomba Mhe. Waziri ni mafanikio yepi katika mkakati huu wa kwanza. Huu mkakati wa pili Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba pia atueleze kwamba umeboreshwa vipi.

Sawa sawa na suala jengine kuhusu suala la mapambano juu ya dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ameeleza kuwa kuna miongozo ya kuanzisha nyumba za makaazi kwa hawa tunaowaita wateja ambao wanaoacha madawa ya kulevya. Hili ni moja Mhe. Mwenyekiti, katika mafanikio haya na tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu.

Lakini sasa kuna tatizo zima ambalo mimi kamati yangu ilikuwa inapita katika *Sober House* hizi. Tatizo kubwa linaloonekana kwamba wanakuwepo pale na wanajikubalisha kuacha hizi dawa za kulevya, lakini jee ya kuondoka pale kuja mitaani, vipi wataweza kupatiwa hali ya kuwa wasirejee tena katika hali ile. Kwa sababu chanzo tunasema kuwa watoto wetu hawana kazi wanajitia katika dawa za kulevya. Kwa hivyo wanapokaa pale yupo kwenye utulivu kama kwenye kifungo.

Lakini yupo pale akasema anakuja zake mitaani, wakati hana shughuli yoyote ya kufanya bila shaka atarudi kule kule. Kwa hivyo jee, serikali ina mpango gani au mkakati gani wa kuwatizama hawa watoto wetu, vijana ambao waliokwishajikubalisha kuondoka katika hali hii na kuwaweka katika hali ya utulivu. Hivyo hili naomba nalo lipewe mazingatio katika suala hili. Kwa hivyo serikali iwe na mkakati wa kutizama, kiasi ya kwamba wajione basi wakitoka kule hawarudi tena kwenye shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niingie katika hili Baraza letu la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, tumshukuru Mwenyezi Mungu tumepata nyumba nzuri, anayepita nje yeyote anasema hii nyumba nzuri, na nyumba ambayo imekusanya Wawakilishi wa majimbo 50 wote wamo humu na wajumbe wa viti maalum wote wamo humu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, itafika wakati kule vyooni tuekewe vijiwe. Maana ya vijiwe vya kustanjia. Nyumba nzuri kama hii, leo imeshafika hadi unakwenda saa nyengine hakuna maji. Kwa hivyo ningeliomba suala hili la uzuri wa hii nyumba tusiitoe hadhi yake. Mji ukawa mzuri wowote basi ukakosa maji huwezi kuishi utahama tu. Ikiwa Baraza la zamani linatoka maji tutasema bora turudi kule, ikiwa yapo maji mengi na chungu nzima na hali ya usafi. Kwa hivyo hili nalo naomba tufikiriwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo limeshazungumzwa na wengi na mimi kama sikutia mdomo wangu japo kidogo basi itakuwa sikutenda haki. Mhe. Mwenyekiti, ni hili jinamizi la Muungano. Lakini kwa tathmini yangu fupi niliyoifanya tangu jana tupo katika michango hii. Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukapelekewa mchumba ukaambiwa mchumba huyu unamtaka, ukasema unamtaka lakini ni mchafu, lakini ana hili.

Mhe. Mwenyekiti, inaonekana wazi wazi kuwa humtaki. Kwa hivyo ninadhani kilichofanya kila mtu kutia kitu kuwa ana hili, bila shaka ni kwenda kujishauri huko. Mashauri yako yatakuja pale pale kuwa hutaki. Tatizo lililokuwepo kuwa hutaki kwa kero na migogoro iliyozidi, na ukitizama kero zenyewe Mhe. Mwenyekiti kuna masuali yaliyokuwa na majibu katika muungano.

Tunarudi pale pale, ina maana masuali hayana majibu hakuna uwezo wa kuyatatua, wala hayatatuliki. Ina maana kitu ikiwa hakitatuliki moja kwa moja imeshakuwa ni kasoro hiyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninadhani hili suala na Mhe. Hija Hassan Hija alisema hapa asubuhi, akamwambia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na mimi ninamuunga mkono, zisiharibiwe pesa bure kwa kutatua matatizo haya.

Mimi ninadhani kabla sijaingia katika Baraza la Wawakilishi, siku zote ukisikiliza Baraza la Wawakilishi utasikia kero za muungano. Mwanadamu ni mwepesi wa kukata tamaa. Kwa hivyo, ni kitu ambacho hakitatuki. Lililobaki sote tukae Wazanzibari tujipange tutafute maslahi ya nchi yetu tunataka nini.

Mhe. Mwenyekiti, ninadhani hili ndilo lililobakia. Hivi sasa baada ya kuona yote hayo tumshukuru Mwenyezi Mungu kutuletea huu mchakato wa Katiba, na hii ni kazi yake Mwenyezi Mungu hamuachi mja wake siku zote kwenye dhiki tu. Baada ya dhiki faraja. Tumepata dhiki muda mrefu tukasubiri. Kwa hivyo sasa ninawaomba Wazanzibari, nawaomba wanawake wenzangu twendeni tukatoe maoni yetu yaliyokuwa madhubuti.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoa mfano hai tuliokuwa nao hapa. Tulipokuwa tunatafuta serikali ya kitaifa. Nina imani kulikuwa na mvutano wa pande mbili mpaka tatu. Yule anataka hivi na vile. Jimbo langu la Koani kulipigwa kampeni watu wasikubali serikali ya umoja wa kitaifa. Lakini kwa rehema yake kesho kura kama leo, mwanamke mmoja tu alitoka akawaambia kwa nini hatuisikilizi kauli ya Rais, yule ndiye wa kusikilizwa. Kwa hivyo Jimbo la Koani tulifanikiwa.

Kwa hivyo na hili viongozi wetu wakuu watatu wakae pamoja, ili tunasema kwamba wao ndio viongozi, "*Alfaaru akbaru asli*". Kwa hivyo ninadhani kauli moja itakayotoka ya Wazanzibari tutapata nchi yetu yenye mamlaka kamili, yule anataka, mimi sitaki, sote tutakuwa kitu kimoja na sote tupo kitu kimoja.

Kama nilivyosema kwamba Mhe. Mwenyekiti, mfano wa mtu anayemtaka mchumba akasema kwamba lakini, hakuna anayeutaka muungano katika hali kama hiyo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninadhani umefika wakati wa kujipanga na Wazanzibari tukae kitu kimoja ili tuondokane na madhila haya ambayo tuliyokuwa nayo kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, nisichukue muda wako mkubwa kwa sababu kuna wengi ambao wanataka na wao kutia baraka zao katika bajeti hii, basi nasema niunge mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na kunipa fursa na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais; ambaye ni kiongozi wetu wa shughuli hapa tunapozungumzia.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ya kitabu hichi cha bajeti. Kwanza kabisa mimi ninataka nizungumze hali ya kisiasa ya nchi yetu ya Zanzibar.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kama ni hali ya kisiasa ya nchi yetu kwa sasa hivi ni nzuri ya kuridhisha, na sote ni mashahidi kama tunakotoka ni mbali, kwa hivyo mwanadamu aliyemkamilifu hasa anatakiwa ashukuru neema ya Mwenyezi Mungu ile anayoipata. Kwa kweli sisi tunakotoka na bora tusikumbushe kilio matangani ni mbali zaidi, na kulikuwa kubaya zaidi, na sasa hivi tulipo tunahitaji kushukuru kutokana na hali ya kisiasa ilivyo.

Lakini mimi kidogo nina masikitiko pamoja na utulivu wa hali ya kisiasa ilivyo, bado kuna wenzetu wachache wanahitaji kuturudisha nyuma kutokana na hali ya kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri anisaidie kitu kimoja kwa sababu ni mdogo wa kuzaliwa, yeye ni kaka yangu ni mkubwa wangu, kwa hivyo pengine yeye au mwengine yeyote aliyekuwemo humu Barazani basi naomba anisaidie tarehe ya kuungana kisiwa cha Unguja na Pemba.

Ikiwa kisiwa cha Unguja na Pemba kiliungana na kuwa ni nchi moja. Kwa nini niseme hivyo? Nasema hivyo kwa sababu nimezungumza kuwa kuna wenzetu wachache ambao wanataka kuturudisha nyuma kutokana na hali ya kisiasa ilivyo. Kwa sababu unapombagua mtu kisiasa, kirangi, kimila, kidini basi ni sawa sawa wewe ni mvunjaji wa amani katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa makusudi kuna kikundi katika nchi yetu kimejibagua kuwadhalilisha Wapemba au kumbagua Mpemba. Mhe. Mwenyekiti, hali ilivyo ya utulivu hivi sasa kuna watu kwa makusudi wanaandika vipeperushi wanavieneza katika nchi ya Zanzibar kuwadhalilisha Wapemba na kuwatukana.

Kwa kweli hawa ni wavunjifu wa amani na hawataki tuendelee kisiasa, yaani nchi iwe hivi ilivyo. Leo wanathubutu kumwambia Mpemba hahusu nchi hii ya Zanzibar, wamwambia mtu kama yeye anatoka Msumbiji, Wazanzibari yaani Waunguja ni Wandengereko kutoka hapo Bara. Leo wanasema Mpemba ni mtu kutoka Msumbiji, kwa hivyo

arudi kwao Msumbiji aende akakae. Lakini Mzanzibari ni Mndengereko kutoka hapo Bara, kwa hivyo huyu sisi tutaungana na wenzetu wa Bara, Mpemba arudi kwao ende Msumbiji.

Kwa hivyo huu ni uvunjifu wa amani, na kwa nini viongozi hamukemei hali kama hii na kama mnavyoiona inavyoanza, kwa sababu donda linaanza kwa chungu, chungu ndio inayosababisha kuwa donda. Siku zote unafanya kipele kidogo baadae linaanguka donda.

Kwa hivyo hawa watu tunawaona wanaichezea ile hali yetu ya utulivu, kwa sababu leo unamtukana Mpemba mpaka unamdhalilisha mwisho wa kumdhalilisha. Wallahi kuna vipeperushi vyengine kama ningekuja navyo humu huwezi kuvisoma anavyodhalilishwa Mpemba na kutukanwa, inatuuma, inatusononesha, inatuumiza sana. Ndio maana mimi nikauliza niambiwe tarehe waliyoungana watu wa Unguja na Pemba tukapata Zanzibar.

Kwa nini iwe hivyo na kudhalilishwa watu wa Pemba. Hii ni kuchafua amani ya nchi. Unapomtukana mtu mama yake, basi na mama yako wewe unataka atukanwe, lakini unapomuheshimu baba yako basi na wa wenzako waheshimiwe. Kwa hivyo hii ni hali ya kisiasa ilivyo Zanzibar. Naomba Mhe. Mwenyekiti, viongozi mukemee hii hali kuwa sio nzuri ni mbaya sana. Hilo ni moja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninataka nizungumze ni kuhusu suala la muungano na mimi. Pamoja na kuwa wengi wameshalizungumza lakini na mimi ninapenda nilizungumzie.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi juzi nilizungumza juu ya suala la muungano na leo ninazungumza tena suala hili. Kwa sababu suala linalozungumzwa na watu wengi ndio linalouma na linatuuma kwa nini? Wazanzibari ni wavumilivu, tumevumilia sana Wazanzibari lakini waswahili wanasema uvumilivu una mwisho wake, ukila na kipofu usimshike mkono, ukimshika mkono atajua kuwa unamtungua, na akijua hivyo yeye atapiga matonge au atakurusha mkono na yeye.

Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti, sisi Wazanzibari tumeungana na wenzetu Watanganyika tukapata muungano wa Tanzania. Lakini muungano huu ikiwa ni wa nchi mbili baina ya Zanzibar na Tanganyika. Lakini kweli hivi sisi hali hii iliopo kwa kweli ni sawa na kuwa tuna muungano au tunakokotwa Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, Tanzania ina mabalozi kama 56, lakini mabalozi wote hao Wazanzibari ni 3 peke yake; ni nchi mbili zilizoungana hizo. Kwa nini mabalozi wasitoke pande zote mbili za muungano na wakati ni nchi zilizoungana na watoke upande mmoja tu. Lakini wakati huo huo tuna taasisi ambazo ni za muungano, ukiacha na hizo zinazokokotwa badala ya 11 zinazofanywa 26. Hizo taasisi ni za muungano hebu nenda akaangalie viongozi wetu wanaotoka huku Zanzibar wamo katika taasisi hizo za muungano.

Sasa kwa kweli kama muungano wa nchi mbili, hivi sisi tumeungana nini. Tumeunganisha kitu gani. Huu si muungano ni muuwano na tunauliwa sisi Wazanzibari. Waheshimiwa viongozi wetu ni lazima tuwe wakweli na wawazi, tukiwa si hivyo basi hatutofika safari yoyote ile. Unapomuoa mke ndugu ukaogopa muhali wa wazee wenu ukasema ni huyu ni ndugu yangu basi hamuzai.

Sasa bahati mbaya Wazanzibari tumeoa ndugu, tena mke ndugu wenyewe ni tasa hazai, kwa sababu Muungano wetu ni tasa hauna faida yoyote, unazaa upande mmoja tu wa muungano, upande wetu hauzai. Jamani taasisi zote zile ambazo ni za uchumi wa Zanzibar zimeshikwa na Muungano. Sasa sisi Zanzibar tuiendeshe vipi kwa sababu zile taasisi za kuleta fedha ni za muungano, wenzetu wamezikalia kitako, ukitazama Wazanzibari hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, kucha kucha tunachonga utumwa eeh! kila nikikaa hapa ninasema viongozi wetu tatizo letu munawaonea haya wenzetu, wao wanatuumiza. Jamani nawaomba viongozi wetu sasa imefika wakati wa kusema ukweli. Kwa nini sisi tunatetea haki zetu. Kama tumeungana haki zetu za muungano wetu tupewe, lakini sisi tumeungana wenzetu wanakula faida ya muungano na sisi tunapata hasara ya muungano.

Mimi ninasema hatuna kero za muungano, tuna migogoro ya muungano au mizozo ya muungano, kwa sababu kero ni zile zinazotatuliwa zikamaliza. Hili tunaliita kero la muungano, halijatatuliwa, kesho kuna jengine ni kero la muungano, halijapata ufumbuzi, kesho yake linakuja.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 5 za ziada.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ninataka nilizungumze ni suala la mipango ya uchumi wetu. Waheshimiwa tukisema hivyo bado viongozi hamjataka kutuletea ile mipango ya uchumi wa nchi, kwa sababu kuna nyenzo za kuongeza uchumi wa nchi. Lakini bado hamujazikalia kikao kwa kweli mukazifanyia kazi hizi nyenzo za uchumi wa nchi yetu.

Kwa mfano bahari kuu, kila tukija kwenye vitabu tunazungumza tu kama kuna uvuvi wa bahari kuu utasaidia uchumi wa nchi yetu. Lakini kwa nini hamjaandaa mipango kabambe ya kufanya kazi katika bahari kuu, wavuvi wetu wakavua uvuvi wa kileo, na kila siku munazungumza kwamba bahari yetu bado haijafanyiwa kazi. Wananchi wetu ni wavuvi Unguja na Pemba ambao wanahitaji wapewe zana za kileo. Serikali iandae mpango kabambe wa kuwapa elimu wananchi ili kuvua bahari kuu, lakini si elimu tu na vitendea kazi, kwa sababu hii ni moja ambayo itainua uchumi wa nchi yetu.

Lakini tunakuja tukitaja tu kwenye vitabu. Wazanzibari mimi ninavyoamini ni wabunifu wa kusoma mambo kwenye vitabu, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mgumu. Tunaanza mambo na tunapitwa na watu wanaokuja nyuma. Hebu viongozi wetu sasa imefika wakati hii bahari tuitumieni, nayo iongeze uchumi wa nchi yetu. Tusiseme tu kwenye vitabu, kaeni muchekeche mupange, lakini almuradi mutupe nyenzo za kufanyia kazi katika bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako ili niwaachie wenzangu na wao watie nyama kidogo. Ahsante sana naunga mkono.

Mhe. Shawana Bukheit Hassan: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi kwa jioni ya leo na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sikutegemea.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza mchango wangu niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 5. Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii inahusiana na suala la Muungano. Kwanza nataka kusema kwamba nampongeza sana baba yetu Marehemu Abeid Aman Karume na pia nampongeza baba yetu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kutuunganisha katika nchi zetu hizi mbili na tukaweza kufanya Muungano. Wao walichukua sehemu hii ya kutuunganisha, lakini hata hivyo tulikuwa tuna Muungano tokea asili ya jadi, Muungano wa damu, wao wametuongezea nguvu, tunawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awarehemu, awape malazi mema.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme ya kwamba wakati wa chaguzi siasa inakuwa kwenye majukwaa, kila mmoja anataka chama chake kishinde, tunapomaliza chaguzi pamoja na serikali yetu ya umoja wa kitaifa, lakini siasa inakwenda kwenye Baraza la Mapinduzi, Baraza la Wawakilishis na inakwenda Bungeni.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala haya ya Muungano ukiangalia utaona kuna upotoaji wa makusudi, kuna upotoaji wa wananchi makusudi ili watoke imani, watoke busara wawe hawana busara na Muungano. Mhe. Mwenyekiti, suala la Muungano sote tunasema kwa asilimia kubwa tunalitaka, lakini kunaonekana dhahiri kuna kazi ya siasa inafanywa ili uonekane Muungano usitakiwe. Lakini Muungano utadumu *Inshaaallah*. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kero za Muungano isiwe ndio sababu ya kuvunja Muungano. Kero zipo na kero zimetatuliwa. Kwa taarifa niliyokuwanayo mimi, kero zilikuwa 13, lakini mpaka sasa hivi kero saba zimeshatatuliwa. Nitazitaja moja baada ya moja, baadae waziri atathibitisha kama ni sahihi au si sahihi atatupa maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Muungano au kero za Muungano zinazohusu Zanzibar, hakuna mtu ambaye anaishi hapa Zanzibar ambapo kuna kero anayohisi hii ama itatupunguzia mapato ama itatupunguzia hadhi yetu katika nchi yetu, ikawa haimkeri na hii kero isihesabiwe kuwa kuna watu fulani maalum ndio inayowakera. Kama kuna mapungufu ndani ya Muungano, Zanzibar tunayazungumza, kama kuna mapungufu ndani ya Muungano Bara wanayazungumza, kama kuna mapungufu ndani ya Muungano Chama Tawala kinayazungumza na kama kuna mapungufu ndani ya Muungano vyama vya upinzani vinayazungumza. Kwa hivyo, lisichukuliwe hili jambo lionekane labda ni ajenda ya watu fulani na watu fulani wako maalum ndio wenye uchungu wa nchi hii, hapana.

Mhe. Mwenyekiti, mwenye uchungu wa nchi hii mmoja wapo ni Mhe. Rais wa mwanzo aliyeikomboa nchi hii na hadi kufikia ukazaliwa huu Muungano. Sasa tusifikie mahali tukaonana wengine hapa labda hawataki Zanzibar ikomboke. Hakuna asiyetaka Zanzibar isikomboke Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja anataka hapa nchi hii iweze kuwa

na mambo yake yale ambayo anahisi tuyapate na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, yakaletwa marekebisho ya katiba baada ya malalamiko mengi. Mhe. Rais Jakaya Mrisho hili kalizungumza na wakati mwengine hata TBC yanatolewa mazungumzo yake, ukisikiliza huku na hili na huku kuna hili.

Kwa hivyo, bora tuamuwe tuunde katiba mpya ambayo kila mmoja itamridhisha. Haya yote tuliyoyazungumza hapa Mhe. Mwenyekiti, yanastahiki twende tukayazungumze kwenye hayo marekebisho ya katiba, tukaseme. Sisi tunataka tukenda nchi za nje tupeperushe bendera yetu, tunataka nchi za nje twende tukakalie kiti chetu na pia utaandaliwa utaratibu, lakini sio la kuvunjwa Muungano Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya michango nimeisikia wanasema hoo! Muungano haukuwa halali huu, hata Baraza la Mapinduzi haukupita. Mhe. Mwenyekiti, nimekuja na *document* hizi kutoka Bungeni, makusudi nimekwenda kuchukua Hansard. Hii hapa *document* inayotoka Hansard Bungeni inayohusu Muungano. Mhe. Mwenyekiti, hii ina kila kitu imejieleza humu ndani na hao walioshiriki kwenye maandalizi ya Muungano huo, wanasema kuwa ni wa Rais Abeid Karume na Rais Nyerere peke yao, sio kweli.

Mhe. Mwenyekiti, orodha hapa ninayo ya wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wananishawishi nitaje. Sijui utaniongezea muda, maana yake yatachukua muda. Kwenye Muungano huo ukiwacha wenzetu wa Muungano wa Bara, huu orodha ninao hapa, lakini ni kubwa mno, lakini hapa Wazanzibari wamo. Kwa wakati huo *member* wa Baraza la Mapinduzi, kulikuwa hakujaanzishwa Baraza la Wawakilishi kama hivi sasa wanatolewa watano kwenda, walikuwa wote wanakwenda na ndio hawa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, wa kwanza wakati huo alikuwepo mwenyewe Marehemu Mhe. Abeid Aman Karume, Mhe. Abdalla Kassim Hanga, Mhe. Abdulrahman Babu, Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Mhe. Hassan Nassor Moyo, Mhe. Idrissa Abdul Wakil Nombe, Mhe. Ibrahim Saadala Akida, Mhe. Thabit Kombo, Mhe. Ayoub Machano, Mhe. Ali Sharif Mussa, Mhe. Muhidin Ali Omar, Mhe. Said Pongwe Said, Mhe. Chum Vuai na Mhe. Khamis Machano.
Hati ya Muungano huu na kikao hiki kilifanyika pamoja na wenzetu Wabunge wa Tanzania Bara wakati huo. Kuna jambo hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, lakini hii naona itatoka. Kwa nini nimetaka kuwataja hawa, nimewataja kwa sababu inaambiwa kuwa Baraza la Mapinduzi halikuhusishwa. Hivi hawa niliowataja hapa sio Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, wengine hata kuzaliwa walikuwa hawajazaliwa. Baraza la Mapinduzi gani lililotakiwa liwe limehusishwa katika suala hili.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tuseme kweli. Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumza siku moja hapa, akasema kwamba mimi nadhani jamani hili jambo sio kero za Muungano tu, na huu UAMSHO sio kweli labda wao kuna kitu wanadai tu hivi hivi, kuna jambo limejificha mimi naamini hivyo. Mhe. Mwenyekiti, nitanukuu maelezo ya ndugu yangu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, alisema siku moja kwamba mwanadamu akisema lakini kuna mambo mengine anayabakisha moyoni mwake. Kwa hivyo, tunapokutana hivi aaah! Mengi tunasema, lakini kuna mengine yamefichwa sio kero tu ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema kwamba Zanzibar tunasema hatujafaidika chochote na Muungano. Jamani, ‘mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni’. Hivi ni kweli tunavyosema kuwa hatujafaidika chochote hapa sisi. Tujitizame Mhe. Mwenyekiti, ni Wazanzibari wangapi tunaoishi Tanzania Bara tumejaa kila mikoa kama ya kwetu kule na kwetu utadhani ni Tanzania Bara, tumejaa kama hapa Zanzibar, ukifanya idadi pengine kama hujatukuta mara sabiini kule. Nani ameekeza zaidi, Watanzania Bara wamewekeza zaidi hapa au sisi tumeekeza zaidi kule.

Mhe. Mwenyekiti, nilipita Kariakoo, sio siri nilikwenda kununua dawa zangu mimi mwenyewe na za mama yangu. Kuna *pharmacy* moja kule imeandikwa *Heko pharmacy*, niliwakuta ndugu zetu wa Kizanzibari wanavyonung’unika vurugu tunalolifanya la kutaka kuvunja Muungano, hali ya kuwa wao wenyewe wameshajiimarisha na walivyo na wanavyoendelea na hivi sasa wanavyoisikia hii bughudha. Kwa hivyo, kupanga ni kuchagua, lakini mimi nadhani hili suala la kero kama nilivyosema sio sisi tu. Hawa viongozi wetu wote wa juu hatuwaamini, wala hawana imani na nchi hii, wala hatuwaamini kazi tuliyowapa. Wanaambiwa Wabunge waseme Bungeni. Wabunge wakisema Bungeni ndio wanamwambia nani, si mawaziri na hapa sisi tukisema tunawaambia nani si mawaziri. Basi na twendeni sote huko Bungeni tukaseme. Ikija hiyo tume ya kusikiliza kero za Muungano twendeni sote. Sasa hawa viongozi tunaowachagua, ina maana hatuwaamini.

Mhe. Mwenyekiti, kero zimeanza kushughulikiwa na Dk. Ali Mohamed Shein akiwa Makamu wa Rais. Kajitahidi kadiri ya uwezo aliokuwa nao na baadhi ya kero zimetatuka. Hapa zilikuwa zikisimamiwa na Ofisi ya Waziri

Kiongozi, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na kule kwa kipindi kile nadhani sijui kama aliwahi yule waziri, lakini Mhe. Pinda na yeye alikuwemo katika hilo suala na sasa hivi linasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, wote hawa hawana uchungu, sisi tuna uchungu peke yetu tu na wao ndio wanataka libomoke. Jamani hamumswalii Mtume. *(Makofi/Vicheko)*

Baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe: *(Allahumaswali Wasalimualey)*

Mhe. Shawana Bukhet Hassan: Mhe. Mwenyekiti, tunasema hatujafaidika, mbali ya hilo nilolisema kuwa tuko kule na tumeshawekeza, tena hatukuwekeza, tumewekeza na tumejipwetekeza. Wengine hata hatupiti huku. Kuna baadhi ya Wabunge wanaishi huko Morogoro na wapi huko, wanakuja kama *transit* tu katika huko walikochaguliwa tunawajua na tunao, anakuja kidogo tu kisha huyoo anarudi kwenye miradi yake. Sisi huku oooh! Muungano hatuutaki, watu wanachanua huko wanajichana Karatu yeye keshajiwekeza. Sasa hivi wanaandikisha Utanzania huko. Mhe. Mwenyekiti, 'hala hala mti na jicho'.

Mhe. Mwenyekiti, hatujafaidika lakini magari hapa tumejaza, yale maeneo ya kuweka na kuuza magari yale yanayoitwa *showroom* tumejaza hapa kila pembe.

Mhe. Mwenyekiti: Unadakika tano za ziada Mhe. Mjumbe.

Mhe. Shawana Bukhet Hassan: Haya. Nimeombewa Mhe. Mwenyekiti, dakika ngapi unanipa, haya. Mhe. Mwenyekiti, magari mpaka chini kuna *showroom*. Lakini nenda sasa ukayaangalie bandari pale sasa uyaone yanavyoondoka, yanakwenda wapi. Utaviona vile vibaskeli, TV, redio, vifriji vile kafa Ulaya maziko Tanzania. Tumevichukua kule tumevileta hapa, tukisha hapa tunavipeleka huko huko, viko kule vile tunaviita visehewa vimejaa kule, lakini vinatoka wapi na wanafaidika kina nani Wazanzibari hatujafaidika, umeme unatoka Tanga uko Pemba sasa hivi wa uhakika. Huo huo umeme wa hapa tunaulaani sijui hayo mapungufu yaliopo, lakini tunao au hatuna. Yawashwe leo yale majenereta tuliyokuwanayo kule Mtoni tuone tutafika nayo siku ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kila siku, kesho tutatengeneza umeme wa upepo, kesho tutatengeneza umeme wa pumzi. Mhe. Mwenyekiti, hakuna suala baya linaloharibu nchi au wananchi wa dunia kwa jumla kama ubaguzi wa kidini, ubaguzi wa kirangi, ubaguzi wa kikabila. Sasa haya yote hapa kwetu tunayo. Ndio maana Marehemu Mzee Karume alisema hapa Mwenyezi Mungu amrehemu, kwamba hapa kama hatujafika miaka 50 usifanyike uchaguzi. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo palipoanzia chanzo hiki. Ndugu yangu kalalamika hapa kasema na ni haki yake aseme, kwa sababu sio utaratibu mzuri. Lakini nani aliyesema machogo yaondoke hapa, si waliambiwa, sasa machogo ni nani. Mimi sikuwepo nilikuwepo Dar es Salaama, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hapa Mwenyezi Mungu anijaalie tu nimalize salama. Nilikuwepo Dar es Salaama kwa sababu hali yangu ilikuwa mushkeli kidogo, tatizo presha. Kwa hivyo, kule kule nilisikia mimi kuwa Wabara masaa 24 waondoke. Sasa hili jambo baya na hili Mwalimu Nyerere alilikemea na alisema dhambi hii ya kubaguana haitoishia hapa na mimi nasema leo tunadai Uzanzibari, kesho tutadai Upemba na Uunguja na huko ndiko tunakoendea na kesho Ukusini na Ukaskazini, kesho Umjini na Ushamba. Tunakuja kuambiwa sisi washamba tukifika mjini tunaambiwa hapohapo simama na ndiko tutakakofikia huko.

Mhe. Mwenyekiti, wanaambiwa Wabunge waseme, lakini nataka niulize yule aliyesema akauliza swali kule Bungeni kuwa Zanzibar nchi au si nchi, akajibiwa aliyojibiwa na hapo ndipo yalipoanza kuchachuka. Alikuwa ni nani yule, ni Mwakilishi Mbunge wa Jimbo la Chwaka Mhe. Yahya, aliuliza au hakuuliza. Si hawasemi na hatusemi. Sasa nasema hivi Mhe. Mwenyekiti, haya mambo madogo madogo, kwa sababu ilipokuja ile ikakaa kidogo hivi ndio likaja suala la mafuta wakasema ndio hapo hapo, Zanzibar yetu, Wazanzibari Watanganyika, Wazanzibari Watanganyika. Ikaja mafuta yetu wenyewe, yakawa sasa yanakuja juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niko hapa mwaka wa 17 huu, kwa hivyo nalijua Baraza a to z. Najua leo hapa panaundwa nini, hapa tunakwenda vipi na hapa tumekusudia kitu gani. Najua vizuri, huwa sitaki tu wakati mwengine. Lakini ikibidi mtu uyatowe ya moyoni ambayo hata kama uliyaficha basi ni lazima uyatowe yote. *(Makofi).*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hapo ndipo yalipoanza, yalianza yale na watu walikuwa na sababu zao ndio wakasema ni hapa hapa. Wanasemaje kule Zanzibar si nchi, eeh ikawa hapa tena na hapo hivi na hivi. Sasa imefikia hatua yale yote sasa hivi tukae tuyazungumze. Sasa tunasema tumechoka kuwatuma hawa viongozi wetu

wanakwenda kukaa kule Bwawani, labda wanakwenda kunywa juice tu hawana wanachokiongea wala hawana wanachofanya. Mimi nawaamini kweli kweli na ndio maana nikawapa kura. Sasa zamu yetu, katiba hiyo inakuja twendeni. Haya yote tuliyoyasema hapa tukayasemeni. Mimi nataka serikali 15, sababu zangu moja, mbili, tatu, nne na tano. Mimi nataka serikali mbili sababu zangu hizi na hizi. Mimi nataka serikali tatu sababu zangu hizi na hizi na wengine nasikia wanasema wanataka serikali nne huko.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kidogo baada ya tulikotoka Zanzibar si nchi

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zingatia muda.

Mhe. Shawana Bukhet Hassan: Haya ndio namalizia Mhe. Mwenyekiti. Maana yake haya mambo nilifanya kazi kweli hata nikayapata. Suala la mafuta hili hapa, kuna siku liliambiwa limeingia kinyemela. Lakini halikuingia kinyemela, hili lilipitishwa Bungeni tarehe 18 mwaka 1968. kikao hicho kilianzia tarehe 18 na kikaishia tarehe 22 mwaka 1968 na wajumbe wake hao waliotoka Zanzibar ni 37. Mhe. Mwenyekiti, umeniambia muda hamna, lakini wapo. Wajumbe wakitaka Hansard nitawapa. Jumla walikuwa kama 118 kutoka Bara na hawa 37.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tusiseme tu mambo, kinyemela kinyemela, kinyemela gani na Hansard yake hii hapa yote iliyozungumzwa kwa muda wote huo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti. Mimi nakubali tuna serikali ya kitaifa, lakini itikadi zetu sio moja na sera zetu sio moja, kila mmoja ana sera zake tusifichane. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba pamoja na maamuzi tunayoyaamua tuyaamuwe kwa Wazanzibari, lakini pia tuzingatie yale mambo yenye ukweli. Tusiwe tunavutana na kubururana kwa kusema Uzanzibari Uzanzibari. Uzanzibari sote tunanufaika kwa namna moja au nyengine. Hayo niliyoyataja ni machache tu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na mengine mengi yanayohusu ndani ya bajeti. Lakini kwa hili nasema mimi sitochangia kwenye suala la bajeti iliyopita, nikasema kuna eneo lake na eneo lake ni hili na mimi nilikuwa natafuta vitu vya uhakika ili nikija kuzungumza nijuwe nazungumza nini, kwa hivyo nikasema eneo lake ni hili na mimi nimedai leo kwa nguvu zote Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa busara zako, umenipatia nafasi angalau nitalala na usingizi utakuja. *(Makofi).*

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna tetesi naomba Mhe. Waziri na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hebu mtusaidie, mambo haya ya kudharau kauli za viongozi wetu mwisho yanatudhuru. Kuna tetesi kuwa sasa hivi kunataka kujengwa *base* ya Marekani Tunguu, pale pale ambapo Marehemu Mzee Karume aliwaondosha, tupeni ufafanuzi hili limekuwaje. Mhe. Mwenyekiti, niliambiwa nizitaje, hapa wajumbe wananiambia mbona hakutaja zile kero zilizotatulika, lakini muda sina. Mhe. Mwenyekiti, nitampelekea Mhe. Waziri ili kama kweli ni sahihi yeye atajibu, lakini nitampelekea na mchango wangu wa maandishi.

Nakushukuru ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake hii yenye mwelekeo mzuri, na kwa uhakika naamini tutafanikiwa kama vile alivyotueleza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuanza na suala la mgogoro wa ardhi. Kwa kweli suala hili la ardhi limekuwa kubwa, tumeanza kupiga kelele tokea eneo la Selem, kule lipo tatizo la ardhi. Lakini hatua za kisheria zilizochukuliwa sijasikia zimefikia hatua gani.

Vile vile eneo jengine kuhusiana na tatizo hili la ardhi ni Bambi. Mhe Mwenyekiti, tatizo hili niliwahi kuona kwenye *television* kwamba wananchi 1,000 wanalima kwenye lile eneo. Lakini pale serikali imetaka kumuweka Mwekezaji na wala sio vibaya, lakini wale wananchi wana malalamiko yao. Kwa hivyo, kama serikali ilikuwa ikae nao kwa ajili ya kuwafahamisha na kuweza kufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikia tena kwamba bado wanalalamika kuhusu suala hili, na wanaiomba serikali iwasaidie. Kwa kweli sisi Wawakilishi au mimi Mwakilishi nikisikia haya masuala ya migogoro ya ardhi, inaniuma sana. Kwa

maana hiyo, ni vyema kuwasaidia wananchi hawa na tuone kwamba tunawatatulia matatizo yao haya, kwa sababu wao wenyewe ndio wanategemea kwa ajili ya maisha yao ya kila siku.

Leo asubuhi nimesikia tena kwenye Mawio, katika eneo la Kijitoupele na wenyewe wanalima, lakini pale wametaka kuwekwa wafanyabiashara kwa ajili ya kuuza miti, na hili pia ni tatizo jengine ambalo linaongezeka, yaani yale kule bado hatujayamaliza mengine yanaongezeka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba masuala haya ya ardhi baada ya kuwaachia watendaji chini naomba sasa Ofisi ingie wenyewe kwa ajili ya kufanya kazi hii, kwa sababu itatuharibia na wananchi wetu wamechoka kuhusiana na masuala ya ardhi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, kwenye muungano kwanza naunga mkono kuwepo kwa muungano, japo kuwa kuna kero, lakini naamini viongozi wetu kwa hatua waliofikia kero hizi zitakwisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tumetoka mbali na tumeanza mbali na mpaka tumefikia hapa leo kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na hii imesimamiwa na viongozi, hivi sasa tuko pamoja tunashirikiana na hizi kero za muungano kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu zitatatuliwa, kwa sababu viongozi wetu tunawaamini na hizi kero zitakwisha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kero hizi za muungano zisitufanye tukaondosha udugu wetu, kwa sababu udugu tayari tunao. Kwa maana hiyo, masuala haya tukae kwa pamoja na tuone hizi kero tunazitatua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyoona ni kwamba tuwaachie viongozi wetu kama walivyoahidi japo kuwa tumeshasema kwa sana, kwa sababu yalianza kusemwa kidogo kidogo, lakini hivi sasa naamini kama serikali imeshasikia, basi naamini haya yote yatatatuliwa. Kwa hiyo, ndio maana tukaanza na hili suala la Katiba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wananchi wajitokeze kwa wingi kutoa maoni yao kwenyeTume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba. *(Makofi)*

Kutokana na kwamba watu wengi wameshachangia sana na mimi niokoe muda, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, kwa ajili ya kutoa maoni yetu katika nchi yetu.

Vile vile nikushukuru wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii. Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake nzuri, iliyojaa hekima na busara, na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mambo yetu yatakwenda sawia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na suala la maafa itakumbukwa siku ya tarehe 10/09/2011 Zanzibar yetu ilikutwa na jinamizi kubwa sana kwa kuondokewa na wapenzi wetu, wananchi wetu katika tukio la Meli ya *Mv. Spice Islander* na hii ni historia kwetu, kwa kweli hii ni historia kubwa na ninaiomba serikali iweke kumbukumbu ya kukumbukwa kila mwaka, na kuwatakia dua waliotangulia mbele ya haki. *(Makofi)*

Lakini kwa masikitiko makubwa sana, tulipenda tujifunze na yaliyotokea na tatizo tunalijua ni nini. Kwa hivyo, Zanzibar tuiambie serikali kwamba kuna haja ya kupata chombo cha uhakika cha kusafiri Unguja na Pemba. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, aangalie *Hansard* zetu tulizozizungumza kabla ya tukio, na hivi sasa tunatoa tena wito huo, kwa jicho la huruma na imani kubwa basi tuwe na meli ya serikali, ambayo ni nzuri kwa ajili ya kusafiri Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, siku hiyo sisi tulikuwa Arusha katika michezo baada ya kumaliza bajeti kama hii, lakini mimi ni mtu wa mwanzo kupata taarifa katika hoteli tuliyokuwa tumelala kama meli inazama tena tulipigiwa simu na mtu ambaye yupo juu ya mgongo wa meli kwamba inazama sasa.

Kwa kweli ilikuwa ni majonzi makubwa sana, na mimi nilithubutu kuwagongea wenzangu akina Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Omar Ali Shehe, hapo hakuna hata mmoja aliyelala tena na kuweza kumtaka Katibu wetu wa Baraza kutupangia safari ya kurudi Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wawakilishi tuliokuja kwa ndege kuja kuona maafa yaliyotokea na tuliwahi vyema. Kwa hivyo, naiomba serikali kwamba hili jambo tusijelisahau mapema, kwani jambo kubwa ni kupatiwa wananchi usafiri wa uhakika, kwa sababu hii ni njia ambayo masaa 24 inapita watu, iwe usiku au mchana na tukio lilitokea usiku.

Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru sana katika kitabu hiki kimeeleza kuanzisha Vituo vya Uokozi. Katika kuanzisha Vituo vya Uokozi ni jambo jema, lakini kama alivyozungumza mwenzangu asubuhi hapa ni bora kinga kuliko tiba. Kwa hivyo, ni jambo jema kuanzisha Vituo vya Uokozi, lakini mimi nathubutu kusema kwamba Serikali izitambue jumuia.

Kwa kweli siku ile kulikuwa na Wakojani wenye *experience* na jambo lile, basi walisaidia vya kutosha na wala si vibaya hata kumtaja kwa jina anaitwa Bakari Makame (Nitakitoa), yaani huyo alitusaidia mpaka alipoteza fahamu na kupelekwa Hospitali pale. Kwa maana hiyo, yanapotokezea mambo kama haya ya kuanzisha hivi vituo, basi jumuia ipo na yenye *divers* wazuri sana. *(Makofi)*

Kwa mfano, tukio la kuzama kwa Meli ya Mv. Fatih walisaidia, pamoja na matukio mengine ya kuzama kwa meli Zanzibar wamesaidia sana, hivyo muwaangalie na wala hawatambulikani kiutaratibu wa kisheria, na wao muwachukue muwaingize huko, kwani wana uzoefu wa kutosha. Hilo ni moja.

Vile vile ndani ya kitabu hiki limetajwa suala la Uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sasa *Alhamdulillah* tunaelekea kuzuri. Lakini Uvuvi wa Bahari Kuu kutokana na Zanzibar ni Kisiwa na kuna wavuvi wengi.
Kwa kweli nathubutu kusema kama zitakuja meli mbili au tatu, bado hajijakidhi haja hata kidogo. Kwa nini niseme hivyo? Nasema kwa kujiamini kabisa kwamba meli hizi mabaharia wake wa kivuvi ni watu 30, na wengine 25 na hata 20 ndio zinabeba wavuvi, kwa hiyo kuja na meli mbili tatu bado Wazanzibari hawajafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na kumpongeza tena Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuweza kutaja Zanzibar kama tunao wavuvi wadodo wadogo, kwa mara ya kwanza nasema kwamba nimefarajika vya kutosha kuwataja wavuvi wadogo wadogo kuwatambua hasa, na imezungumzwa kwamba watawaendeleza, ni imani yangu kwamba kama jambo hili litakuwa la kweli kabisa. *(Makofi)*

Kwa mfano, katika Sekta Binafsi uvuvi umeajiri watu wengi sana, Mhe. Mwenyekiti naomba muende Malindi asubuhi na kuangalia pale, ukiachana na uvuvi waangalie wahusika wanaokuja pale wananchi walaji pamoja na wachuuzi wanaokuja pale, utajua kama kweli hii Sekta Binafsi imeajiri watu wengi. *(Makofi)*

Hivi sasa wafanyabiashara ya samaki wabichi ni wanawake. Kwa mfano, ukienda Darajabovu, Darajani, Mikunguni utamkuta mwanamama ndiye mwenye kupanga samaki. Hali hii inaonesha kwamba watu wamejiajiri na hivyo inafaa kuwaendeleza na kuwaenzi kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tusiwabane wavuvi, isipokuwa tuwape uhuru wa kutosha, kwani hiyo ndiyo ajira yao. Kwa kweli ukiangalia sana Uvuvi na Ukulima ndizo sekta zinazoajiri watu wengi na wala hakuna sehemu nyengine. *(Makofi)*

Katika suala la Uvuvi wa Bahari Kuu kuna na ufugaji wa samaki pia, na ilitajwa katika bajeti iliyopita, lakini mpaka sasa hatujaona maendeleo yoyote ya ufugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti, shahidi wangu ni Mhe. Said Ali Mbarouk aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tulitembelea wafugaji na wavuvi wa samaki tarehe 19/02 ndani ya jimbo langu pamoja na majimbo mengine. Lakini bado hatujawa na ule ufugaji wa kupata tija hasa, kwa sababu siku zote sisi tunaanza na wala hatumalizi, tunaweza kuwa na *pressure* kubwa sana ya kuanza, lakini hatumalizi na jambo lolote unalolianza kama hukumaliza, basi ni sawa na *zero*. *(Makofi)*

Naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ijipange vizuri kwa lengo la kuwaendeleza hawa na tutaona faida yake baadae.
Mhe. Mwenyekiti, sitaki nikucheleweshe sana kwa muda wako, kwa sababu wachangiaji ni wengi na ulikuwa tayari umeshataja majina hapa kwamba hatutapata kuchangia, lakini kwa bahati nzuri umetuonea huruma, basi na mimi niko na wenzangu, ili na wao wapate kuchangia. *(Makofi)*

Suala la mwisho ni kuhusu shughuli nzito tuliyonayo ni Muungano. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna watu ambao wanaoweza kuvunja muungano ni Watanzania Bara. Kwa nini niseme hivyo? Kwa kuwa kero zisizoweza kutatuka ni matatizo. Kwa kweli yamezungumzwa kwa muda mrefu, na hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa imekuja juzi na imezungumzwa na kumaliza, lakini kero za muungano zipo muda mrefu na mpaka leo bado hazijatatuka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari nathubutu kusema ni watulivu, tukumbuke tulikotoka tulikuwa hatuzikani kabisa, na *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu ametuletea neema hii ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa sote tunatambuana, tunazikana vizuri sana na kila mazishi tunashiriki sote hakuna CCM, CUF wala chama chengine, na sote tunashiriki vizuri katika Zanzibar hii na haya yalikuwa ni tete kwetu.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho naomba anieleze kidogo tu, kwamba ni kero ngapi za Watanzania Bara tunazowakera sisi Wazanzibari, halafu aniambie ni kero ngapi Wazanzibari tunazowakera Watanzania Bara. Hapa ndipo tutajua nani mwenye kutaka kuvunja muungano. Mhe. Mwenyekiti, namuomba kwa heshima kubwa sana Mhe. Waziri atakapokuja anieleze. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo, na mtu mzima halii tu, isipokuwa kuna jambo limemkera ndani ya moyo wake na lazima atoe machozi kwa ajili ya kupunguza machungu. Kwa kweli hawa tunaowaita Uamsho ni jina tu, lakini hawa ndio Wazanzibari na kauli mbiu tumeshaisikia na mimi kama Mwakilishi wa wananchi basi nasema kwamba Muungano tulionao sasa hautufai kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba, tayari imeshakuja na Mwenyekiti alihutubia. Lakini nawaomba Wazanzibari wote tuwe pamoja kama tulivyokuwa pamoja katika kutoa maoni yetu kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa na tumepata kitu kizuri, basi na hapa tuwe ni kitu kimoja na wala tusiwe na nia ya kubaguana hata kidogo. Kwa kweli tukiwa wamoja hakuna lisiloweza kufanyikana, lakini tukianza kubaguana basi hata hayo maoni yetu yatakuwa hayafai.

Tuangalie madhila tunayoyapata na wala tusije tukamtafuta mchawi ni nani, wachawi ni sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mwisho nawaomba Viongozi wetu wa Kitaifa kwamba, hili ni Baraza tukufu la wananchi na tunawasemea wananchi, kwa hivyo tunaposema hapa kwa mujibu wa taratibu za kisheria na maoni yanayotolewa hapa yafike mahala ndipo. Kwa hivyo, tunaomba Viongozi wetu wa Kitaifa wasiwe woga, na maamuzi ya Wazanzibari yasikilizwe, na tukisikiliza maamuzi ya Wazanzibari, basi *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kila jambo litakuwa zuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Wazanzibari wote tuwe pamoja na wala tusibaguane, na twende kwenye Tume ya Kukuasnya Maoni ya Marekebisho ya Katiba kwa ajili ya kutoa maoni yetu, na sisi kama Wawakilishi wa wananchi tutayalinda yale wanatakayoyatoa wananchi wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimshukuru *Allah Subuhanahu Wataalla* kwa kutujaalia jioni hii kuweza kutoa mawili matatu kuhusiana na Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013.

Kwanza naipongeza hotuba hii. Pili nayakubali yaliomo. Lakini kuna baadhi ya mawili matatu naomba nitoe mawazo yangu. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye ukurasa wa 3 kifungu cha 7 kuhusu hali ya kisiasa. Katika hali ya kisiasa kuna mambo mengi ambayo yameelezwa. Lakini nataka nitoe mawazo yangu kuhusiana na ndugu zetu hawa wa Uamsho. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini pale Uamsho na hili ni swali ambalo inafaa tujiulize. Uamsho ulikuja kutokana na tangazo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba ndani ya mwaka huu tutakuwa na mabadiliko ya Katiba, na mabadiliko haya yataanza mwaka 2012 hadi 2014, na mwisho kutafanywa Kura ya Maoni kwa ajili ya kuweza kutoa mwelekeo wa nchi yetu wapi tunakwenda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Zanzibar muda wote karibu mwaka suala hili imelinyamazia kimya hakuna mwelekeo au muongozo wowote ule wananchi wafanye jambo gani. Kwa hivyo, kutokana na utaratibu na mimi kwanza Mhe. Mwenyekiti sikubali kwamba Uamsho ni kikundi kidogo, hili mimi sikubaliani nalo, isipokuwa Uamsho ni kundi kubwa na limeenea maeneo yote ya Zanzibar. *(Makofi)*

Lakini hasara zaidi Mhe. Mwenyekiti ni kukidharau kitu, kwa sababu cheche ya moto ni ndogo ukiiona, lakini athari yake ni kubwa mno inaweza kuondosha ulimwengu mzima. Kwa mfano matukio kama haya yametokea kwenye maeneo mbali mbali, kama vile hivi karibu ndugu zetu wa Kenya mtu mmoja tu mvutaji wa sigara aliangusha sigara yake ni ndogo tu, lakini karibuni Msitu wa Kenya umalizike kuwaka na watu waweze kuondoka katika ulimwengu.

Kwa hivyo, athari utakayoiona hii ni ndogo au ukasema kikundi cha watu kidogo, basi kitu kidogo ndicho kinachosababisha kuwa kikubwa. Kwa mfano, tunaambiwa kwamba lile tone ndilo linalokuwa mto, na hatimaye mto ukawa bahari. Mhe. Mwenyekiti, tusione kwamba Uamsho ni watu wachache, na kama ukitaka tathmini Mhe. Mwenyekiti jaribu kupita katika maeneo yetu ya Zanzibar sehemu tofauti basi utakuta kwamba asilimia 90 watu ni Uamsho, watu kufika asilimia hiyo huwezi kuwadharau.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba Uamsho ni watu wengi, na hatuna budi kuwaweka kitako kwa ajili ya kushauriana nao na kuwapa maelekezo namna gani tunataka twende katika muungano huu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri suala hilo asilibeze hata kidogo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala zima la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichangie kama wanavyochangia watu, lakini niseme kwamba hapa tulipofika leo na serikali kuanzisha hii Tume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba, baadhi ya wahubiri suala zima la muungano wanalipotoa.

Kwa mfano, juzi nimesikia habari kwenye redio kwamba kuna Mhubiri mmoja Morogoro aliwaambia Watanzania hasa Wazanzibari walioko kule, kwamba Wazanzibari watakapoukataa muungano itapelekea Wazanzibari walioko Bara kupoteza mali zao.

Hali hii ni kuwatisha wananchi Mhe. Mwenyekiti, na wala haiwezekani kama watu wametoa maamuzi kwamba muungano huu hatuutaki tunataka ulio hivi, kwa nini watu wapoteze mali zao.

Vile vile tukiangalia Wazanzibari tunaishi nchi tofauti, tuache hii tuliyoshirikiana kimuungano, lakini Wazanzibari wameenea ulimwenguni hata nchi ambazo huo muungano haupo na Wazanzibari wapo huko na mali zao pamoja na vitu vyao mbali mbali na wanaishi, tuache leo tulipoungana Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, tuichukue hii Tanzania kwani wale wanaoishi Dar-es-Salaam na mikoa mingine ni Wazanzibari tu, wapo Waganda. Kwa kweli Tanzania imewalea Waganda mpaka wengine wakawapa Urais wa Uganda na wala hakuna muungano. Tanzania imewalea Wakongo, wamewasomesha Wakongo mpaka wengine wamepewa Urais hadi leo na wala hapana muungano.

Kwa hivyo, tusione kwamba Wazanzibari waliopo pale kama muungano huu utavunjika waambiwe kwamba mali zao zitapotea tushachuma sana, hapana. Kwa kweli nchi zinashirikiana kwa mambo mbali mbali, kama vile tunaweza kushirikiana kwenye biashara na mambo mengine.

Lakini jambo la msingi ni kuwapa elimu wananchi na kuingia kwenye sakata hili la Katiba, na wala tusikae muda tunao japo kuwa ni mfupi, lakini muda mfupi huu ni muhimu wananchi wetu kuwapa elimu, ili wananchi wetu waje waingie kwenye majadiliano bila ya kuingia kwenye zile njia ambazo hazitaleta mustakbali wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili alione Mhe. Waziri kwamba wakati tulionao wananchi wapewe elimu kwa nini serikali haiundi Kamati Ndogo kupita kwenye mikoa, wilaya na majimbo, ili wananchi wakaelimishwa namna gani tunataka twende.

Lakini tukibakia tu kusema kwamba jiandaeni nendeni kwenye Tume tena kwa wingi, bado hatujafanya kitu, sawa na kumchukua mtoto na kumtuma dukani ukampa fedha na kumwambia nenda dukani, lakini kile unachokihitaji usimwambie itakuwa umempa kazi ya kwenda kule na kurudi. Kwa maana hiyo, jambo la msingi ni kuwapa elimu wananchi namna gani waende wakakabiliane na Tume kwa ajili ya kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Sasa niende kwenye ukurasa wa 15 kifungu cha 30 ambacho kinazungumzia kuhusu suala zima la maafa. Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu hapa kwamba maafa yalitukumba Wazanzibari na Watanzania kwa jumla, kwa sababu meli ile ilianza kutoka Dar-es-Salaam ikafika hapa Unguja na baadae kuelekea Pemba, kwa hivyo watu waliokuwemo ni mchanganyiko, kwa maana Watanzania Bara na Wazanzibari.

Kwa kweli lile si suala dogo, isipokuwa ni kubwa tena ni vyema kuwekewa kumbukumbu, ili liweze kuwa ni historia na wananchi waweze kukumbuka kwamba, kujazana kwenye vyombo vya usafiri haiwezi kutuletea maendeleo katika nchi yetu na inaweza kutuletea maafa makubwa zaidi.

Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti hadi muda huu serikali haijatoa kauli hata moja, kwamba imeshajiandaa kuwapatia wananchi wa Zanzibar usafiri wa meli ya uhakika ambayo inayotayarishwa na serikali na hili ni tatizo. Kwa hivyo, suala hili watu wengi wameshasema na tayari limeshapigiwa kelele tangu Kikao cha Januari, 2012 hadi leo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu ni sikivu sana na tayari wameshaliona hili, natumai kwamba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho hapa anaweza kutupa taarifa kuhusu hii meli.

Vile vile jambo jengine ambalo linalonisikitisha katika suala zima la maafa nimeona hapa kwamba kuna michango ya wafadhili mbali mbali karibu shilingi bilioni 1, ni milioni 248,550,761/=ambazo zimetolewa na wafadhili. Lakini sijakiona kile ambacho serikali kama serikali kile walichokitoa.

Sasa najiuliza hapa serikali katika maafa haya imesaidia nini kama hizi zote zimetolewa na wafadhili. Kwa hivyo, ikiwa ndio hizi haiwezi kuwa serikali ilitoa taarifa zake kueleza wananchi pamoja na Jumuia mbali mbali za Kimataifa au za ndani ya nchi.

Vile vile kuna hivi vitu kama vile nguo na mambo mengine, tangu kutokea maafa yale huu ni mwezi wa 9 mambo haya au nguo hizi bado hazijawakuta wale walengwa na *kufa ni kupishana*. Kwa mfano, alikuwemo kwenye ajali lakini ameshaandaliwa mambo ayapate, lakini kuchelewa chelewa huyu aliyekusudiwa anaweza kufariki na haya ambayo ilikuwa ayapate yeye, basi aje ayapate mtu mwengine asiyehusika. Ningeliiomba sana serikali ijaribu hivi vifaa vilivyobakia kuweza kuvigawa na vikawafikia wale walengwa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba maelezo ya hotuba hii ni mazuri mno. Tatizo kubwa tulilonalo Wazanzibari ni utekelezaji. Hapa tunapokuja kusema, kama tunasema kuiambia matambiko au mizimu, kwa hiyo ukishakuushtakia mzimu, basi mzimu utafanya kazi. Lakini hapa tunawaambia watu na watu tunaowaambia ni Serikali. Kwa hivyo yale yote tunayowaambia serikali hebu ijaribu kuyatekeleza.

Tokea kuanza Serikali hii ya awamu ya saba tuna tatizo la ardhi, na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akaingia kwa kasi mno kulisimamia suala hili. Sijui ilifikia hatua gani kasi ile ikamalizika haraka. Mimi nilifikiri kwamba Makamo wa Pili mara hii atakunjua mbawa zake zote 400. Lakini bahati mbaya hizi mbawa zinakuwa zinaanza kunyonyoka moja moja, hatima yake tutarudi pale pale katika dimbwi la kuonekana kwamba serikali hii ya Umoja wa Kitaifa nguvu zake ni za soda. Mara moja inakuja juu na hatima yake inarudi chini. Ningekuomba sana Mh. Makamo wa Pili uzi ni ule ule.

Mhe. Mwenyekiti hivi sasa tuna matatizo mengi. Mimi katika jimbo langu la Tumbe nina maeneo ya wananchi kuna maeneo ya serikali, lakini mpaka yale ya wananchi yanachukuliwa yanapimwa. Watu wanajiwekea kwa maendeleo yao. Wale wanaomiliki yale mashamba hata kuuliziwa neno. Hizi kesi tunazo katika majimboni kwetu. Pia nina wananchi wangu waliokuwemo katika jimbo la Tumbe lakini wanaishi maeneo ya Makangale, wana mashamba yao tokea enzi na enzi. Hivi sasa kuna wakubwa ndani ya Serikali hii mashamba yake wanakwenda kuyapima na kuweka vitega vyao uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, huo ni uonevu, na tukioneana unyonge huyu mnyonge naye atakwenda wapi. Kwa hivyo ni vyema Mhe. Mwenyekiti kwa kupitia Wizara hii ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, suala la ardhi akalipa kipaumbele ili kuhakikisha wananchi wetu wale wanyonge wamepata rasilimali zao.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa na mimi nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati na kumpongeza Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, pia nitumie fursa hii kumpongeza Makamo wa Pili wa Rais kwa juhudi zake ambazo anatupatia.

Mhe. Spika, nianze na mimi mchango wangu katika suala zima la Muungano. Wenzangu wamechangia sana suala hili lakini na mimi kwa kuwa mdau, inanipasa na mimi nitoe mchango wangu japo mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwanza kila mmoja katika masuala ya muungano basi yaheshimiwe yale maoni yake. Kwa sababu katika suala hili la Muungano mimi binafsi nautaka muungano. Tena nautaka muungano ule ule wa serikali mbili. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mawazo yangu hayo naomba yaheshimiwe na isiwe kikwazo cha kulaaniwa kwa sababu naupenda muungano. Naupenda kwa sababu nazijua faida zake.

Mhe. Mwenyekiti, niseme wale ambao wamenichagua kuingia katika Baraza hili wanaupenda huu Muungano, na tiketi hii waliyonipa nije hasa niwatetee. Nilipoapa niliapa kwa kiapo hicho, nimeapa kwa Katiba ya Zanzibar kwamba nitaitetea lakini pia nikaapa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwamba nitaitetea. Pia naamini Waheshimiwa waliokuwemo humu ndani wote wametumia kiapo hicho. Bila shaka ni yale matatizo machache ambayo yanatukwaza, na *Inshallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu yatatatuka ili tuweze kuona tunaishi katika Muungano wetu kwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la muungano naona linachukuliwa kama labda katika dini kwamba tukiukataa muungano labda ndio tiketi ya kuingilia Peponi, hapana. Mhe. Mwenyekiti, Peponi mtu ataingia kwa kumcha Mwenyezi Mungu kwa dhati. Muungano ni sawa sawa na vyama vyetu, ni sawa sawa na vyama vya mpira. Mimi kama naipenda Yanga huwezi kunilazimisha niipende Simba, na kama naipenda CCM huwezi kunilazimisha niipende CUF, hiyo ni ridhaa ya moyo wangu. Mhe. Mwenyekiti, naomba na sisi ambao tunaupenda muungano yaheshimiwe sana mawazo yetu hayo na wale wafuasi ambao wanaupenda muungano.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mjumbe alizungumzia kuhusu suala zima la Misikiti kwamba kuna watu wanaingia katika Misikiti bila ya kuwa na nidhamu nzuri na pale ni pahala patukufu. Kweli nakubaliana naye, lakini nataka nitumie fursa hii adhimu kuomba na sisi wenyewe waumini tusizivunje taratibu za msikiti. Nasema hayo kwa sababu kuna mwaka mmoja wakati ilipotokea ngangari ile ya kwenda katika jimbo la Donge, dhiki kubwa ilikuwepo maeneo ya Mahonda na ni karibu ya Msikiti. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupigwa mabomu yale watu wengi walikimbilia msikitini bila ya kujua kama wana viatu miguuni au hawana, waliingia ndani ya msikiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuona askari hawakuvunjika moyo wanakuja mle mle msikitini basi watu wale walisali rakaa mia bila ya udhu wala nia ni kwa sababu mabomo yaliyowafanya waingie ndani ya Msikiti. Nawaomba sana, sana waumini wenzangu pale ni pahala pa dini tuzingatie si pahala pa kusema ni kichaka cha kwenda kujificha. Tukiwa tumeshajiandaa basi tujue na mwa kukimbilia, mule ni Msikitini tumupe heshima yake.

Mimi niende katika suala zima la Kamati hii ambayo imechaguliwa kuja kuratibu maoni. Mimi kwa nia nzuri kabisa niwaombe Waheshimiwa wenzangu kuona nafasi hii tunaitumia vyema, vyenginevyo nafasi itakuja na tutachukua jazba zetu tushindwe kukipata kile kitu ambacho tunakihitaji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sidhani kwamba Tume hii ya kukusanya maoni kama itakuja kutuuliza muungano tunautaka au hatuutaki. Nahisi inakuja na suala zima la katiba kwamba tunataka mabadiliko ya katiba mpya, hatutaki basi tutabaki na katiba ya zamani. Sasa kuendelea sisi kuwapa wananchi wetu elimu ya kuwa tuukatae muungano naona kama tunapoteza muda. Niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu kuona suala la muungano tunalisimamia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri, katika muungano kuna kero, na kero hizi ni lazima tusikilizwe maoni ya Wananchi ili kuona kero hizi zinapatiwa ufumbuzi wa dhati, lakini na haki zetu kama zipo za Wazanzibari katika muungano huu ziweze kupatikana kwa mujibu wa taratibu. Nasisitiza sana muungano kwa sababu katika nchi yetu mpaka sasa hivi tunaishi kwa amani, utulivu na mshikamano. Tukivunja muungano naomba ninukuu maneno ya baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ambaye alisema kwamba mkianza kuuvunja Muungano wa Tanganyika, basi muuelewe kwamba dhambi hiyo haitaishia hapo. Mtaendelea hata nyinyi wenyewe kati ya Waunguja na Wapemba matokeo yake mtaanza kubaguana wa Kusini na Kaskazini. Dhambi itaendelea kuwala tu, hata na Bara na wao wakaparaganyika ikawa Wa Arusha ni Arusha na wa Mwanza yuko Mwanza. Hili ni suala la kutilia maanani sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la maafa, suala hili nimuombe sana Mhe. Waziri katika vituo ambavyo vimepangwa vya uokozi, namuomba sana kituo cha Mkokotoni cha KMKM hichi ni kituo muhimu sana.Nawaomba wapatiwe zana pale, wawe na boti ambazo zitakuwa za kisasa, lakini pia kuwe na utaratibu wa kuwekewa mafuta. Mara nyingi zimekuwa zikija simu pale kwa sababu ya kuharakisha chombo ambacho kinatoka Tanga na wao ndio wanakwenda kukifungasha. Lakini mara nyingi kumejitokeza watu ambao wanazama kwa mfano Kisiwa cha Tumbatu mwaka uliopita walizama watu ambao walikuwa wanakwenda katika Maulidi. Watu ambao tunawategemea katika uokozi ni wao, na walikimbilia lakini mara nyingi wanakuwa hawana mafuta. Hilo Mhe. Waziri mlione ili liweze kuwapatia *support* nzuri. Kusema kweli wanafanya kazi kizalendo, wanajitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 40 kuna Idara ya Sherehe. Hili nilikuwa naomba zinapofanyika Sherehe za Muungano, basi kuwe na maandalizi mazuri ambayo yatawafanya vijana wetu wanaotoka hapa kwenda katika Sherehe kule waweze kufanikiwa vizuri bila ya kupata usumbufu wowote. Kumejitokeza wanapokwenda inakuwa ni usumbufu mpaka usiku hawajajua watalala wapi, naomba maandalizi yaanze mapema ili watu wetu waende katika sherehe na isiwe kuchukia sherehe ile.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hassan Hamadi alizungumzia suala la uvuvi, na mimi kwa kuwa katika Mkoa ninaoishi ndio kazi inayofanywa na mimi nalisisitiza. Kweli umezungumzia uvuvi wa Bahari Kuu, lakini pia kuna wavuvi wetu wadogo wadogo ambao wanasumbuka kupata vifaa vile ambavyo vinatakiwa. Kwani wavuvi hawa tumewachomea nyavu zao kwamba hazistahiki zinaharibu mazingira, lakini pia tunasahau kuwapa nyengine ambazo zinakwenda na wakati. Hilo naliomba tuwatimizie wavuvi wetu hawa ili waweze kujipatia rizki zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala zima la mwani mlilitaja, na hiyo pia ni kazi inayofanywa na akina mama wa Mkoa wa Kaskazini. Nimuombe Mhe. Waziri kuwashughulikia akina mama kuweza kuwapatia soko la uhakika ambalo litazingatia kupata bei nzuri ya mwani wao.

Mhe. Mwenyekiti, mawazo yangu ni hayo, lakini nasisitiza sana suala la amani jamani tulizingatie. Amani ikitoweka maana yake hayo mahitaji yote ambayo tunayahitaji yatakuwa hayapatikani. Hakuna kitu chengine isipokuwa amani. Tushikamane tuweze kuona tunafanikiwa juu ya hilo. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa fursa hii, ili uniruhusu nitoe ufafanuzi kuhusu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, imehusishwa kwa kutowajibika kwa kuwaacha watendaji bila ya kuwasimamia kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napenda nimfahamishe Mhe. Mwakilishi alilileta Barazani suala hili kwamba kama watendaji wa Wizara ya Afya walikuwa hawawajibiki pengine ilikuwa zamani, wakati hata mimi mwenyewe pengine nilikuwa sina uwezo wa kusema kwamba wanawajibika au laa. Lakini kwa sasa nataka nikwambie Mheshimiwa uloleta ujumbe huu kama kwa watu wa Wizara ya Afya wanaojua kuwajibika, kwao ni lazima kwa sasa hivi sio suala la hiyari. Kwa sababu Mhe. Waziri wetu anajitahidi iwezekanavyo hilo litendeke. Mapungufu ya ubinaadamu hakosi lakini hili la maabara kutowajibika haliko. Wala Ofisi ya Makamo wa Pili haina kosa.

Nitazungumza kwa nini nasema hivyo. Nataka niwaeleze Wawakilishi waliokuwepo hapa na wananchi wafahamu. Kama Wizara ya Afya tumepewa jukumu la kuhakikisha kwamba hospitali zinapandishwa hadhi. Moja katika hospitali hizo ni Hospitali ya Mnazi Mmoja inatakiwa ipandishwe iwe hadhi ya Rufaa. Ili kufanya hiyo hospitali iwe ya rufaa, kunahitajika maandalizi na hayo maandalizi sio ya siku moja wala sio mwaka mmoja. Ni kitu endelevu

kwa kipindi kitakachotosha kufikisha lengo hilo. Katika vitengo muhimu vya kutambua maradhi ni viwili. Kuna *image* ambapo kunahusika masuala ya *X-ray, Ultra-sound, CT- Scan, Endoscope* na mengineyo. Sehemu ya pili kwa kazi hiyo sio kwa umuhimu lakini ni uchunguzi wa maabara.

Zanzibar kwa kipindi kirefu tulikuwa kwanza hatuna mtaalamu anayehusika na maradhi ya uchunguzi katika kitengo cha *histopathology*. Mimi mwenyewe nimeshaombwa na Dokta Shein mwenyewe niende nikasome hilo suala nikakataa. Kwa sababu cha kukisoma mtu anaamua nafsi yake kile anachokipenda. Alijaribu sana kuna wakati nilikubali halafu nikakataa, mwisho sikwenda kusoma nikasoma kile ninachokitaka. Leo katokea aliyetokea kasoma kwa hivyo ni lazima mtu yule tumuandalie pahala pa kufanyia kazi.

Histopathology ilikuwa inafanywa Muhimbili, na wakati huo Muhimbili ilikuwa inafanya *histopathology* za nchi nzima kama imebadilika hivi leo kwa sababu hospitali za rufaa ni nyingi, ni pale ambapo tunapochukua sehemu za mwili zikapelekwa kule kwenda kuchunguza kwa maradhi tofauti, sio kensa tu kama ilivyoelezwa hata damu inakwenda ikipimwa kule. Kwa kufanya hivyo Wizara ya Afya ikaona kwa makusudi kwamba sasa hichi kitengo kiwepo Zanzibar, kwa sababu wananchi wetu wanasumbuka mno. Kwa hiyo kupitia mpango ya *UNDP* vikaombwa vifaa, tenda ikapitishwa, waliopata ni Shirika moja linaitwa *LAB EQUIPMENT LTD* ambao walikuwa na mkataba wa kuuza hivyo vifaa na kwenda kuvisimika katika maabara ile.

Kilichojitokeza ni kwamba wakati wale wameleta vifaa kwa wakati, maabara nayo ilikuwa inahitaji kufanyiwa utaratibu ili vifaa vile viweze kuingizwa, kwa hali iliyokuwa, ilikuwa maabara haiwezi kufanya hivyo. Kwa hivyo Mrada mwengine wa *ICAP* ukaletwa ili kuifanyia matengenezo makubwa maabara, ili hivyo vifaa viweze kwenda kuwekwa pale.

Kwa bahati mbaya *ICAP* imechukua karibu mwaka mzima kukamilisha hiyo kazi, mkataba ulikuwa chini ya hapo. Kilichotendeka ni kwamba baada ya *ICAP* kumaliza sasa vifaa viende vikawekwe pale ili vifanye kazi. Vifaa vilipoletwa vilikuwa Wizara ya Afya, lakini kwa kuwa Wizara ya Afya hakuna nafasi ikatafutwa nafasi vikapelekwa Mbweni. Mbweni vimekaa kwa mwaka mzima ndani ya maboksi yake havikufunguliwa.

Baada ya maabara kuwa tayari wameambiwa wale watu waje wavihifadhi vile vitu. Vikapelekwa vikatolewa Mbweni vikapelekwa Mnazimmoja, vifaa vilivyokuwemo mle vingi wao ni vifaa vya kisasa. Kwa kweli kuhimili kishindo cha leo Mnazimmoja, kesho Mbweni, kesho kutwa Mnazimmoja athari imetokea na kuna baadhi ya vifaa vimepata mikwaruzo. Kilichotizamwa pale kwamba kile kifaa chenyewe kikipata mkwaruzo kimoja hakiwezi chengie kufanya kazi. Wala hatuwezi tukenda tukanunua *part* moja kwa ajili ya kufidia pale, hayo ndiyo yaliyojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, wakati walipofungua hao wenyewe vifaa kutaka kuvi – *install* wakakuta baadhi ya vifaa havimo. Wakawaandikia barua wakawaambia jamani humu kuna vitu vimepungua. Wakasema jamani mkataba wetu umeshakwisha. Hayo yangekuwa wakati ule wa kipindi cha mkataba tungesema tunawajibika, lakini mmeshakaa mwaka mzima, sasa hivi hilo hatuwezi kuchukua dhamana, labda angalieni huko huko pengine hamjui mmeweka wapi. Lakini vifaa havikufunguliwa ni *parts* ndogo ndogo za zile mashine. Kwa hivyo hapo mtendaji anahusika vipi?

Kilichotendeka kwa vile ile maabara tunaitaka na ile kazi inatakiwa ifanyike, Wizara iliwasiliana na wale watu, wakashauriana na wakakubali watupe vifaa vyengine ambavyo vitafanana na hivyo na sisi tulipe na hayo mengine watatusaidia ili hiyo maabara iweze kuwepo. Kwa maneno niliyoyasikia jana alipopigiwa simu mwenyewe huyo bwana kasema kwamba wiki ijayo vifaa vitatoka Dar-es-Salaam, vitakuja na vitawekwa pale.

Ninachotaka kusema kwa vile hii Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inawajibika kwa hilo, lakini kwa hili la kuchelewa Maabara la kuhakikisha kwamba hivi, hilo hata kama wangelilisimamia kulikuwa hakuna uwezekano wa kufanya vyenginevyo. Kwa kweli hata sisi tumeathirika kwa sababu sisi wenye taaluma hiyo tunataka kama leo kitengo kile kifanye kazi kwa umuhimu wake. Kwa sababu wananchi wanasumbuka, Muhimbili kuna foleni kubwa sana, mtu anafika mpaka kufa kipimo hakijarudi. Inatuathiri sana. Kwa hivyo na sisi tunaona uchungu, lakini wajibu wetu tunafanya na tutahakikisha hicho kitengo kinakuwa Inshallah.

Hayo ndiyo ninayoweza kuyasema kuhusu suala hili. Lakini na mimi nichukue nafasi hii kwa vile watu wote wamesema Muungano, na mimi ni mwana Muungano niseme kidogo. Sitosema kama walivyosema watu, nitasema kwa *staili* yangu.

Mimi nimefaidika na Muungano, nimesoma Diploma na Digrii ya Kwanza kupitia Muungano, Serikali ya Mapinduzi haikunipa hata shilingi, kwa hiyo nimefaidika na Muungano. Nimetembea Bara Mikoa yote unayoijua wewe, na kote ninao watu na marafiki na ndugu. Sio kuwa wa damu lakini nisengependa niwapoteze kwa sababu hii. Sikatai kama jamani kero hakuna na wala sote hatukatai. Wengine labda hawajasema tu, lakini wengi sio kwamba tunalikataa kwamba kero hazipo. Kero zipo na zinatuudhi sote.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna mtu ambaye nnayemuamini na nnayemuona jasiri ni Mhe. Kikwete. Kwa sababu haya hayakuanza leo hivyo, yameanza siku nyingi na hakuna aliyethubutu kusema kwamba sasa hivi tukaeni kitako tulizungumze hili. Hakuna sentensi ninayoipenda kama anaposema "Jamani hakuna kisichozungumzika, tukizungumza tutafikia muafaka". Ni yeye hivyo Kikwete siku aliyoapishwa alisema kwamba "kero za Wazanzibari kugombana wenyewe kwa wenyewe zimenitosha, nitahakikisha kwamba Wazanzibari wanaungana". Tumeungana hapa na tunajisifu, kasema yeye hivyo.

Leo yeye huyu anatupa fursa hapa, wakati tulikuwa tunapiga kelele hatukushirikishwa, tulikuwa hatujazaliwa, wengine hatuujui, wengine tumetaka hatukupewa nafasi. Leo kaunda Tume, kakushirikisheni shirikini, toeni mawazo, kila mtu atoe mawazo. Hakusema kila Mwakilishi awasemee watu wake, ni kila mtu atoe mawazo. Kwa sababu wewe Mwakilishi unaweza ukasimama ukasema kwamba mimi kwa niaba ya Jimbo langu nasema hivi. Unajuaje kama watu wote katika jimbo lako wanataka hivyo. Wacheni wenyewe *waseemee*. Msitutilie maneno midomoni mwetu. Kila mtu aseme lile analotaka, nafasi imetolewa kila mtu aseme. Hapa uwakilishi hauna nafasi ya hivyo. Tuna nafasi ya kuja kusema hapa ya kwetu, lakini kwa la Muungano aah hilo nafasi hatuna. Tumepewa ruhsa kila mtu akaseme.

Mie hapa sisemi nitasema kwenye Tume kama nautaka au siutaki, na nautaka wa aina ngapi, maana hapa si pahala pake. Hata nikisema haisaidii, sina haja ya kupoteza nguvu kwa kitu ambacho najua hakileti matunda, nitakwenda kusema huko. Lakini mjue na huko nje watu wanasema hivyo kwamba nyie mnaukataa Muungano. Aliyoyasema Bi Shawana sio ya uongo, wanasema Serikali hazitokuwa mbili au tatu zitakuwa nne, Pemba yake, Unguja yake, Bara yake, ndio tunapotaka kwenda huko? Mimi nautaka Muungano. Ahsanteni.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, na pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kutoa mawili matatu katika kuunga mkono bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote ninapenda nitamke kwamba mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka naunga mkono asilimia mia kwa mia. Lakini la pili napenda nichukue nafasi hii kutoa pongezi zangu kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwenye bajeti hii na hasa katika ukurasa wa 8 kifungu cha 15 na 16, kwa kuonesha dhamira na azma ya Serikali katika kusaidia na kuimarisha shughuli za kilimo, lakini shughuli za wavuvi hasa wavuvi wadogo wadogo.

Ni imani yangu kwamba kwa kutambua kuwa uwekezaji wa meli Mhe. Mwenyekiti, za wavuvi zitakuwa ni chache au hazitotanua wigo kwa sehemu kubwa kwa wananchi. Mategemeo yetu kuwa tutakapoweza kuunga mkono na kuviimarisha vikundi hivi vya wavuvi wadogo wadogo, mategemeo yetu kuwa wananchi hawa wataweza kuongeza nguvu ya kipato, lakini uwezo wa kuhimili changamoto na ugumu wa maisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo na mimi nichukue nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa mambo machache sana, likiwemo suala la kwanza lililohusiana hoja ya kwamba kama kuna maelewano mazuri kati ya Jeshi la Polisi na Idara ya Usafiri na Leseni Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda nikiri kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana kati ya taasisi hizi mbili. Lakini pia kumejitokeza changamoto, na changamoto hii ipo katika sehemu mbili.

Upo upande mmoja wa Serikali, kwa kumaanisha kuna mapungufu ya kisheria lakini upande wa pili ni wenzetu wa Polisi kuregeza kamba katika usimamizi na utekelezaji kwa mujibu wa masharti ya sheria iliyopo. Mategemeo yangu kwamba Jeshi la Polisi wataendelea kuimarisha uhusiano wetu huu kwa kutambua wao wana jukumu la kusimamia sheria za nchi yetu. Matarajio yangu watafanya hivyo kama vile wanavyofanya katika usimamizi wa sheria Na. 6 ya mwaka 2004; inayohusiana na makosa ya jinai na kutunga sheria yetu ya Na. 7 ya mwaka 2003 katika usimamizi na hasa usalama wa vyombo vya barabarani. Na sisi kama Wizara tatizo la Kanuni hasa katika hiki kitu ambacho wanachokipigia kelele Polisi cha kuweza kuwaruhusu kupiga faini maeneo ya hapo hapo, tupo mbioni katika kukamilisha na tutakapokamilisha Kanuni hii tunaamini kwamba jambo hili nalo litawapa nguvu Polisi katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni suala linalohusiana na kampuni ya ZAT katika utoaji wa huduma kwenye Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume International Airport iliopo Kisauni Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu kampuni hii ilikuwa imeingia mkataba na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa huduma za uchukuzi wa mizigo pamoja na huduma nyengine za *ground handling* katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume. Kwa bahati nzuri mkataba wao huu ulikuwa ni mkataba wa kipekee, kwa maana hakuna shirika jengine ambalo liliruhusiwa kufanya biashara hii. Lakini tabaan muda umekuwa mrefu na Serikali ikafanya maamuzi kwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kutakiwa kukaa na kampuni hii katika kuona namna ya ufanyaji wake kazi kwa kuona mtaji wao, fedha zao lakini vifaa kwa ajili ya kutoa huduma.

Baada ya kukaa na kutafakari kwa kina kukaonekana kuna mapungufu, aidha ya kiutawala au ya uendeshaji wa kampuni hii. Ndipo Serikali ilipofanya maamuzi ya kushauriana kisheria na hatimaye kufikia pahali pa kuwataka kampuni iondolewe ile kipekee katika mkataba wake, na kuruhusu kampuni nyengine kuja katika ushindani wa kutoa huduma.

Msimamo wa Serikali Mhe. Mwenyekiti, kampuni hii itaendelea kuwepo na kutoa huduma zake katika uwanja wa ndege, lakini kilichoamuliwa na serikali itolewe fursa ya kutangaza zabuni kwa kampuni nyengine kuja kununua zabuni kufuata masharti yaliyopo, na kampuni itakayoshinda kuweza kushirikiana na kampuni hii kwenye kutoa huduma.

Hivyo basi Mhe. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe na wengineo watakaosikia kama mtu amekuja na kauli ya kusema kwamba ZAT inaondoshwa, kauli yake si sahihi. Kauli iliopo ni kuona kwamba ZAT inaimarika kwa mujibu wa sheria iliopo na kushirikiana na kampuni itakayoshinda zabuni.

Mhe. Mwenyekiti, matarajio ya Serikali kwamba kampuni itakayoshinda ikishirikiana na ZAT, huduma za uwanja wa ndege zitaimarika na zikiimarika huduma za uwanja wa ndege ndio kuimarisha mapato, kwani sote tunatambua kuwa uwanja wa ndege ndio mlango mkuu wa sekta ya uwekezaji hasa na watembeaji, kwa maana ya watalii wanaoingia nchini mwetu. Kwa hivyo ikiwa uwanja wetu utaimarika kihuduma tabaan, na wageni wetu nao watafurahia huduma hizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine limezungumzwa ni suala la ununuzi wa meli. Kwa muda mrefu Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya jitihada zake kuwaondoshea wananchi matatizo ya usafiri hasa kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Kwa muda mrefu tumekuwa tunamiliki meli mbili ambazo zimekuwa chakavu, na muda mara kwa mara kama desturi ya kuharibika, na inapoharibika meli kweli kunakuwa na usumbufu na matatizo ya usafiri kwa watu wanao-*cross* visiwa hivi kutoka Unguja kwenda Pemba.

Katika kuliona hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikia maamuzi mazuri na kuiamuru wizara kuingia machakachani kwenda kutafuta wazabuni na wajenzi wa meli kwenda kwa ajili ya maamuzi ya ujengaji wa meli mpya itakayokidhi mahitaji ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda nitoe kauli kwamba suala hili la utafutaji wa meli, maelezo mazuri zaidi yatakuja katika bajeti yetu tutakayokuja kuisoma tarehe 13 kwenye majaaliwa. Naomba wavute subra kwa kuamini kuwa Serikali imefanya maamuzi mazuri, sahihi na yenye matumaini kwa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine lililozungumzwa hapa ni suala la barabara kwa eneo la Ngomeni. Ninamuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Halmashauri husika, tutakaa tuone watu wa huko nao kwa kiasi gani tutawapunguzia changamoto hii ya kukosa huduma ya barabara.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala jengine limezungumzwa ni suala la mfanyakazi, na ninaomba sana tuweke kumbukumbu sahihi. Maelezo yaliyoelezwa hapa kwamba kuna mfanyakazi amefukuzwa kazi katika wizara yangu kwa sababu tu ametoa taarifa nzuri kwa Kamati Teule. Taarifa hizi si sahihi Mhe. Mwenyekiti, na si kweli.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tukumbushane Waheshimiwa Wajumbe tupo katika chombo muhimu, na chombo hiki kina kauli ndefu na kubwa. Taarifa za kusema mfanyakazi amefukuzwa kazi kwa sababu tu ametoa ushirikiano mzuri kwa kamati teule hazikuwa sahihi, na haikuwa haki kusemwa kwa kauli kama ile.

Mhe. Mwenyekiti, mfanyakazi aliyefukuzwa ni mfanyakazi muongo, mdanganyifu, aliyeipotosha serikali kupata kwake ajira. Amedanganya katika cheti chake cha kuzaliwa, kitambulisho cha Mzanzibari, cheti cha skuli na tabaan na vyeti vyengine alivyoviambatanisha wakati alipofanya maombi ya uajiri serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ilichokifanya katika utaratibu ulioelekezwa na serikali katika kuhakiki wafanyakazi, alipotakiwa mfanyakazi huyu aende akatafute kitambulisho cha Mzanzibari ndipo alipokwama katika Idara husika. Amekwenda katika Idara ya Vitambulisho akadanganya jina lake halisi kwa kutaja jina ambalo ameingiziwa kazini. Baada ya kuangalia katika *database* ya watu wa vitambulisho, wakamwambia mtu mwenye jina hili yumo kitambulisho chake nambari hii, wewe jina lako ni jina fulani na kitambulisho chako nambari hii.

Baada ya watu wa vitambulisho kugundua hilo, ndipo walipotuandikia Wizara yangu. Jitihada ya wizara yangu tukawaandikia Tume ya Utumishi Serikalini. Tume ya Utumishi ikataka tujiridhishe, tukawarejeshea tena kwamba tumejiridhisha na taarifa hii. Tume ya Utumishi wakatuamuru tumsimamishe kazi tumpe nafasi ya kumuuliza. Tumemsimamisha kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ninayo barua ambayo yeye mwenyewe mfanyakazi amekiri kwamba mimi nimedanganya na ninaomba mnisaidie niendelee kubaki kazini. Sasa anapokuja Mhe. Mjumbe kwa kusema kwamba amefukuzwa kazi kwa sababu tu ametoa ushirikiano kwa Kamati Teule, hii si sahihi. Usahihi angesema kwamba amedanganya na amepotosha.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ambazo wenzetu wa vitambulisho wanasubiri ni kuamuru tu kwamba sisi tumeshamuondoa kazini na wao waendelee na mchakato wa kumfikisha mahakamani kama sheria inavyowaruhusu, lakini pia tumeshamuandikia DPP kwa kuchukua hatua stahiki za kumshtaki mahakamani kwa kudanganya kwani ni kinyume na sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine mimi naomba tu kwa nafasi ndogo sana nichangie suala la Muungano. Suala la Muungano ni miongoni mwa changamoto za kukuza demokrasia na kutafuta haki kwa upande unaostahiki. Naomba sana kwa Waheshimiwa Wajumbe tutumie haki hii, fursa hii kwa kuheshimu mipaka ya kila mmoja wetu. Kila mmoja ana utashi katika moyo wake.

Lakini utashi wa mmoja usimsukume mwengine kwamba alazimike kufuata maamuzi ya mwengine. Mimi moyo, mawazo na utashi wangu na ukifika wakati wa kufanya maamuzi nitafanya maamuzi kwa ridhaa yangu.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tusichukue kigezo hiki cha kufanya mabadiliko ya Katiba kutafuta sababu ya kurudi kule ambapo tumerudi. Sote tumeona kadhia ya kutoishi pamoja, kutokuwa ndugu na kutokuwa marafiki.

Msingi ule ule tuliotumia kufanya kura ya maoni ya kuwa na serikali ya umoja wa kitaifa, mimi ninaamini hakuna ambaye aliyeshurutishwa, hakuna ambaye aliyelazimishwa na hakuna aliyetoka kufanya kwa niaba ya mwengine. Mategemeo yangu kwamba uhuru ule ambao tumeupata tutaendelea kuuheshimu, wenzetu kila mmoja atoe maoni yake, awe uhuru bila ya shindikizo, bila ya ulazima kufanya maamuzi kwa manufaa ya kundi fulani au watu.

Ninayasema haya kwa kutambua kwamba kuna dhana ya kuwa tunataka tutengeneze sote tuwe na kauli moja, jambo ambalo haliwezekani kwa sababu jambo hili linakuja kwa mnasaba wa kuamua. Ukifika pahala pa kuamua kila mmoja ana maamuzi yake, na uhuru huu umo katika Katiba na uhuru huu unatokana na maumbile ya mwanadamu kwamba pakifika pahala pa kuamua kila mmoja ana akili na mawazo yake. Aliyeona kasoro ameziona, aliyeona faida ameziona, aliyechoshwa na kasoro na aliyeridhika na faida anaziona. Sasa tuombe Mhe. Mwenyekiti, kwamba uhuru huu wa Kikatiba tunauheshimu na usiwe chanzo cha kupandikiza chuki miongoni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba nirejee tena kwa kusema kwamba mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka tunaunga mkono bajeti hii asilimia mia moja kwa mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata fursa hii kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimeigusa wizara yangu, sijibu hoja ninatoa ufafanuzi.

Pili naomba nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji wa hotuba ya bajeti ya matumizi kwa kipindi cha mwaka 2012/13 ambayo imewasilishwa kwa niaba yake na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo na yeye nimpongeze pamoja na watendaji wao kwa kukaa na kufikiri wakaweza kutuletea bajeti yao hii, na leo hii tupo hapa kama Baraza la Wawakilishi tumepata kazi ya kufanya kwa siku ya jana na leo.

Mhe. Mwenyekiti, nitapenda nizungumzie eneo hasa linalohusu masuala ya uwajibikaji, lakini nitaliunganisha na masuala ya utendaji wa utumishi wa umma kama lilivyochangiwa na Waheshimiwa Wawakilishi katika Baraza lako tukufu hili kuanzia jana na leo hii.

Katika kusema hili sitapata nafasi ya kuweza kusema nani kasema, lakini mimi ninatoa ufafanuzi kama nilivyosema, sijibu hoja.

Ni kweli ninakubaliana na wale Waheshimiwa waliosema kwamba watumishi wetu katika nchi yetu ya Zanzibar wamekuwa wanafanya kazi kwa mazoea. Katika hali hiyo kunakosekana uwajibikaji katika wajibu wao mkuu wa kuweza kuwatumia wananchi ambao sote ndio waliotuajiri, kuanzia mtumishi wa ngazi ya chini mpaka Mhe. Rais, wananchi ndio waliotuajiri.

Sasa ninakubaliana na Waheshimiwa ambao waliosema ni kweli katika kipindi kirefu tumekuwa tunafanya kazi kwa mazoea lakini tunafanya kazi vile vile kwa muhali, kama rafiki yangu mmoja alivyoninukuu kufuatia swali nilivyolijibu juzi. Sasa hii inatokana na nini. Inatokana na kwamba kwa muda mrefu sasa tumekuwa hatuna utaratibu wa kiutumishi na usimamizi uliokuwa bora zaidi ya usimamizi katika masuala ya utumishi.

Kama tunavyoelewa Serikali ya awamu ya saba ilipoingia madarakani ilirithi wazo kutoka serikali awamu ya sita la kufanya mageuzi katika utumishi wa umma. Kwa maana hiyo Serikali ilifanya ilipoweza, na serikali ya awamu ya saba ilipoingia tukaona jambo la msingi la kwanza ni kuja na sheria Na. 2 ya mwaka 2011 ya Utumishi wa Umma.

Sheria hii sasa imeweka misingi ya utumishi uliotukuka, utumishi utakaokwenda na kiwango cha kimataifa kwa mujibu wa kiwango cha kimataifa na sheria au na mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (ILO). Kuna mambo mengi ambayo tumeyazungumza katika sheria hii ya utumishi wa umma ambayo yanaitambua sheria Na.11 ya 2005 ya *Employment Act* ya hapa Zanzibar, ambayo sheria hiyo imekuja kwa kuzingatia mikataba ya Shirika la Kazi Duniani.

Sasa na sisi tulipotunga sheria yetu tukasema suala zima ambalo limezungumzwa na Wajumbe ni kuhusu suala la wafanyakazi kutotimiza masaa yao ya kazi katika kufanya wajibu wao. Hilo ni kweli. Ninakubaliana na Waheshimiwa wote waliolisema hili kwamba katika eneo hili tumekuwa tukifanya kazi kwa muhali.

Mara nyingi wafanyakazi hasa watumishi wa umma rahisi kudai maslahi, lakini wanasahau wajibu wao wa pili kama Mheshimiwa mmoja alivyosema kwamba hakuna haki bila ya wajibu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba tumsikilize Mhe. Waziri wakati anatoa baadhi ya maelekezo. Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hakuna haki bila ya wajibu. Haki na wajibu ni watoto pacha.

Ili uweze kupata maslahi mazuri lazima utimize wajibu wako. Ndio maana katika sheria hii tunakuja na vitu vya msingi katika kuoanisha haki na wajibu kwa watumishi wa umma. Ndio maana tumekuja na dhana hii ya kumpima mtumishi katika utendaji wake wa kazi, tunaita *Performance Appraisal*.

Katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha tunategeneza kitu kinaitwa mkataba kati ya wananchi na mtumishi wa umma, ili mtumishi ajue kwamba anafanya kazi kwa makubaliano kati yake yeye na wananchi. Lazima atimize yale masharti ambayo yatawekwa kwenye mkataba ndipo ataweza kupata haki zake nyengine za msingi hasa zile zinazohusu maslahi ya utumishi.

Lakini katika dhana nzima ya uwajibikaji kwenye ngazi mbali mbali, kuanzia mtumishi wa umma mpaka Mhe. Rais wetu, kama nilivyosema juzi na leo nataka nirejee, kuna kitu kinaitwa *Performance Contract*, kinakuwa kati ya wananchi na sote tunaowatumia wananchi. Waziri mkataba wake upo kwa nani, tabaan Waziri mkataba wake upo kwa Mhe. Rais na ndio maana kumekuja hii dhana ya kwenda na utekelezaji wa kipindi cha robo mwaka kwa kila Wizara. Tunakwenda na mpango kazi.

Hii ni kuonesha kuwa kuna mkataba kati ya Waziri na Mhe. Rais, na kuna mkataba vile vile kati ya Katibu Mkuu na Waziri wake, kuna mkataba vile vile kati ya Katibu Mkuu na Wakurugenzi wake, kuna mkataba vile vile kati ya Wakurugenzi na wafanyakazi wao wa chini. Kila mmoja ana eneo analoliongoza.

Katika hali hiyo vile vile kuna mkataba kati ya Serikali na Wananchi kupitia Baraza la Wawakilishi, ndio inapokuja ile dhana ya usimamizi wa serikali. Sasa mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba waendelee kuvumilia si kwa muda mrefu sana vipimo hivi vitaonekana wazi wazi, na atakayekuwa hatowajibika basi taratibu za uchukuaji hatua kwa kila mmoja kwa eneo lake zitawekwa.

Kama munavyoelewa kwamba Wizara hii imeundwa katika awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Wakati tunaingia tunapewa jukumu hili la kupima utendaji wa watumishi hatuna hata sera ambayo inatuongoza. Lakini ninapenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kipindi hiki cha muda mfupi tayari tuna Sera ya Utawala Bora. Humu yamo mambo ya uwajibikaji ambayo yameelezwa. Katika suala zima la utawala bora kuna mambo ya msingi ya utawala bora kama sita.

Jambo la kwanza katika hayo sita ni suala la uwajibikaji. Imeelezwa kwa wazi kabisa uwajibikaji ni nini, na nani anatakiwa asimamie hili. Sasa Wizara yangu kwa niaba ya serikali tunaifanya hii kazi. Katika kitabu hiki cha sera ya utawala bora kuna eneo la tamko la sera katika lengo makhususi la sita la utawala bora katika mkakati wa sita wa sera kifungu cha 3 kinazungumza hivi naomba ninukuu, “Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na kikundi kazi cha taifa cha utawala bora kitatoa matokeo yote ya utafiti kwa umma pamoja na ripoti ya mwaka ya utawala bora Zanzibar”.

Katika lengo la Saba tamko la sera kwenye kifungu cha 4 kinasema hivi, naomba ninukuu, “Wajumbe wa kikundi kazi cha kitaifa cha utawala bora watakuwa ndio dhamana ya kuandaa Ripoti hii na kuwasilisha Wizara inayoshughulikia utawala bora, ripoti hiyo itakuwa ni sehemu ya ripoti ya mwaka ya utawala bora Zanzibar ambayo itatolewa kwa umma”.

Yote haya yamefanywa kwa madhumuni ya kuondokana kufanya kazi kwa mazoea. Kwa hivyo sisi kama wizara husika tunaosimamia suala la uwajibikaji, kazi yetu ni kuanika wazi masuala yote ya uwajibikaji, kuanzia mtumishi

wa umma kutokana na yale maelezo niliyoyasema mwanzo yapo katika eneo la utumishi yatakayoainishwa na suala zima la uwajibikaji katika sera hii ya utawala bora.

Kwa maana hiyo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais itakuwa ni rahisi sana kumgundua nani miongoni mwa wasimamizi ambao wamepewa dhamana hawajibiki ipasavyo. Itakuwa kazi yake ni rahisi sana, na bahati nzuri Baraza hili nalo kuna sehemu limetajwa, nalo vile vile itakuwa kazi yao ni rahisi sana na hatimaye kila anayehusika na kumuwajibisha mtumishi husika atafanya kazi hiyo. Kwa kuzingatia kwamba hiki kikundi cha kitaifa cha utawala bora kina Wakurugenzi sera, utafiti wa wizara zote pamoja na taasisi nyengine zisizo za kiserikali.

Tunategemea kwamba kila Wizara kwa mujibu wa muongozo wa sera unatakiwa kuwa na kamati hiyo. Ni wito wangu kwa Wizara na taasisi za umma zilizokuwa hazijaanzisha zianzishe, ili tuweze kupata tathmini kweli ambayo itakuwa inaelezea hali halisi ya uwajibikaji katika utumishi wa umma

Mhe. Mwenyekiti, nilisema niseme hayo na isionekane kama kwamba serikali ya awamu ya saba hakuna jambo ambalo tumelifanya. Tuko mbali, Sheria hii ya Utumishi wa Umma ilikuwa haiko. Zamani kulikuwa na *Public Service Degree* ya mwaka 1959, baadae kukawa na sheria ya Tume ya Utumishi Serikalini. Hizi zote zilikuja kwa lengo hilo. Lakini pia tukaziona zote hizi haziwezi kutufikisha pale ambapo tunakusudia kufika, napo ni watumishi kuwajibika. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe nakubaliana na wale wote waliosema kwamba watumishi wetu wamekuwa wanafanya kazi kwa mazoea, wanakwenda kazini *time* anayotaka mwenyewe na anaondoka *time* anayotaka mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niseme kwamba baada ya kukamilisha hizo taratibu zote, hakuna mtumishi ambaye atapata msamaha katika uwajibikaji wake katika kuwatekelezea wananchi majukumu yaliyowekwa. Kwa mujibu wa mkataba wake, tumegundua hata hii mikataba ya utumishi iliopo sasa ina mapungufu. Ndio maana tunaona sasa hivi kuna watumishi ambao wanaweza leo wakaajiriwa, kesho wakatafuta nafasi ya kwenda kusoma, kabla ya kutimiza yale masharti ambayo anatakiwa ayafuate. Tunataka watu wajiendeleze, hatukatai, lakini inapotangazwa nafasi mpya tupu ya ajira maana yake kuna pengo. Kwa hivyo, ni lazima mtumishi uitumikie nafasi ile kwanza, halafu ikifika muda wa miaka miwili serikali itakupa fursa ya kwenda kujiongezea maarifa.

Kwa hivyo, niwaombe kwa kupitia Baraza lako tukufu na kupitia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mwenyewe, kwamba watumishi sasa tubadilike na tutakapokuwa tunafanya kazi hiyo, niwaombe sana wenzangu waone kwamba sheria na taratibu zetu za miongozo hii ya sera inatutaka tufanye hivyo, tusije tukaonekana Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora tunafanya kazi za wizara nyengine, tunatekeleza tu ule wajibu wetu. Katika hilo sitochelea kuchukua hatua kwa kuchelea kuona kwamba mtu ataniona ninamuingilia majukumu yake ya kazi. Maana ndio mkataba ambao nimeuchukua mimi na Mhe. Rais aliyeniteua, na mimi nitaripoti kwa bosi wangu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba shughuli hizi kuna moja, mbili na tatu. Lakini vile vile shughuli zitakuwa wazi kwa mujibu wa taratibu, wananchi wote wataona. Kwa hivyo, yule anayezembea wananchi pia watajua kwamba fulani anazembea.

Mhe. Mwenyekiti, katika misingi hiyo sita, hilo ni eneo moja tu la uwajibikaji, lakini kuna suala la kufuata utawala wa sheria na mambo mengine. Kwa hivyo, yote hayo katika suala la uwajibikaji ni lazima yote tuyazingatie, unapotekeleza, unapomuwajibisha mtu, unamuwajibisha tu kwa sababu Ripoti ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasema hivyo, imefuata sheria na nini. Lazima tufike huko.
Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, nilisema nizungumzie eneo hili linalohusu watumishi wa umma nilihusishe na suala la uwajibikaji. Nitakapokuja kwenye wizara yangu kesho kutwa kwenye bajeti yangu nitayaeleza mambo haya kwa upana zaidi, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi vitabu hivi nitavitoa kwa waheshimiwa wote, ili wajuwe huo utawala bora ni nini na uwajibikaji ni nini. Baada ya kwishakusema hayo naunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Haya Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile muda wetu umebakia mdogo na Mhe. Mwanasheria Mkuu hajazungumza. Tumuombe basi Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ili tuweze kuweka kanuni kando tuendelee na utaratibu wetu. Mhe. Waziri.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa shughuli zilizokuwa mbele yetu za leo bado zinaendelea, na kwa kuwa muda uliobakia hautoshi kumalizia shughuli zilizokuwa mbele yetu. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando, ili tuweze kusikiliza mchango wa Mhe. Mwanasheria Mkuu na baadae tuweze kuahirisha Baraza letu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuweka kanuni kando, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono juu. Wasioafiki. Walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa nikupe shukrani zangu kwa kunipa fursa hii. Pia niwashukuru Wajumbe kwa kukubali tupate muda kidogo, labda kusaidia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa wakati Waheshimiwa Wajumbe walipokuwa wakichangia hoja. Nitajitahidi sana kadiri inavyowezekana, nisitumie muda wa ziada. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, zilizungumzwa hoja nyingi, lakini mimi naomba nitoe mchango katika hoja kama nne tu. Hoja ya kwanza ambayo imezungumzwa sana ni suala la migogoro ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wameonesha *concern* yao juu ya ukubwa wa hili tatizo. Mimi nakiri kwamba ni kweli linaonekana kuwa tuna tatizo katika eneo hili. Pengine tatizo ni kubwa zaidi kuliko hata hivyo Waheshimiwa Wajumbe wanavyoliona. Kwa hivyo, kilio chao nadhani ni cha msingi kabisa. Lakini nilisema niwatanabahishe wenzangu kwamba katika migogoro ya ardhi, tuna tatizo la msingi kabisa. Niliposema kwamba inawezekana kuwa tatizo ni kubwa zaidi kuliko wanavyoliona, ni kwamba wenyewe pengine tuna migogoro ya ardhi, hata sisi wenyewe bila kujua. Naamini wengi tunamiliki ardhi ama mashamba ama vikataa ama vya mtu mmoja mmoja au vya familia, lakini wachache sijui kama wapo ukimuuliza waraka wa shamba hilo au kikataa hicho kama anao. Kama huna waraka maana yake huo ni mgogoro, kwa sababu hasa utakachotumia ni hoja tu, ya kwamba aah! Nilikuwepo zamani hapa mimi, hii ni ardhi yetu tokea enzi za zamani, na mwengine atasema na zama hizo hata sisi ilikuwa ni ardhi yetu.

Tatizo Mhe. Mwenyekiti, limeanza muda mrefu. Zanzibar yenyewe ina historia ya migogoro ya ardhi. Bwana mmoja anayeitwa Midlton aliandika kitabu nadhani mwaka 1952 akaeleza. Kitu cha kushangaza migogoro mingi ambayo tunaizungumza leo basi imezungumzwa toka wakati huo. Kile kitabu nilimpa Mhe. Ali Juma Shamuhuna, naamini alikipenda maana yake bado hajanirudishia, kwa sababu kinaeleza huko tunakotoka. Lakini Serikali wakati ule pia ikaja nchi yetu ikawa inaongozwa na sheria nne tu za ardhi. Sura ya 93, 94, 95 mpaka sura ya 100. Lakini baada ya Mapinduzi, nchi yetu ikaongozwa na sheria mbili tu za ardhi, sheria nambari 8 ya mwaka 1964 na sheria nambari 10 ya mwaka 1966. Ilichojua ni ile kuendeleza sera ya ardhi baada ya Mapinduzi. Kuchukua ardhi ikagaiwa kwa wananchi, maana sheria moja ilikuwa ni ya kuchukua, hiyo nambari 8 ya mwaka 1964, sheria nambari 10 ilikuwa ni ya kugawa ardhi. Sheria hizo mbili tokea mwaka 1964 mpaka mwaka 1989 ndio sheria zilizokuwa zikisimamia ardhi katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukafika pahala tukajikuta kweli tuna tatizo la msingi, maana wale waliopewa ardhi wengi wameigawa tena, wengine wameiuza na wengine wameiacha. Kuna maeneo yale ya serikali hayakugaiwa hayajulikani nani mwenyewe. Kwa hivyo, ule mgogoro au tatizo la ardhi katika nchi yetu kwa kweli limekuwa ni kubwa sana. Kuanzia mwaka 1989 mpaka mwaka 1994 serikali ikapata msaada wa kupata mtaalamu, ambapo tatizo la ardhi kwa Zanzibar likatazamwa kwa kina kabisa. Pia akaja na mapendekezo ya kutungwa kwa sheria saba za ardhi.

Kwanza sheria ya Kamisheni ya Ardhi nambari 6 ya mwaka 1989, sheria ya utambuzi wa ardhi. Maana yake hilo tatizo ndio hilo ninalosema, lilikuwepo na yeye alichosema kwa Waswahili wangesema labda sisemi msemo huu kwa kumkera Mhe. Hamza Hassan maana naona hii misemo inamkera. Lakini waswahili wanasema, ‘chuwa unachagua kwenye mchele, sio kwenye mpunga, ukichagua kwenye mpunga chuwa utaumwaga mpunga wote kwa kweli’. Sasa yeye alichopendekeza ni kwamba jamani mlionao sasa ni mpunga. Kwa hivyo, tutengeneze mchele

halafu ndio tuchague chuwa. Ndio wakaja na sheria hii ya utambuzi wa ardhi, nani mwenye kipande hiki cha ardhi, hichi cha nani na hichi cha nani, inaitwa *Land Adjudication*.

Jengine akaja na mapendekezo ya sheria ya *Land Survey* nambari 9 ya mwaka 1990, *Registered Land Act* nambari 10 ya mwaka 1990, *Land Tenure Act* nambari 12 ya mwaka 1992 na sheria ya sita ni *Land Tribunal Act* nambari 7 ya mwaka 1994 na mwisho akaja na sheria ya kupendekeza kwamba ule utaratibu wa kuhaulisha ardhi basi usiwe wa kiholela, ndio akaja na mapendekezo ya sheria ya *Land Transfer Act* nambari 8 ya mwaka 1994. Sheria hizi zilitakiwa zitekelezwe kwa mpango, yaani ikitoka sheria hii.

Kwanza unaanza na hiyo kamisheni ya ardhi yenyewe iwepo, iwe na wataalamu wafanye kazi ili ufanywe sasa utaratibu huo wa kutwanga huo mpunga wenyewe. Yaani *Land Adjudication* na hiyo *Land Adjudication* Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya haikufanyika na kama hujafanya *Land Adjudication* maana yake ndio tunasema, tunaona mizozo ya ardhi ni ile tunayoizungumza, lakini sisi wenyewe humu ndani tuna mizozo chungu nzima ya ardhi, kwa sababu hatuna ushahidi, hatuna nyaraka na hiyo ni kawaida kwa watu, nenda katika kijiji chochote watu wanamiliki ardhi, lakini hakuna anayejulikana. Kwa kule Pemba kila zikizaliwa karafuu basi mizozo ya ardhi inakuja. Kwa sababu mpaka mara hii ulipita hapa mtu mara nyengine anakuja anakuambia hapana, mpaka wangu ulikuwa hapa bwana, huu mkarafuu miaka yote tunauchuma huu, inazuka kwa sababu hili halikufanyika.

Sasa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kweli alipokuja alifanya kazi nzuri sana, kazi yake ilisaidia na ilichosaidia ilisaidia kukata lile gugu, kujua hasa tatizo kwani liko pahala gani. Serikali ndipo ilipokaa na kutafakari ikasema baada ya ile juhudi yake iliyofanya, ikasema hapana, hapa tuna tatizo, tukienda nalo hivi kipande kipande tatizo hili haliwezi kutatuka, hebu turudi katika utaratibu wa kusimamia huu mfumo ambao tulikwishawekewa, lakini baadae tukauacha na ndio sasa hivi kinachofanyika na serikali kuandaa utaratibu. Waraka aliuleta Mhe. Mohamed Aboud kulieleza tatizo hili, na kazi hiyo ndio sasa hivi serikali inaifanya, kwamba turudi katika utaratibu wa kama vile ambavyo tulikubali ushauri, tukapitisha sheria, lakini sheria tukaziweka upande na tukaanza kwenda katika utaratibu ambao umetuzidishia migogoro ya ardhi.

Kwa hivyo, kweli ni tatizo, lakini serikali haikukaa kimpya na watu walioona labda Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alifanya kazi halafu ikawa ni nguvu ya soda. Mimi nadhani sio sahihi. Kazi yake kwa kweli ilisaidia sana kukata lile gugu na kuonesha tuna tatizo kiasi gani na ndio sasa hivi linalofanyiwa kazi. Sasa kama kuna watu wanasema labda mpaka kwa Kamati Teule. Hilo sijui, lakini ninachosema ni kwamba tatizo *anatomy* yake iko hapo, kama hujajua *anatomy* sijui kama utaweza kufanya operesheni. Lakini tatizo liko hapo na hayo mengine ya moja moja nayo yana utaratibu wake wa kushughulikia.

Jambo jengine la pili Mhe. Mwenyekiti, ambalo nilihisi nilizungumzie ni suala la kutanabahisha kanuni zetu, zimekuja hoja nyingi kuhusiana na Kamati Teule. Mhe. Mwenyekiti, tulilizungumza suala hili la kamati teule kwa kina katika bajeti ya serikali, tukalitolea ufafanuzi, tukalitolea maelezo na kanuni zetu ziko wazi Mhe. Mwenyekiti. Kanuni ya 58 fasili ya 5 inaeleza wazi jambo ambalo tumelizungumza katika mkutano huu huu tu, tena bajeti iliyopita. Halafu leo tukilirudisha sidhani kama tutaweza kwenda mbele, ikiwa jambo tumelizungumza hapa kisha tukalitolea ufafanuzi tukasema twende mbele, halafu tukilirudisha sijui tena, maana kanuni zetu zinatukataza. Sijui kama hilo litatusaidia katika kuendesha shughuli zetu, na hasa katika kipindi hiki tuna shughuli nyingi na kubwa za kufanya. Mhe. Mwenyekiti, nilisema hilo nilitanabahishe tu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando alizungumzia suala la uwajibikaji wa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano katika suala la *MV Spice Islander*. Mhe. Mwenyekiti, hiki ni chombo kikubwa na utaratibu wake wa kufanya maamuzi basi unaweka kigezo cha maamuzi ambayo yatakuja baadae. Wanasheria kina Mhe. Jussa wanasema *precedent*. Sasa suala la uwajibikaji ndani ya Baraza hili kwa mawaziri na serikali ni kuhusiana na kwanza katiba, sheria, kanuni na taratibu ziliopo.

Mhe. Mwenyekiti, iliundwa tume na tume ile ripoti yake nadhani tuliipata, hakuna pahala popote paliposema Mhe. Waziri alivunja katiba, alivunja kanuni au alivunja sheria au alivunja utaratibu, hakuna popote. Sasa kilichobakia kusema kwamba *political responsibility*, uwajibikaji wa kisiasa jamani ni vizuri tuielewe kwanza dhana yenyewe na maana yake, dhana ya uwajibikaji wa kisiasa ni suala la mtu waliomchagua au waliomteua. Baraza hili mtu anaweza kuwajibishwa kama kavunja katiba, sheria, kanuni au utaratibu. Lakini *political responsibility* ni yeye na aliyemteua au ni yeye na waliomchagua, wakimuona hafai hawatomrudisha.

Lakini pia tunapitisha Sheria hapa za Mashirika na Idara ambavyo ni vitu tofauti, hiyo dhana ya *political responsibility.* Mimi naomba watu tukaisome na tuiangalie maana mwahala mwa kusoma tukajielimisha mumo. *Political accountability* maana yake kama una mashirika na shirika na idara ni vitu tofauti. Shirika na idara ni sawa na kuwa una watoto wako, mmoja ni wa chini ya umri na mwengine tayari ni mtu mzima. Sasa akifanya mtoto mdogo utajua namna ya kumchapa na pengine utawajibika, lakini akifanya mtu mzima huo wajibu wako unabaki ni wa kizee tu. Hiyo ndiyo mipaka ya *political responsibility* kwenye mashirika yaliyoundwa, maana tumeyapa sisi hadhi humu ndani. Kusema yatashtaki na kushtakiwa. Ndio maana ukishtaki shirika la umma lililoundwa kwa sheria, huhitaji kutoa *notice* ya siku 60 kwa serikali, kwa Mwanasheria Mkuu, bali unaishtaki moja kwa moja. Lakini ukiishtaki Idara ya serikali ni lazima utoe *notice* ya siku 60 umpe Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi, kwa nini? kwa sababu yule ni mtoto wa serikali aliyekuwa chini ya dhamana moja kwa moja ya serikali, na yule mmoja mwengine ni mtoto wako lakini anajitegemea.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tuna Shirika la Bandari na tuna ZMA ni sisi tumepitisha sheria ya kuwapa *Board Corporate* inabaki dhima, kwa sababu ni watoto wako. Lakini dhima ya kwamba wewe unawajibika moja kwa moja, hiyo dhima inapungua na ndio misingi inavyosema. Mimi naomba sana wenzangu tujielimishe katika hili na tutaona. Suala hili huko serikalini limezungumzwa sana, lakini tukasema huwezi kufanya maamuzi ni lazima uwe na msingi wa maamuzi katika hili. Kwa hivyo, sasa kama kuna mtu anaona sivyo hivi, hilo basi litakuwa ni lake yeye, na yeye lakini kwa misingi ya kisheria na kiutaratibu nadhani hilo sio la kusema kulazimishwa na Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo naomba nimalizie dakika mbili tu kwenye suala la Muungano. Mimi sikutaka niseme maana yake yamezungumzwa mengi. Lakini mimi naomba tu kuwatanabahisha wenzangu, pengine na kuwatanabahisha wananchi kwa jumla. Ni kwamba wayasikilize vizuri yale maneno ya Mhe. Hamza Hassan Juma alipokuwa anazungumza, sikuwemo humu ndani, lakini nilimsikiliza. Ile hesabu yake ya 30, 30 itakuja kutudhuru. Ile hesabu yake aliyoisema, mimi naomba watu waisikilize vizuri ya 30, 30 itakuja kutudhuru na itatudhuru namna gani. Itatudhuru kwa sababu, sisi naona ugomvi wetu umekuwa zaidi katika chombo cha kupakilia kile tunachokitaka. Nilidhani kwanza tutachuma tuseme jamani eeh! Machumo yetu ni haya tumepata gunia 100 hizi, sasa je gunia 100 hizi zitaingia kwenye gari moja au zitaingia kwenye gari mbili, au zitaingia kwenye gari tatu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa maana ya kwamba asiyeutaka Muungano ana sababu zake, kwa sababu ya mambo ambayo anahisi pengine haya na haya hayakutimizwa, na hata anayeutaka, anayeupenda na anayeuamini naye anaupenda na kuuamini kasoro, Muungano huu kwa mapenzi naupenda, lakini aah! Pamoja na mapenzi yangu lakini si kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, watu mkiwa na tofauti mkitaka kutengeneza pahala yaani msimamo unaofanana, haiwezekani kama alivyosema nadhani Mhe. Issa Haji Ussi Gavu, kwamba haiwezekani tukawa na *unify stand*, maana yake sote tunapigania jambo moja la maslahi. Sasa kama jambo la maslahi basi ni lazima mtafute mnapokubaliana, mkishakubaliana basi tofauti zenu ni rahisi kuzitatua. Lakini ila mmoja akishikilia kutafuta anagombana wapi na mwenzake, kila mmoja akishikilia tofauti yake na mwenzake, mimi nadhani hilo linaweza likawa ni tatizo. Tunaweza tukawapotosha watu, tukagombana kwa sababu ya jambo la kheri, badala ya kupatana katika kheri hii basi itakuwa ni jambo la ajabu kweli.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili moja nimalizie kwa kusema kwamba, mimi nadhani tusiiambie serikali ikawaambie watu nini cha kusema, mimi nadhani huu ni wajibu wa jamii, na tunaposema jamii kuna *professional society*, kuna jumuia mbali mbali, na zikitaka kuna wataalamu mbali mbali jumuia hizi wa kusaidia. Lakini serikali ikienda kujenga msimamo, basi unaweza ukaja baadae ukawa ugomvi baina ya serikali na watu wake, wale ambao wanasema mmh! Hili silo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani serikali ni kuwahimiza watu kama ilivyofanya, kuwahimiza watu jamani tufuate utaratibu katika hili, kuwahimiza watu waende, kuwatengenezea watu mazingira ya usalama wa kutoa maoni yao, lakini nadhani hii ni *responsibility* yetu sote, ya vikundi vya kijamii kuwafahamisha watu na kuwafahamisha bila ya kuwapotosha, bila ya kupeleka mbele maslahi yao binafsi, bali kuweka mbele maslahi ya nchi kwa ujumla. Fursa hii ikiwa itatugombanisha, basi sidhani kama itatokea fursa nyengine ya kutuunganisha tena.

Kwa hivyo, mimi naomba sana katika hili ni vyema tuwe makini. Niliwahi kusema na naomba nirejee. Waswahili wanasema, ‘ndege mjanja hunasa kwenye tundu bovu’. Tusipokuwa makini ujanja wetu wote Wazanzibari tutakuja kunasa kwenye tundu bovu. Mhe. Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja na naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa namna tulivyoshirikiana kwa pamoja, hadi tukaweza kufikia hapa tulipofikia, na ni matumaini yangu kwamba kesho asubuhi baada ya kipindi kifupi sana cha maswali na majibu, basi Mhe. Waziri atapata nafasi ya kufanya majumuisho, baadae tutaendelea na taratibu zetu kama tulivyokuwa tumezipanga mwanzo.

Baada ya maelekezo hayo sasa, kwa heshima na taadhima natangaza kwamba tunaliahirisha Baraza hili mpaka kesho siku ya Jumatano, tarehe 27/06/2012 saa 3:00 za asubuhi, ahsateni sana

(Saa 1:52 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 27/06/2012 saa 3:00 za asubuhi)